

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Sita – Tarehe 9 Februari, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):**

Magazeti ya Serikali na Nyongeza zake:-

1. Toleo Na. 14 la tarehe 03 Aprili, 2020;
2. Toleo Na. 15 la tarehe 10 Aprili, 2020;
3. Toleo Na. 16 la tarehe 17 Aprili, 2020;
4. Toleo Na. 17 la tarehe 24 Aprili, 2020;
5. Toleo Na. 18 la tarehe 01 Mei, 2020;
6. Toleo Na. 19 la tarehe 08 Mei, 2020;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

7. Toleo Na. 20 la tarehe 15 Mei, 2020;
8. Toleo Na. 21 la tarehe 22 Mei, 2020;
9. Toleo Na. 22 la tarehe 27 Mei, 2020;
10. Toleo Na. 23 la tarehe 05 Juni, 2020;
11. Toleo Na. 24 la tarehe 12 Juni, 2020;
12. Toleo Na. 25 la tarehe 19 Juni, 2020;
13. Toleo Na. 26 la tarehe 26 Juni, 2020;
14. Toleo Na. 27 la tarehe 03 Julai, 2020;
15. Toleo Na. 28 la tarehe 10 Julai, 2020;
16. Toleo Na. 29 la tarehe 17 Julai, 2020;
17. Toleo Na. 30 la tarehe 24 Julai, 2020;
18. Toleo Na. 31 la tarehe 31 Julai, 2020;
19. Toleo Na. 32 la tarehe 07Agosti, 2020;
20. Toleo Na. 33 la tarehe 14 Agosti, 2020;
21. Toleo Na. 34 la tarehe 21 Agosti, 2020;
22. Toleo Na. 35 la tarehe 28 Agosti, 2020;
23. Toleo Na. 36 la tarehe 4 Septemba, 2020;
24. Toleo Na. 37 la tarehe 11Septemba, 2020;
25. Toleo Na. 38 la tarehe 18 Septemba, 2020;
26. Toleo Na. 39 la tarehe 25 Septemba, 2020;
27. Toleo Na. 40 la tarehe 2 Oktoba, 2020;
28. Toleo Na. 41 la tarehe 9 Oktoba, 2020;
29. Toleo Na. 42 la tarehe 16 Oktoba, 2020;
30. Toleo Na. 43 la tarehe 23 Oktoba, 2020;
31. Toleo Na. 44 la tarehe 30 Oktoba, 2020;
32. Toleo Na. 45 la tarehe 06 Novemba, 2020;
33. Toleo Na. 46 la tarehe 13 Novemba, 2020;
34. Toleo Na. 47 la tarehe 20 Novemba, 2020;
35. Toleo Na. 48 la tarehe 27 Novemba, 2020;
36. Toleo Na. 49 la tarehe 4 Disemba, 2020;
37. Toleo Na. 50 la tarehe 11 Disemba, 2020;
38. Toleo Na. 51 la tarehe 14 Disemba, 2020;
39. Toleo Na. 52 la tarehe 25 Disemba, 2020;
40. Toleo Na. 01 la tarehe 01 Januari, 2021;
41. Toleo Na. 02 la tarehe 08 Januari, 2021;
42. Toleo Na. 03 la tarehe 15 Januari, 2021;
43. Toleo Na. 04 la tarehe 22 Januari, 2021; na
44. Toleo Na. 05 la tarehe 29 Januari, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Casato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 73

**Kituo cha Uwekezaji TIC**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Kituo cha Uwekezaji (TIC) kinampa haki mwekezaji kuajiri wataalam lakini upande wa pili sheria inampa mamlaka Kamishna wa Kazi kufanya maamuzi kuhusu maombi ya vibali vya kazi:-

Je, ni lini Serikali italeti marekebisho ya sheria ili kuondoa mgongano huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili, naomba nichukue fursa hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Shinyanga ambao walinichagua kwa kishindo. Pia nikishukuru zaidi Chama cha Mapinduzi, wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa kishindo nchi nzima usio na mashaka yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pole kwa wananchi wa Shinyanga kwa kupotelewa na Mwenyekiti Mstaafu wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Erasto Kwilasa. Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kufungua milango kuwavutia wawekezaji kuwekeza nchini. Serikali kupitia Sheria ya Uwekezaji, Sura 38 kama ilivyofanyiwa marekebisho na marejeo yake mwaka 2015 inatoa motisha mbalimbali (*incentives*) kwa wawekezaji. Miongoni mwa motisha hizo ni kuwaruhusu wawekezaji kuajiri wataalam wa kigeni watano, kwa lugha ya kigeni inaitwa *Immigration Quota* wakati wa hatua za awali za utekelezaji wa miradi yao (*startup period*) inapoanza kufanyika chini ya kifungu cha 24 cha Sheria ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulinda uchumi wetu, ajira za wazawa, maslahi na usalama wa nchi yetu, Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na.1 ya mwaka 2015 kupitia kifungu cha 5(1)(b) na 11 kinampa Kamishna wa Kazi mamlaka ya kusimamia ajira za raia wa kigeni nchini kwa lengo la kuhakikisha ajira zinazotolewa kwa wageni ni zile ambazo sifa za kielimu, ujuzi, uzoefu wa kazi ni adimu hapa nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamishna wa Kazi hupokea na kuchambua maombi ya vibali vya kazi vya raia wa kigeni kutoka kwenye kampuni/taasisi zinazohitaji kuajiri wageni wanaokidhi vigezo na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamishna wa Kazi ameendelea kuzingatia sheria zote, taratibu, sera na kanuni katika kufikia maamuzi yake. Napenda kumhakikishia

Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge katika kupokea maoni na mapendekezo yanayolenga mabadiliko ya sheria na sera ili kuimarisha zaidi uwekezaji nchini bila kuathiri matakwa ya sera, sheria, taratibu na kanuni na miongozo iliyowekwa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana kabisa na Serikali kwamba ina wajibu wa kulinda ajira za Watanzania kwanza, ndiyo *priority*. Hata hivyo, Sheria hii ya Uwekezaji sababu ya kutoa nafasi hizo tano *automatic* mojawapo ilikuwa ni hiyo *trust* ambayo mwekezaji anayo kwa wale watu watano bila kujali sifa walizonazo ni adimu au siyo adimu. Kwa mfano, watu wa *finance* mtu amewekeza mradi wake wa milioni mia moja *in any way* hata kama huyu mtu hana CPA...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Swali la kwanza, ni lini Serikali ita-*harmonize* hizi sheria mbili ili kutengeneza mazingira bora ya uwekezaji ili kuendana na kasi ya kuvutia wawekezaji nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kwa sasa vibali vile *life span* yake ni ya muda mfupi mfupi na baadhi ya uwekezaji ni wa muda mrefu, je, Serikali iko tayari kuongeza *life span* ya vibali vile katika kuvutia wawekezaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika,

naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kuhusiana na mabadiliko ya sheria, mabadiliko ya sheria hufanyika pale tija inapoonekana. Katika mazingira ya sasa, Sheria ya Uwekezaji tuliyonayo, Sura 38, inatoa nafasi ya mwekezaji kuweza kupata watu watano kwa maana *immigration quota*. Watu hao watano wanapewa bila masharti yoyote, yeye ndiye atakayewachagua na hakuna hayo matakwa anayosema yapo kwa maana ya kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ni sehemu ya *incentive* au motisha. Katika kufanya hivyo, mwekezaji baada ya kuwa amekidhi vigezo vyote atakuwa na uhuru wa kuweka watu wake hao watano. Hiyo ni kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria inayohusiana na kuratibu ajira za wageni, yenyewe pia inatoa tu utaratibu na mwongozo mzuri wa *local content* katika kulinda uchumi wa nchi yetu lakini pia kulinda ajira za wazawa. Sasa katika mazingira haya ukiacha goli wazi, kwa sehemu kubwa uzoefu unaonyesha kila mwekezaji angependa kufanya kazi na watu ambao ni wa kutoka nje. Tuna taarifa kwamba wapo pia wawekezaji wanapata mikopo kutoka kwenye mabanki mbalimbali na masharti inakuwa ni kuajiri raia wa huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Serikali yetu tunawekeza sana kwenye elimu, tuna mpango wa elimu bila malipo ambapo Serikali inatoa fedha nyingi katika sekondari lakini pia vyuo vikuu tunatoa mikopo, vijana hawa wanapomaliza vyuo na ajira hizo zikichukuliwa na wageni inakuwa ni changamoto kwa nchi. Ndiyo maana kwa ikatungwa sheria hiyo udhibiti ili kuhakikisha kwamba ajira za wazawa zinalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake dogo la pili kuhusu *life span* ya *permit*, nimweleze tu Mheshimiwa kwamba nalo

limezingatiwa vizuri na sheria za sasa zinatoshia kabisa katika kuelezea hilo. Mwekezaji nchini mbali na kupewa idadi ya watu watano ambao wanaweza kufanya nao kazi, Sheria ya Uwekezaji inatoa muda wa kipindi cha miaka mitano lakini pia akiombea kupitia *T/C* anapewa kipindi cha miaka kumi. Katika miaka hii kumi na yule anayepewa miaka mitano imewekwa katika awamu ili kuhakiki na kujiridhisha kwamba kweli bado ajira hiyo ni adimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka miwili anapata *permit* yake ya kwanza ambapo atahitaji kuwa na *succession plan* aturidhishe kwamba kuna Mtanzania nyuma anajifunza kazi hiyo ya kitaalamu ili hata baadaye hata akiondoka nchini tuweze kubaki na wataalamu. Atapewa tena awamu ya pili miaka miwili na mwisho atapewa *final grant* kwa maana ya kufikisha miaka mitano. Mazingira hayo yote yanaangaliwa na wakati mwingine wamekuwa wakikata rufaa ofisi ya Waziri mwenye dhamana na zimekuwa zikitolewa kwa kupima mazingira yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mpaka sasa hitaji la kubadilisha sheria halijaonekana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana ameshaelewa.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la muhimu hapa, Mheshimiwa Umy Mwalimu atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporejea Dodoma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Umy tafadhali hamia karibu na kiti anachokalia Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, majibu ya ziada.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu kuongezea kidogo kwenye majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali pia ipo katika mchakato wa kufanyia marekebisha Sheria ya Uwekezaji. Pamoja na mambo mengine tutayaangalia baadhi ya mambo Mheshimiwa

Mbunge ameya-raise hapa. Pia Waheshimiwa Wabunge watapata nafasi ya kuipitia sheria hiyo na kama kuna maeneo ya kuimarisha basi itakuwa ni fursa nzuri ya kuweza kurekebisha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 74

### **Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Novemba, 2015 hadi Septemba, 2020, Serikali imejenga Hospitali 101 za Halmashauri na kuongeza idadi ya Hospitali za Halmashauri kutoka Hospitali 77 zilizokuwepo mwaka 2015 hadi Hospitali 178 Septemba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kigezo muhimu kwa Halmashauri kupata fedha za ujenzi ilikuwa ni kuandaa eneo la ujenzi. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ilikosa fedha za



ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri kwa kuwa hadi wakati wa tathimini ya Halmashauri zilizotenga maeneo ya ujenzi, Hospitali ya Halmashauri ya Mbinga ilikuwa haijapata eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 27 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 27 mpya nchini. Aidha, kwa kuwa sasa tayari Halmshauri ya Wilaya ya Mbinga imebainisha eneo la ujenzi, Serikali itaipaa kipaumbele sambamba na Halmashauri nyingine ambazo hazina Hospitali za Halmashauri kwenye awamu zinazofuata kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali japo siridhiki nayo kwa sababu maeneo ya kujenga Hospitali ya Wilaya katika Jimbo la Mbinga Vijijini yapo mengi katika maeneo tofauti tofauti, ni uamuzi tu wapi tujenge hospitali hiyo. Je, Serikali inawahakikishia nini wananchi wa Mbinga Vijijini katika bajeti ijayo ikiwa bajeti mbili tofauti zimepangwa na hizi fedha hazikupelekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wananchi wa Mbinga Vijijini kwa kuunga mkono juhudi za Serikali wamejenga na kukamilisha zahanati sita; zingine zina miaka miwili toka zikamilike. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka wahudumu katika zahanati hizi ili zifunguliwe zianze kuwahudumia wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kujibu kwenye swali la msingi, kigezo muhimu cha kupeleka fedha katika Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Halmashauri ambacho Serikali iliweka ilikuwa ni Halmashauri husika kuainisha eneo na kuwasilisha taarifa ya uwepo wa eneo husika ndipo fedha ziweze kupelekwa kwenye Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mbinga Vijijini imekuwa na mivutano ya muda mrefu kuhusiana na wapi Makao Makuu ya Halmashauri iwepo. Januari hii wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipopita ndipo ilipata majibu ya kuwa na Makao Makuu ya Halmashauri yawepo. Kwa sababu hizo, hawakuwa na eneo rasmi ambalo liliwasilishwa Serikalini na ndiyo maana fedha haikupelekwa. Hata hivyo, kwa sasa, kama nilivyosema kwa sababu wamekwishawasilisha eneo ambalo limetengwa, katika shilingi bilioni 27 ambazo zimetengwa na Serikali, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba watapata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mbinga Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na zahanati sita ambazo zimekamilika na hazijaanza kutoa huduma kwa sababu ya upungufu wa watumishi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Kapinga kwamba Serikali inathamini sana kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa Mbinga Vijijini. Kwa sababu zahanati hizi zimekamilika tutakwenda kuona utaratibu mzuri kwanza kwa kutumia watumishi waliopo ndani ya halmashauri kufanya *internal redistribution* ya watumishi hao angalau kuanza huduma za afya. Katika kibali cha ajira kinachokuja Halmashauri ya Mbinga Vijijini tutawapa kipaumbele ili watumishi hao waweze kwenda kutoa huduma katika zahanati hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo. Kwa kuwa na sisi watu wa Makete tuna changamoto ya hospitali ya wilaya toka mwaka 1982 kituo cha afya kilivyopandishwa

hadhi kuwa hospitali ya wilaya, hadi sasa hatuna hospitali ya wilaya. Je, ni lini Hospitali ya Wilaya ya Makete itanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, kiasi cha shilingi bilioni 27 kimetengwa kwa ajili ya kujenga hospitali za halmashauri zile ambazo ni chakavu, tutajenga hospitali za halmashauri mpya na Halmashauri ya Makete ni miongoni mwa halmashauri ambazo tutakwenda kutenga fedha na kuhakikisha kwamba ujenzi wa hospitali ya halmashauri unaanza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza dogo, kwamba Jimbo la Ndanda lenye kata 16 lina Kituo cha Afya kimoja tu cha Chiwale. Hata hivyo wananchi wa Ndanda, Lukuledi, Panyani, Mihima pamoja na Chilolo walijitahidi kwa kutumia nguvu zao pamoja na nguvu ya Ofisi ya Mbunge kujenga maboma kwa ajili ya zahanati na mengine kituo cha afya. Nini kauli ya Serikali kuhusu kuwapokea wananchi mzigo huu wa kukamilisha maboma haya ili yaweze kutumika na kutoa huduma za afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Ndanda kwa kujitolea nguvu zao na kuanza ujenzi wa zahanati na vituo vya afya na hiyo ni kauli ya Serikali ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaibua miradi na Serikali inaunga nguvu miradi hiyo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka huu wa Fedha 2020/2021, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 27.75 ambazo zitakwenda kufanya kazi ya kuchangia nguvu za wananchi katika kukamilisha ujenzi wa maboma 555 nchini kote. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mwambe kwamba jimbo lake na vijiji na kata husika zipo katika mpango huu na Serikali itahakikisha inatoa mgao kwa ajili ya umaliziaji wa vituo hivyo ili viweze kutoa huduma kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile swali la msingi linalohusu Mbinga Vijijini linafanana kwa kiasi kikubwa na tatizo la Madaba na kwa vile Madaba ilishatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na kwa vile kwa miaka miwili mfululizo fedha hiyo haijatoka. Ni lini sasa Serikali itapeleka fedha Madaba ili ujenzi wa hospitali ya wilaya uanze?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mbunge wa Madaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za halmashauri.

Katika kipindi cha miaka mitano sote tumeona kazi kubwa iliyofanyika kwa kujenga hospitali za halmashauri zaidi ya 101 na katika mwaka huu wa fedha, kiasi cha shilingi bilioni 27 zimetengwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika vituo na hospitali za halmashauri ambazo zitajengwa Jimbo lake la Madaba pia litapewa kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe.

Na. 75

### **Chumba cha Kuhifadha Maiti – Hospitali ya Mbogwe**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itajenga chumba cha kuhifadha maiti kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali ya halmashauri. Majengo yaliyohusika katika awamu

ya kwanza ni jengo la wagonjwa wa nje na maabara. Ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 60.5 ambapo kiasi cha shilingi 33.5 ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali za halmashauri 67 nchini na kiasi cha shilingi bilioni 27 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za halmashauri 27 mpya ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe iliyotengewa kiasi cha shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe inaelekezwa pamoja na majengo mengine, kujenga jengo la kuhifadhi maiti pindi itakapopokea fedha za ujenzi kwa kuwa tayari ina majengo mawili kati ya majengo saba yanayotakiwa kujengwa na hivyo fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2020/2021 itakuwa sehemu ya fedha ya kujenga jengo la kuhifadhi maiti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali langu la nyongeza; ni lini sasa Serikali itatoa vifaa vya upimaji kwenye wilaya ya Mbogwe? Maana Wilaya ya Mbogwe inakua na ina watu wengi sana, lakini hatuna vipimo vya *x-ray* pamoja na vipimo vingine. Kwa hiyo wananchi wa Mbogwe wamekuwa wakipata taabu sana wanapopata ajali wale waendesha bodaboda na watu wengine; ni lini Serikali inawahakikishia wananchi wangu wa Mbogwe kwamba itapeleka hivyo vifaa vya upimaji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 33.5 kwa ajili ya kwenda kuongeza nguvu za kununua vifaa tiba katika hospitali mpya 67 za halmashauri kote nchini.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Hospitali ya Halmashauri ya Mbogwe ni moja ya hospitali ambazo zitanufaika na bajeti hii kwa kupata kiasi cha shilingi milioni 500 kadri ya fedha itakavyopatikana ili ziweze kununua vifaa tiba kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 76

### **Wanufaika wa Mfuko wa TASAF**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi wa Manispaa ya Bukoba kuwa wanufaika wa TASAF ni wananchi wenye uwezo badala ya kaya maskini:-

Je, hayo ndiyo malengo ya kuanzishwa kwa TASAF?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nami ndiyo mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu, napenda kuanza kwa kumshukuru Mungu kwa mema yote ambayo anaendelea kutujalia hadi kufika siku hii ya leo. Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa

Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa imani yake kwangu na kuiteua kuwa Naibu Waziri katika ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mpango wa *TASAF* ni kuzinusuru kaya maskini katika Halmashauri zote za Tanzania Bara na Unguja na Pemba kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini ulianza rasmi mwaka 2000 hadi 2005; awamu ya pili ilianza mwaka 2005 hadi 2012; na awamu ya tatu, kipindi cha kwanza ilianza kutekelezwa mwaka 2013 hadi Desemba, 2019; na kipindi cha pili cha awamu ya tatu kilianza Februari, 2020 hadi Septemba, 2023 ambapo jumla ya kaya maskini 1,100,000 zimeweza kuandikishwa na wanufaika kunyanyua hali yao ya kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kagera jumla ya kaya maskini 68,915 zimeandikishwa na kuingizwa kwenye Mpango huu wa *TASAF*. Katika utekelezaji wa kipindi cha kwanza walengwa wamepokea ruzuku kwa takribani miaka mitano. Hali hii imechangia walengwa hawa kuwa na miradi mikubwa ya uzalishaji mali kama mashamba, mifugo na shughuli za ujasiriamali ambazo zimewawezesha wao kuboresha maisha na kujiimarisha kiuchumi. Walengwa kama hao ndio wanalalamikiwa kuwa *TASAF* inasaidia watu wenye uwezo badala ya kaya maskini. Ukweli ni kwamba kaya hizo ziliingia kwenye mpango zikiwa na hali duni na ziliweza kujikwamua kiuchumi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.



**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri na ya kina. Maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo: Swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kanzidata kwa kutumia TEHAMA ili kuhakikisha kwamba wanaonufaika ni wale ambao wanakidhi vigezo vilivyowekwa na pia kuondoa mianya ya watu wanaonufaika kusajiliwa mara mbili kwenye maeneo tofauti?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, ni je, sasa Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba kaya ambazo hazikunufaika awali sasa zitanufaika katika hii Awamu ya *TASAF III*, hususan wazee siyo tu wa Bukoba Manispaa, Mkoa wa Kagera bali wa Taifa kwa ujumla? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mpango huu wa kuanzisha kanzidata ya walengwa wote wanaopokea fedha za *TASAF* imeanza. Mwanzo ilianza katika halmashauri 19 nchini lakini hadi hivi ninavyoongea tayari imekwenda katika halmashauri 39 na tayari tunaanza kuweka mfumo kwa ajili ya kuunganisha na *NIDA*, kuunganisha na mitandao yetu ya simu ili walengwa hawa badala ya kupokea fedha hizi dirishani kwa wale wanaokwenda kugawa, fedha hizi ziende moja kwa moja kwenye simu zao. Tutafanya hivi ili kuhakikisha kwamba hakuna kwanza *double payment* katika suala hili, kwa sababu kuna maeneo ambayo watu huwa wanalalamika mtu anapokea mara mbili au mtu akiwa hayupo watu wengine wanachukua zile fedha. Sasa ili kudhibiti hilo ndiyo maana tunakwenda sasa katika ku-*roll out* hii katika halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na tuta-*roll out* katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali lake la pili, kwamba ni lini Serikali sasa itatanua mpango huu kwa wazee ambao hawakuvingia na kaya ambazo hazikuvingia. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge yeye wa Viti Maalum anafahamu anatoka Kagera, lakini hata wa Jimbo la Bukoba Mjini Mheshimiwa Byabato anafahamu kwamba sasa kaya zote katika Awamu hii ya Pili ya *TASAF* zinakwenda kuingia kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwatoe mashaka Wabunge wote wa Majimbo humu ndani na wa Viti Maalum kwamba mpango huu unakwenda kwenye kaya 1,400,000 ambayo ni sawasawa na watu milioni saba wanakwenda kunufaika na Mpango huu wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimeona kuna Mbunge amesimama pale, tafadhali jitambulishe. Simama ujitambulishe, halafu uliza swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge kutoka Kibaha Vijijini. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, najua *TASAF* ilianza awamu ya kwanza kwa kuwapatia walengwa miradi ya uwekezaji kama majengo mbalimbali zikiwemo kumbi za maonyesho. Katika Jimbo la Kibaha Vijijini, wazee walipewa mradi huu awamu ya kwanza; je, *TASAF* wana mkakati gani juu ya kuwafanyia ukarabati jengo ambalo walipewa katika awamu ya kwanza ambalo sasa limechakaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

naomba kutumia nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge, awamu ya kwanza ilijikita zaidi katika ujenzi wa miundombinu na si Kibaha Vijijini tu bali katika halmashauri nyingi sana katika nchi yetu ambazo majengo haya au miradi hii ilifanyika. Sasa baada ya awamu ya kwanza kuisha na kwenda awamu ya pili na sasa tuko awamu ya tatu *phase II*, ni kwamba majengo haya na miradi hii yote ilikabidhiwa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri husika. Na ni wajibu wa Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba wanatunza majengo haya na wasiwaachie tu wale walengwa peke yao; ni wajibu wa Wakurugenzi kuhakikisha *sustainability* ya miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kuelekea katika halmashauri yake na kuhakikisha tunakwenda kuangalia miradi hiyo na kuwaagiza Wakurugenzi ili kuhakikisha kunakuwa na *sustainability*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.  
(*Makoff*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai.

Na. 77

### **Kuongeza Idadi ya Watumishi wa Afya 403**

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE** aliuliza:

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni ya kuongeza watumishi 403 wa afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka ya 2015 hadi 2020, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 14,479 wa kada mbalimbali za afya. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali inatarajia kuanza kuajiri watumishi 75 wa kada mbalimbali za afya kwenye Wilaya ya Hai kwa ajili ya hospitali ya wilaya moja, vituo vya afya sita na zahanati 28 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, majibu ambayo kimsingi yatapunguza maumivu makubwa waliyopata wananchi wa Hai tarehe mbili kutokana na majibu ya swali lao kuhusu suala la ushirika. Niwaambie wananchi wa Hai watulie Serikali yao inawapenda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niulize swali la nyongeza la kwanza; kwa kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa wananchi wa Hai tarehe 28 walifanya jambo lao kwa asilimia kubwa sana na kuleta utulivu humu Bungeni na huko nje; je, ni lini sasa Serikali itatekeleza kwa kiwango angalau cha asilimia 50 ya ahadi ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali italipa madeni ya watumishi wa afya na Walimu ambao ni wastaafu, deni ambalo mimi mwenyewe nimeshaliwasilisha

kwa Mheshimiwa Waziri la milioni 171 ili watumishi wa afya waendeleo kufanya kazi yao kwa uaminifu? Ikingatiwa miongoni...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umeshauliza swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameuliza ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi ya kuajiri watumishi wa afya japo kwa asilimia 50. Bunge lako Tukufu na Wabunge wote humu ni mashuhuda wa jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kujenga Hospitali za Wilaya, kuongeza vituo vya afya na zahanati. Hivyo basi, pale ambapo bajeti itaruhusu, tutaendelea kuajiri watumishi katika Idara ya Afya; na hawa 75 wanaokwenda Hai, ni sawa na asilimia 18.6 ya watumishi wote ambao wameajiriwa hivi sasa. Kwa hiyo, kadri uwezo utakavyoruhusu, tutaendelea kuleta watumishi katika Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili juu ya madeni ya watumishi, Mheshimiwa Mbunge kwanza amekuwa mstari wa mbele kupigania haki za hawa watumishi na ili jambo amenieleza mimi mwenyewe zaidi ya mara mbili. Tayari tunashughulikia, ukiacha deni ambalo alikuwa analizungumzia la shilingi milioni 171, tayari yalikuja maombi 137 katika Ofisi ya Rais Utumishi yenye jumla ya thamani ya shilingi milioni 246 ili yaweze kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa madeni yaliyolipwa ni Sh.50,690,000/= na madeni yenye thamani ya shilingi milioni 148 ambayo ni sawa na watu 88, yamerudishwa kwa mwajiri ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Hai kwa sababu yalikuwa na dosari mbalimbali. Pale ambapo Mkurugenzi wa Hai atarekebisha dosari zile na kuzileta katika

Ofisi ya Rais Utumishi, basi nasi tutazifanyia uhakiki tuweze kulipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna madeni ya watu 27, sawa na shilingi milioni 33 na kitu hivi, tayari yameshafanyiwa uhakiki na yametolewa katika Ofisi ya Rais, Utumishi na sasa yapo Wizara ya Fedha, tayari kwa malipo muda wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Lushoto ina uhaba mkubwa sana wa watumishi katika sekta ya elimu na afya. Katika sekta ya elimu, msingi peke yake ambapo tuna shule 168, tuna uhaba wa watumishi 1,274. Tuna vituo 63 vya kutoa huduma za afya lakini tuna uhaba wa watumishi 1,218. Ni lini Wizara hii itaiangalia Halmashauri ya Lushoto kwa jicho la huruma na kutuondoa katika kadhia hii ambayo wananchi wanaendelea kupata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri walimu kadri bajeti itakavyoruhusu. Katika bajeti ya mwaka 2021, Serikali ilitenga bajeti ya ajira 9,500 kwa walimu na watumishi katika kada ya afya 10,467. Hivyo basi, pale Serikali itakapoanza kuajiri hawa, tutaangalia pia na Mlalo kule ili aweze kupata watumishi hawa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Esther Nicolas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 78

### **Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria**

**MHE. ESTHER NI. MATIKO** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Tarime utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mji Mdogo wa Tarime wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia Mradi wa Maji wa Mserereko Nyandulumo; visima vitatu Rebu, Jeshi la wokovu na Viambwi, na bwawa la maji Tangota. Vyanzo hivi vyote vinazalisha wastani wa lita 1,200 kwa siku wakati jumla ya mahitaji ni lita 6,000 za maji kwa siku. Utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria utaweza kuhudumia maeneo yote ya mji wa Tarime kwa kuzalisha wastani wa lita 6,500 kwa siku ambazo ni zaidi ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Tarime, Serikali imepata mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim jumla ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Moja ya miji itakayonufaika na mkopo huo ni Mji wa Tarime ambao utatumia chanzo cha Ziwa Victoria. Kwa sasa mradi upo katika hatua za manunuzi ya wakandarasi wanaotarajiwa

kuwepo eneo la mradi ifikapo mwezi Aprili, 2021 na ujenzi wa mradi unatarajiwa kuchukua miezi 24.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicolas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali imekiri kabisa kwamba wananchi wa Tarime asilimia 20 ndiyo wanaopata maji. Tatizo la maji ni Tanzania nzima. Sasa napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa miradi ya muda mfupi; visima virefu, Mradi wa Bwawa la Nyanduma ambalo tumekuwa tukilitengea fedha lakini haziendi na miradi mingine kama ya Gamasala na kwingineko kwa Tarime Mji, napenda kujua, ni lini Serikali itaenda kuchimba vile visima 23 ambavyo wameahidi kuanzia mwaka 2016 viweze kuwa suluhisho la muda mfupi kwenye Kata ya Kitale, Nyandoto, Kenyamanyoli na Mkende wakati tunasubiria Mradi wa Ziwa Victoria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, jana wakati wameweka Mpango hapa, Serikali imekiri kabisa kwamba imepeleka maji vijijini kwa asilimia 70.1, wamechimba visima miradi 1,423 ambapo kuna vituo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther, naomba uulize swali tafadhali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Miradi hiyo ina vituo 131,000. Kwa Rorya tuna mradi mkubwa kule Kirogo ambao umetumia zaidi ya shilingi bilioni 1.3, ulitakiwa kuwa na vituo 23...

**NAIBU SPIKA:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** ... lakini kuna vituo vitatu tu ambavyo vinatoa maji. Ni lini sasa Serikali itahakikisha maji yanatoka kule Kirogo kwa vituo vyote 23 na siyo vituo vitatu tu? *(Makofi)*



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi, salama na ya kutosheleza kwa maeneo yote ya nchi yetu ya Tanzania. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri alikuwa ziarani hapo Tarime na aliweza kuwasiliana na kuambatana na Mbunge wa Tarime Mjini ambaye ni Mheshimiwa Kembaki na Mbunge wa Tarime Vijijini, Mheshimiwa Naibu Waziri Waitara na Mheshimiwa Waziri ametoa ahadi hivyo visima vyote vitachimbwa ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano. Kwa kuanza, katika mwaka wa fedha ujao, visima vitachimbwa na maji safi na salama yatapatikana bombani kwa wananchi wote wa Tarime. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa ziara yake aliyofanya ndani ya Jimbo langu la Rorya ikiwa ni pamoja na maelekezo ya Mradi wa Kirogo kwamba mkandarasi aliyetekeleza ule mradi kwa kiwango cha chini achukuliwe hatua. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa maamuzi makubwa na mazuri aliyoyafanya kipindi alipofanya ziara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu wa maji unaotoka Ziwa Victoria kwenda Tarime unaanzia ndani ya Jimbo langu la Rorya, zaidi ya Kata 11 na vijiji zaidi ya 28 vinategemea kufaidika na mradi huu. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuanza kutekeleza mradi huu hata kama ni kwa awamu ili kutatua changamoto za mradi huo wa maji

ambao kimsingi utashughulika na Jimbo la Rorya, Tarime Vijijini na Tarime Mjini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali tumeweka mikakati kuhakikisha tunaondoa changamoto ya maji kwenye maeneo yote yenye shida hiyo. Kwa Jimbo la Rorya, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge, tayari Wizara iko kwenye michanganuo ya kuleta fedha katika maeneo hayo. Vilevile nimwambie tu kwamba baada ya Bunge hili, fedha awamu hii inayofuata, Jimbo lake pia limezingatiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa Reuben swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa miaka mingi wananchi wa Jimbo la Handeni Mjini wamekuwa wakiishi katika dhiki kubwa ya maji. Ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji wa Handeni Trunk Main kutoka Mto Ruvu kwenda Handeni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda kumpongeza Naibu Waziri wangu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anayelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo ya mgonjwa. Mimi naishi Tanga, najua moja ya changamoto kubwa ni eneo la Handeni. Serikali imeainisha miji 28 na tumeshapata Dola milioni 500 kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa tuko katika hatua ya manunuzi. Ndani ya mwezi Aprili, Wakandarasi wote watakuwa *site* kuhakikisha tunajenga miradi mikubwa ya maji. Hii ni katika kutimiza azma ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kumtua mwanamama ndoo kichwani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria umeshafika Mkoani Tabora. Jimbo la Tabora Mjini ni moja kati ya wanufaika wa mradi huo. Je, ni lini Serikali itanza usambazaji wa maji katika Jimbo la Tabora Mjini ili wananchi wa maeneo ya pembezoni ambao hawana maji kabisa waweze kunufaika na mradi huu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Moja ya ahadi kubwa sana kwa wananchi wa Tabora ni kuyatoa maji ya Ziwa Victoria na kuyaleta Tabora. Ni jambo kubwa ambalo amelifanya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na ahadi hiyo imetimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni wa zaidi ya shilingi bilioni 600, nasi kama Wizara mradi huu tumeukamilisha na tume-*save* zaidi ya shilingi bilioni 25. Fedha zile zilizobaki zote zitatumika kwa ajili ya usambazaji wa maji, wananchi wote ambao hawana maji katika Mkoa wa Tabora wataweza kupata huduma ya maji. Kazi hiyo imekwishaanza na wakandarasi wako *site* kwa ajili ya uendelezaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Rwakajunju ulioko Karagwe, nimeshauliza sana maswali katika Bunge la Kumi na Moja na mara zote huwa najibiwa kwamba mradi huo utatekeleza hivi karibuni lakini hadi sasa bado haujatekelezwa. Nini majibu ya Serikali kuhusu mradi huu ili kuwatua ndoo akina mama wa Karagwe? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu utatekelezwa kwa awamu katika mwaka wa fedha wa 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

Na. 79

### **Ukamilishaji wa Mradi wa Maji – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, lini utekelezaji wa mradi wa maji kwa vijiji 57 vya Wilaya ya Kyerwa utanza kwa kuwa usanifu wa kina wa mradi huo umeshakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebba Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Kyerwa, Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia Programu ya *PforR* na Programu ya Malipo kwa Matokeo (*PBR*) imetekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Nkwenda, Rugasha, Kitwechenkura, Kaikoti, Rwensinga, Kagenyi pamoja na sehemu ya Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mwaka huo, ukarabati wa visima virefu na vifupi umefanyika katika vijiji vya Kibale, Nyamiaga, Magoma, Rutunguru, Kihinda, Rwenkende, Kyerwa, Mirambi na Nyakakonyi ambapo wananchi wapatao 51,025 wananufaika na huduma ya maji safi. Utekelezaji wa miradi katika vijiji tajwa hapo juu ni sehemu ya utekelezaji wa miradi katika vijiji 57.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha vijiji vilivyobaki kati ya 57 vya Wilaya ya Kyerwa vinapata huduma ya maji, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.56 kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 12 vya Runyinya, Nkwenda, Nyamweza, Rwabwere, Karongo, Iteera, Muleba, Chanya, Muhurile, Kimuli, Rwanyango na Chakalisa. Pia vijiji hivi viko ndani ya mradi wa vijiji 57.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali itaendelea kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 35 vilivyobaki ili kukamilisha utekelezaji wa mradi wa vijiji 57. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa juhudi za kuwapatia wananchi wa Kyerwa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza maswali, kwenye majibu aliyotujibu, kuna sehemu ambayo haiko sahihi. Vijiji vya Kibale, Nyamiaga na Magoma hakuna kisima ambacho kimechimbwa. Kwa hiyo, hiyo taarifa aliyonipa siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, huu mradi ni muhimu sana kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Kyerwa. Mheshimiwa Waziri ananihakikishia kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 atatenga fedha kwa ajili ya mradi huu ili uweze kutekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ziko Kata ambazo haziko kwenye huu mradi, Kata za Bugomora, Kibale, Murongo pamoja na Businde. Serikali ina mpango gani wa kuzipatia maji Kata hizi ili nao watoke kwenye adha wanayoipata? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Bilakwate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza kuhusu kutengwa fedha kwa mwaka wa fedha ujao kwa mradi huu mkubwa, azma ya Serikali ni kuhakikisha miradi hii yote tunaitekeleza kwa wakati. Hivyo, katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022 mradi huu utapatiwa fedha kwa awamu na utekelezaji wake utaanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge, napenda tu kusema kwamba tutahakikisha maeneo yote yenye matatizo ya maji,

maji yanapatikana. Kwa mradi huu mkubwa ambapo bomba kubwa litapita, michepuo ya maji pia itazingatiwa; na kwa maeneo ambayo michepuo haitafika kwa urahisi, basi uchimbaji na ujenzi wa visima utazingatiwa katika mwaka wa fedha ujao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo na swali la Mheshimiwa Yahya Ali Mhata, Mbunge wa Nanyumbu.

Na. 80

### **Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma Kwenda Nanyaka**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, ni lini utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kwenda Mji wa Manyaka utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ali Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepata mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim jumla ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika miji 28 Tanzania Bara na Zanzibar. Moja ya mji unaonufaika na mkopo huu ni Mji wa Mangaka. Kwa sasa mradi upo katika hatua za manunuzi na wakandarasi wanatarajiwa kuwepo eneo la mradi kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi ifikapo Mei, 2021 na utekelezaji ni muda wa miezi 24.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ali Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali ila naomba yafanyike masahihisho. Ni Mji wa Mangaka, sio Banyaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu mawili ni kama ifuatavyo; la kwanza; kwa kuwa Mradi huu wa kuvuta maji kutoka Mto Ruvuma kwenda Mji wa Mangaka unaanzia Kata ya Masuguru, unapita Nanyumbu, Chipuputa, Kilimanihewa hadi Sengenya ambapo matenki yatajengwa. Swali, je, vijiji vitakavyopitiwa na bomba hili vitanufaika vipi na mradi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tunatambua kwamba mradi huu utachukua miaka miwili na wananchi wa Jimbo langu wana shida kubwa ya maji. Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuwanusuru wananchi hawa wakati wanasubiri mradi kukamilika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza, kwa sababu Mradi wa Ruvuma utapita kwenye hizi Kata tano alizozitaja, vijiji vitanufaikaje. Kama tunavyofahamu Sera ya Maji hairuhusu Kijiji cha B kianze kupata maji A kikarukwa. Nipende kusema kwamba vijiji vyote ambavyo mradi huu utavipitia, basi watapata maji kwa sababu lile bomba kuu litaruhusu michepuo kwa vijiji vile vinavyopitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ameongelea suala la muda mfupi. Mradi huu tunautarajia uchukue miezi 12 na tunatarajia uanze mwezi Mei mwaka huu. Mheshimiwa Mbunge hii kazi itafanyika kwa kasi kwa sababu tayari fedha zipo, hivyo itakuwa ni kazi ya muda mfupi na maji yataweza kuwafikia wananchi wetu kwa wakati. *(Makofi)*



**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa za Serikali za kumaliza tatizo la maji katika Mji wa Tunduma, bado changamoto kubwa imebaki kuwa kukosekana kwa chanzo cha uhakika katika Mji wa Tunduma. Je, nini mkakati wa Serikali wa kutekeleza ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais wakati wa uchaguzi ya kuvuta maji kutoka chanzo cha uhakika kilichopo katika Mji wa Ileje? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha uhakika cha maji kwa Mji wa Tunduma kama alivyoongelea chanzo cha maji kutoka Ileje, *feasibility study* inaendelea kufanyika na mara itakapokamilika basi mradi ule utatengewa fedha kwa awamu na utekelezaji utaanza mara moja. Vile vile kwa nyongeza pale Tunduma nimeshafika na kuona namna gani bora ya kuweza kupatikana kwa maji kwa sababu miundombinu ya awali tayari ilikamilika Mheshimiwa Mbunge niseme tulishaweza kumpa maelekezo Meneja wa Maji Mkoa, *RUWASA* na yule *Engineer* ni *Engineer* ambaye tunamtegemea katika Wizara na anafanya kazi vizuri sana. Hivyo, nikuhakikishie shida ya maji katika Mji wa Tunduma inakwenda kuwa historia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unaweza kupata picha ya tatizo la maji; unawaona Waheshimiwa Wabunge wengi kabisa wamesimama hapa lakini sasa hawawezi kupata fursa wote ya kuuliza. Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Sisi Namtumbo kule tuna miradi ya maji

yenye takriban miaka nane lakini bado haijakamilika na kuna changamoto ya ukamilifu wa miradi hiyo hasa vifaa na mabomba. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwa tayari kuongozana nami kabla ya Bunge la Bajeti kwenda kuona miradi hiyo na changamoto yake na kuona ni jinsi gani atatuongezea nguvu ili kukamilisha miradi hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa unataka kuongozana na Naibu Waziri au Waziri? Ni yupi uliyemwomba kati ya hao? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna anavyojibu maswali vizuri na nimpongeze na Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Kawawa kwa kazi kubwa anayoifanya Namtumbo. Kubwa mimi nipo tayari kuongozana naye. Mkoa wa Ruvuma pia ni moja ya mikoa ambayo tumeainisha hii changamoto ya maji na tumewapatia zaidi ya bilioni nane na katika wilaya yake tumeipa 1.3 *billion* katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Kwa hiyo, tunamtaka Mhandisi wa Maji, Namtumbo aache porojo, afanye kazi kuhakikisha wananchi hawa wanaweza kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri anajua Mradi wa Maji wa Bunda umetumia zaidi ya miaka 13, tayari maji yameshatoka Ziwa Victoria, kata saba za mjini wameanza kueneza mtandao wa maji na takriban milioni 300 zilienda. Ninachotaka kujua kama Mbunge *senior* wa eneo lile na kipenzi cha

Wanabunda, ni lini Kata 14 zitapata maji safi na salama?  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Ester kipenzi cha Wanabunda ni wewe au ni Mbunge wa Jimbo la Bunda?  
(Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kuhusiana na Bunda mradi uliokaa kwa miaka 13 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji lengo letu ni kuona kwamba tunaleta mapinduzi makubwa sana kuona maji sasa yanakwenda kupatikana. Miradi hii ambayo miundombinu imekamilika bado maji hayatoshelezi, wataalam wanaendelea na kazi na tutahakikisha maji yanaenda kupatikana. Napenda kusema kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo alishafika kwangu mara kadhaa na suala hili tunakwenda kulitekeleza haraka. Ziara yangu baada ya hapa ni kuelekea ukanda huo, basi Bunda napo pia nitafika na maji yatapatikana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote nawaona, lakini sasa muda wetu kidogo unaleta changamoto. Kwa hiyo kama nilivyosema watauliza wale waliotangulia. Mheshimiwa Anton Mwantona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kabla ya yote nipongeze sana Wizara ya Maji. Napongeza Wizara ya Maji, Naibu Waziri alikuja kwetu Rungwe Jimboni, ametembelea miradi, ameona matatizo ya maji kwa wananchi wa Rungwe. Naomba sasa niulize swali langu; je, ni lini mradi wa maji wa Mji Mdogo wa Tukuyu utanza kutekelezwa hasa baada ya Naibu Spika kutembelea na kutuahidi pale. Lakini pia upembuzi yakinifu ulishafanyika...

**NAIBU SPIKA:** Umeshauliza swali.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantona Mbunge wa Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji mdogo wa Tukuyu tunafahamu kabisa miundombinu yake ni chakavu na idadi ya watu imeongezeka, tayari maelekezo yapo kwa Meneja wa Maji Mkoa wa Mbeya na ameshaanza manunuzi ya vifaa vya kazi na kufikia mwezi Machi kazi zitaanza kufanyika pale Tukuyu na upatikanaji wa maji unakwenda kuboreshwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hayo maswali yametoshwa kwa Wizara ya Maji isipokuwa kuna swali la pili la Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko ambalo aliuliza kuhusu Rorya lilijibiwa swali moja. Nadhani unaweza kulijibu kwa sababu nimekuandikia hapo karatasi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la awali ambalo ni jibu langu la msingi. Eneo la Rorya visima hivi vitatu kwa sasa hivi vinapata maji kati ya 27. Vijiji hivi vinakwenda kupatiwa huduma kupitia Mwaka wa Fedha 2021/2022 lakini vile vile tayari Wahandisi wetu wa eneo lile wanaendelea na hii kazi na visima vile ambavyo vilisalia vinakwenda kuchimbwa na kuhakikisha kuona kwamba vinakwenda kutoa maji ya kutosheleza kwa wananchi wote wa Rorya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 81

## Ujenzi wa Barabara ya Likuyufusi – Mkenda

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Likuyufusi - Mkenda yenye urefu wa kilometa 124 kwa kiwango cha lami ili kufungua zaidi fursa za kiuchumi kati ya nchi yetu na Msumbiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye km 124 ni barabara muhimu kwa kuwa inaunganisha Nchi ya Tanzania na Msumbiji kupitia Mto Ruvuma.

Aidha, barabara hii inahudumia wasafiri wanaotumia uwanja wa ndege wa Songea wanaotokea Nchi jirani ya Msumbiji na maeneo mengine ya Mkoa wa Ruvuma. Vile vile, barabara hii ni muhimu kwenye suala la ulinzi wa mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali ilikamilisha usanifu wa kina wa barabara hii chini ya Kampuni ya *Crown Tech - Consult Limited* ya Tanzania. Hata hivyo, kufuatia uchimbaji wa makaa ya mawe kwenye eneo la Mhukulu lililopo kilomita 80 kutoka Songea na kilomita 60 kutoka Likuyufusi, Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS*, ilikamilisha mapitio ya usanifu wa kina wa barabara hii (mwaka 2020) ili iendane na mahitaji

na mazingira ya sasa. Vile vile, katika Mwaka huu wa Fedha 2020/2021, Daraja la Mkenda limetengewa shilingi milioni 110 kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa awamu ambapo katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 shilingi bilioni 1.59 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilomita 10. Kazi inatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2021 baada ya kukamilisha taratibu za manunuzi. Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.346 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili barabara hii iweze kupitika majira yote ya mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama kwa namna ambavyo halali usiku na mchana anafuatilia kuona kwamba barabara hii inajengwa ili kuweza kuchochea uchumi wa wananchi wa maeneo husika Mkoa wa Ruvuma na Nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Ruvuma ni mkoa ambao umeshika nafasi ya kwanza mara tano mfululizo kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka. Wananchi wa maeneo hayo wanajishughulisha na kilimo, uzalishaji wa makaa ya mawe, soko la mazao la Kimataifa, lakini pia kuna shamba la miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Naomba uulize swali Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najenga hoja. Swali la kwanza, je, Serikali haioni

kuwa kuchelewesha ujenzi wa barabara hii ni kuendelea kufanya udumavu wa maendeleo kwenye maeneo husika hasa kwa Mkoa wa Ruvuma na Jimbo la Peramiho na kwa nchi yetu kwa ujumla? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nafahamu kwamba Kamati ya Bajeti imetenga fedha shilingi milioni 110 kwa ajili ya kufanya usanifu wa ujenzi wa daraja, daraja ambalo limekwishajengwa, daraja la Mkenda. Je, ni kwa nini Serikali sasa isihamishe fedha hii shilingi milioni 110 ikaanze ujenzi wa barabara mara moja ili kuweza kuchochea uchumi wa maeneo husika? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii na kwa kutambua umuhimu wa uzalishaji ambao uko katika Mkoa wa Ruvuma lakini pia na makaa ya mawe; katika jibu langu la msingi tumesema barabara hiyo pia ni muhimu sana kwa ulinzi wa nchi yetu na pia ni moja ya vipaumbele vya nchi kuunganisha nchi na nchi na hii ni *trunk road* wala sio *regional road*. Ndiyo maana tayari barabara hii imeanza kutengewa fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kama Mheshimiwa Mbunge amenisikiliza vizuri, kulifanyika usanifu wa awali ambao wakati huo barabara haikuwa na matumizi ambayo inayo sasa hivi na ndiyo maana kukafanyika *redesign* yaani usanifu mpya kwa sababu tayari sasa kule kuna makaa ya mawe na mgari yaliyokuwa yanapita wakati ule wakati barabara inafanyiwa usanifu siyo ambayo sasa yanapitika. Kwa hiyo lazima lile daraja lifanyiwe usanifu mpya ili liweze kumudu shughuli ambazo sasa zitaweza kufanyika

kwa maana ya kuwa na uwezo wa kuhimili magari ambayo yatapita na uzito wake hasa baada ya kugundua makaa ya mawe na kuongezeka kwa *traffic* kwenye hiyo njia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, lakini pia swali hilo linafanana na hali ya kule Mufindi. Kwa kuwa Mufindi ni kitovu cha viwanda nchini na zaidi ya viwanda tisa viko pale na miundombinu imekuwa ni mibovu sana; na kwa kuwa barabara ya Nyololo - Mtwango na Mafinga - Mgololo zimeahidiwa kuanzia wakati wa Mwalimu Nyerere, pamoja na Rais Magufuli, zimeahidiwa na Mawaziri Wakuu, Mzee Pinda na Mzee Kassim Majaliwa, zimetajwa kwenye Ilani ya CCM karibu mara tatu...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuingiza kwenye bajeti barabara hizo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara zote alizozitaja zinakwenda kwenye maeneo ya uzalishaji mkubwa sana ambao yanachangia fedha nyingi sana kwenye Mfuko wa Serikali na kama alivyosema barabara hizo zimeahidiwa na viongozi wengi wa Kitaifa, lakini pia barabara hizo zimetajwa kwenye Ilani, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizo kwa sababu ya umuhimu wake, kuanzia bajeti inayokuja zitaanza kutengewa fedha ili ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofi*)



**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi.

Na. 82

**Kujenga kwa Lami Barabara ya Lupiro – Malinyi – Londo – Namtumbo**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Lupiro – Malinyi – Londo – Namtumbo, yenye urefu wa kilometa 296 ambayo ipo katika Ilani ya CCM 2020?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Lupiro – Malinyi – Londo – Namtumbo yenye urefu wa kilometa 296 ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi – Kidatu – Ifakara – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha yenye kilometa 547 ambayo inaunganisha Mikoa ya Morogoro na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, Wizara kupitia *TANRAODS*, imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwaka 2018. Ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara kilometa 66.9 kwa kiwango cha lami pamoja na Daraja la Ruaha Mkuu unaendelea. Fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu iliyobaki ikiwemo ya Lupiro – Malinyi – Londo – Namtumbo zinaendelea kutafutwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ikiendelea kutafuta fedha za ujenzi, Serikali pia imeendelea kutenga fedha za matengenezo mbalimbali ya barabara hii, ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 720 na shilingi milioni 377.2 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii katika mikoa ya Morogoro na Ruvuma mtawalia ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antipas Mgungusi, swali la nyongeza.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya barabara hiyo kutoka Kijiji cha Misegese kufika Malinyi Mjini huwa haifikiki kipindi chote, hata mvua ikinyesha siku moja tu, tunalazimika kutumia mitumbwi kufika Malinyi Mjini na magari hayafiki kabisa. Mkandarasi ambaye yuko *site* anaweka *calavat* moja badala ya yanayotakiwa kama sita au saba. Amepewa kazi ya kuinua tuta mita 200 badala ya kilometa moja ambayo ni uhitaji halisi. Je, Serikali haioni haja ya kumuongezea uwezo kujenga kulingana na uhitaji ambao nimeutaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda Malinyi baada ya Bunge hili ili kujionea hali halisi ya miundombinu na kutafuta suluhisho la pamoja? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mgungusi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na swali la mwisho, naomba niseme kwamba barabara hii imekuwa inaulizwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao ni wanufaika wa barabara hiyo. Kwa hiyo, niwadhihirishie ama

niwaaminishe kwamba mara baada ya kikao hiki nitahakikisha naitembelea barabara hiyo ili niweze kuifahamu vizuri kwa sababu kila mara Wabunge wa eneo hilo wananifuata kwa ajili ya kutafuta utatuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili alilouliza kuhusiana na tuta linalojengwa na mkandarasi, naomba Mheshimiwa Mbunge Mgungusi kwa sababu, bahati nzuri mkandarasi yuko *site*, tutaongea na Meneja wa *TANROADS* ambaye ndiye anamsimamia mkandarasi huyu ili kama kuna shida ya kitaalamu ama ya uwezo, Serikali tutahakikisha kwamba tunampa maelekezo ya afanye vile inavyotakiwa kama ambavyo ipo kwenye *design*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mara kwa mara Serikali imekuwa ikizungumzia kujenga barabara inayotoka Mtwara Mjini kuelekea Msimbati ambako kuna mitambo na visima vya gesi. Je, ni lini sasa Serikali itajenga barabara hiyo muhimu kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Shamsia kwamba katika kitu ambacho Serikali ya Awamu ya Tano inakifanya, kwanza tumetoa ahadi kujengwa kwa barabara za wilaya, mkoa na za kitaifa na barabara zile ambazo zinaenda maeneo muhimu kwa maana ya uchumi wa Taifa. Kwa hiyo, kama barabara hiyo inaangukia humo, nataka nimhakikishie kwamba kuanzia bajeti tunazoanza na katika Mpango huu ambao tunaendelea nao, nina hakika katika miaka mitano barabara hii itakuwa imejengwa kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kama ilivyo kwa barabara hii ya Lupiro – Malinyi, barabara ya Korogwe – Dindira – Bumbuli mpaka Soni iliahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ilikamilika. Napenda kujua, ni lini sasa kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami itaanza ili kuwasaidia wananchi wa Korogwe na Lushoto kwenye eneo la usafiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge ambaye ameuliza barabara ya Korogwe hadi Soni ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge wawe na imani na Serikali hii ya Awamu ya Tano kwani kwanza ni ahadi za viongozi wetu wa kitaifa Mheshimiwa Rais lakini pia zimetajwa katika Ilani. Naomba tuanze bajeti na nina hakika hizi barabara ambazo tunaziulizia zimo, kwa sababu tumeahidi tutatengeneza hizi barabara kwa kiwango cha lami. Nashauri Waheshimiwa Wabunge wawe na imani kwamba barabara hizi zitajengwa ikiwa ni pamoja na barabara ya Korogwe kwenda Soni. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, sasa aulize swali lake.

Na. 83

### **Kipande cha Barabara ya Mbagala Zakhem – Mbagala Kuu na Mbande – Msongola**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza kipande cha barabara kutoka Mbagala Zakhem hadi Mbagala Kuu na kipande cha barabara toka Mbande – Kisewe hadi Msongola?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mbagala Zakhem – Mbagala Kuu yenye urefu wa kilometa 5.1 ni miongoni mwa barabara ambazo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne alitoa ahadi mwaka 2017/2018. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ilijenga kilometa moja ya lami katika barabara hii ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha barabara ya Mbande – Kisewe – Msongola ni sehemu ya barabara ya Chanika – Mbande – Mbagala Rangi Tatu yenye urefu wa kilometa 29.4 inayounganisha barabara ya Kilwa na barabara ya Nyerere. Kati ya kilometa 29.4 kilometa 22.8 zimekwishajengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 6.06 zilizobaki zipo kwenye kiwango cha changarawe. Barabara hii inasimamiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Msongola mpaka Mbande kilometa 6.06 kwa kiwango cha lami. Ujenzi unaendelea kwa awamu kupitia fedha za maendeleo ambapo kuanzia mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2020/2021 jumla ya shilingi bilioni 1.05 zimetumika kujenga kilometa moja kwa kiwango cha lami nyepesi. Kazi hiyo imeanza Msongola kuelekea Mbande. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni nini kauli ya Serikali kwa kumalizia kipande cha Mbande – Kisewe ambacho kimekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Kata ya Chamazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, barabara ya Zakhem – Mbagala Kuu imepata fedha za Mradi wa Uboreshaji wa Jiji la Dar-Es-Salaam na imeshindwa kujengwa kwa sababu ya uwepo wa bomba la mafuta la TAZAMA. Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia walao *corridor* ya mita saba ili barabara hiyo ambayo tayari inayo fedha iweze kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tunavyoongea sasa hivi, Mheshimiwa Chaurembo ni shahidi, tulikuwa na kilometa 6.05; kilometa moja imeshakamilika zimebaki kilometa 5.06. Nimhakikishie Mheshimiwa Chaurembo katika mwaka huu wa bajeti, kupitia fedha ya matengenezo, sasa tutaanza barabara ya kutoka Mbande kuja Msongola ambapo tunajenga kilometa 1.5 kwa kiwango cha lami. Pia kwa fedha ya maendeleo tutaendelea kutoka Msongola kwenda Mbande kilometa 1. Kwa hiyo, tutabakiwa kama na kilometa 2.5 ambazo zitakuwa bado hazijakamilika na fedha itakapopatikana tutaendelea kukamilisha barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuhamisha bomba ama barabara Serikali imelipokea na itakwenda

kulifanyia kazi tuone kama tutahamisha kwa sababu inapita karibu na bomba. Tutaangalia namna ya kufanya ili barabara ile muhimu sana iweze kuanza kujengwa. Pia kwa sababu suala hili siyo la Idara yangu pekee kwa maana ya Wizara ya Ujenzi ni Wizara nyingi, kwa hiyo, tumelipokea na tutakwenda kulifanyia kazi kuona ni namna gani tufanye kuhamisha barabara hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 84

### **Kuruhusu Watu Binafsi Kununua Kahawa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Mfumo wa ununuzi wa kahawa kupitia Vyama vya Ushirika umekuwa mwiba kwa wananchi wa Kyerwa na Karagwe kupitia *KDCU*:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiruhusu watu binafsi kununua kahawa moja kwa moja toka kwa mkulima?

(b) Je, ni lini wakulima wanaodai watalipwa fedha zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Anatropia kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa ununuzi wa kahawa hapa nchini unawaruhusu wanunuzi binafsi kununua kahawa kutoka kwa wakulima kupitia Vyama vya Ushirika.

Kahawa inayoruhusiwa kwa wanunuzi binafsi ni ile ambayo tayari imepitia utayarishaji wa ngazi ya awali na ikiwa tayari kupelekwa kiwandani au kuuzwa kwenye soko la mnada au soko la moja kwa moja. Pia Vyama vya Ushirika vinaruhusiwa kuingia makubaliano na kampuni binafsi kupitia utaratibu wa kilimo cha mkataba, utaratibu wa wafanyabiashara kwenda moja kwa moja kwa wakulima, maarufu katika Mkoa wa Kagera *butura*, hauruhusiwi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera hadi kufikia tarehe 20 Januari, 2021 katika msimu wa 21 jumla ya wanunuzi binafsi saba wamenunua kiasi cha kilo milioni 13 za kahawa maganda kupitia kwenye Vyama vya Ushirika. Kutokana na maboresho hayo ya kuruhusu wanunuzi binafsi na Vyama vya Ushirika wameweza kulipa bei ya Sh.1,200 kwa kilo ya kahawa ya maganda kwa msimu wa 21 ukilinganisha na kiasi cha Sh.1,100 kwa kilo katika msimu uliotangulia wa mwaka 2020. Aidha, Bodi ya Kahawa itatoa vibali mapema kwa wafanyabiashara binafsi ambao wako tayari kununua kahawa katika msimu wa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Karagwe (*KDCU*) katika msimu wa kahawa wa mwaka 2020/2021 kimekusanya kahawa maganda kilogramu milioni 40.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 48 kutoka katika Vyama vya Msingi 123. Aidha, hadi kufikia tarehe 18 Januari, Chama Kikuu cha Ushirika (*KDCU*) kilishamaliza malipo yote ya wakulima wa Mkoa wa Kagera.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Niweke kumbukumbu sahihi, siyo kweli kwamba wamemaliza kulipa vyama vyote; kuna *AMCOS* ya Rumulo ikiunganisha Vijiji vya Rugasha, Kibingo na Mrongo wamelipwa nusu ya malipo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Changamoto kubwa ambayo wakulima wanakutana nayo



inayotokana na Vyama vya Ushirika ni kushindwa kuwapa fedha kwa wakati na sababu ni kwamba fedha inakopwa benki kwa asilimia 9. Serikali haioni ni wakati muafaka kwa benki za kilimo kupunguza riba kwenda mpaka asilimia 5, ili waweze kupata uwezo wa kulipa kiasi cha kutosha cha kahawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, sasa tunafanya biashara huru kwa kilimo na biashara nyingine ikiwa ni sera ya Serikali. Nchi jirani kama Uganda wananunua kahawa kwa gharama au kwa bei nzuri. Ni kwa nini Serikali isitengeneze *special arrangements* kwa wakulima hata wa Kagera waweze kuuza kwa makampuni ya Uganda ambayo yanatoa bei iliyo nzuri? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatopia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitashukuru akinipa *facts* za kwamba Chama cha Msingi alichokitaja hakijalipwa kwa sababu takwimu tulizonazo Wizarani na fedha zilizotolewa na *TADB* kwa ajili ya kulipa wakulima wa Mkoa wa Kagera tumelipa 100%. Kwa hiyo, kama kuna kiongozi yeyote wa Chama cha Msingi ama Chama Kikuu cha Ushirika hajafikisha fedha kwa wakulima hao, tutachukua hatua *immediately* kwa sababu ni uhujumu uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la bei ya Uganda; mwaka huu katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki, ukitoa wakulima walioko katika nchi ya Rwanda ambao wana mkataba maalum na *Starbucks* ambapo sisi kama Serikali sasa hivi tumeanza maongezi nao kwa ajili ya kununua moja kwa moja kutoka kwa wakulima, wakulima wa Mkoa wa Kagera wameuza bei nzuri kuliko mkulima wa Uganda. Kama mna bei na *facts* kwamba kuna mnunuzi Uganda anatoa bei nzuri kuliko mnunuzi wa Tanzania, milango ya

Wizara ya Kilimo iko wazi, karibuni mtuletee. Hata hivyo hatutaruhusu biashara isiyokuwa na *contract*; yenye *clarity* ya mambo mawili (bei na *volume*) kuliko kuwaambia wakulima kwamba tutanunua na mchezo wa butura umekuwa ukiendelea. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hatutaruhusu mkulima kufuatwa shambani kununuliwa kahawa. Mheshimiwa Mbunge wewe ni mzoefu, Kagera kumekuwa na biashara inaitwa butura na biashara hii imekuwa ikisimamiwa na viongozi wenye mamlaka na nguvu ambao wamekuwa wakienda kununua kahawa kwa wakulima kwa Sh.500 na Sh.700 hatuwezi kuruhusu. Kama kuna tatizo la malipo katika Vyama vya Msingi, tushughulikie tatizo la ucheleweshaji wa malipo na wala siyo kuu mfumo tulionao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la riba, mpaka sasa kupitia *Tanzania Agricultural Bank* ndiyo imekuwa benki ambayo imeshiriki katika kushusha riba kwa wakulima ambao wamekopa katika benki mbalimbali. Walianza na riba ya asilimia 11 Vyama vya Ushirika vya Kagera sasa hivi wamepewa kwa riba ya asilimia tisa.

Vilevile *commercial banks* zilikuwa zinawapa riba kwa asilimia 20 kwa *guarantee* ya kupitia *TADB*, mikopo hiyo wamekuwa wakipewa kati ya asilimia 13. Tumeanza mazungumzo na *commercial bank* ili riba katika sekta ya kilimo isizidi asilimia 10. Majadiliano haya yameanza na tunaamini tutafikia lengo hili kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mikopo yenye riba nafuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 85

**Bei ya Zao la Kahawa**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza mazingira wezeshi ya kuongeza bei ya zao la kahawa ili wakulima wa zao hili waweze kunufaika kama ambavyo wakulima wa nchi jirani ya Uganda wanavyonufaika?

(b) Utaratibu wa ununuzi wa zao la kahawa unapitia Vyama vya Ushirika, hali inayoonekana kutovutia ushindani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi ili kuvutia ushindani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ndaisaba, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua tunazochukua kwa ajili ya kuongeza bei bora ya kahawa kwa wakulima wa Mkoa wa Kagera na Tanzania nzima; moja tumeanza utaratibu wa kuwapatia vifaa kwa ajili ya kuweza kuchakata kahawa yao na badala ya kuuza kahawa ghafi wauze kahawa ambayo imeshaanza kuchakatwa. Aidha, Serikali inafufua na kujenga upya na kuimarisha ushirika wa wakulima kupitia umoja wao waweze kuamua na kupata bei nzuri ya kahawa. Pia, Serikali imeanza kuruhusu mifumo ya *direct export* ambapo Vyama vya Ushirika na wakulima moja kwa moja wamekuwa wakiuza moja kwa moja kwa wateja. Hatua nyingine ambayo Wizara inachukua sasa hivi tumeanza mchakato wa kutafuta *identification logo* ambapo kahawa ya Tanzania kokote kule itakaponywewa duniani iweze kutambulika kwamba ni *Tanzania produce*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ununuzi wa kahawa hatua ambazo tunachukua kama Wizara ni kwamba Serikali sasa hivi tumeruhusu ushindani wa moja kwa moja wa makampuni binafsi, lakini vile vile yakishindana na Vyama vya Ushirika. Aidha, katika kuhakikisha kama nchi kufikia

malengo ambayo tumejiwekea ya mwaka 2025 yaliyoainishwa katika Ilani kufikia tani 300,000 Serikali inatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa miche bora ya kahawa ambapo jumla ya miche bora milioni 55 inazalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, mkakati uliopo ni kuzalisha miche bora milioni 20 ambayo itakuwa ni *specific* kwa ajili ya *organic coffee*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Ruhoyo Ndaisaba, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na aliyoyasema yakitekelezeka basi Tanzania ndani ya kipindi cha miaka mitatu itakuwa inaongoza kwa uzalishaji wa kahawa ukiachia Ethiopia, Uganda, Cote d'Ivoire pamoja na Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niulize swali langu la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha miche milioni 20 inayotarajiwa kuzalishwa inawafikia wakulima wa Tanzania wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Ngara kwenye Tarafa za Kanazi, Nyamiaga, Rulenge pamoja na Murusagamba?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari mwaka huu tutagawa katika Mkoa wa Kagera kuanzia tarehe 27 Februari, 2021, tutagawa jumla ya miche 1,000,000 kwa wakulima bure. Kwa hiyo hiyo ni sehemu na malengo tuliyojiwekea ni ugawaji wa jumla ya miche milioni 20.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini sasa swali lake liulizwe.

Na. 86

### **Hitaji la Kituo cha Uhamiaji na cha Polisi Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza :-

Jimbo la Tunduru Kusini limepakana na Nchi ya Msumbiji kwa upande wa Kusini.

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Uhamiaji na cha Polisi kuhudumia maeneo hayo ya mpakani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja "C" unaofanywa na Halmashauri ya Tunduru umefikia katika hatua ya lenta. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji utategemea makubaliano baina ya Serikali ya Tanzania na Msumbiji kama taratibu za ujenzi wa Vituo vya Uhamiaji mipakani unavyotaka. Kwa sasa makubaliano hayo bado hayajafanyika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza

**MHE. DAIMU IDDI MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jimbo la Tunduru Kusini lina tarafa tatu, Tarafa ya Nalasi, Lukumbule na Sakata na zote zimepakana na Mto Ruvuma, kwa ng'ambo ni Msumbiji, lakini katika Jimbo hilo Kituo cha Polisi kiko kimoja tu kipo kwenye Tarafa ya Nalasi peke yake. Swali la kwanza, je, Serikali haioni ni muhimu sana

kwa sasa kukamilisha Kituo cha Polisi Lukumbule ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi wa mipakani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Lukumbule ni sehemu ambayo watu wengi wanapitia kwenda na kutoka Msumbiji katika harakati za kufanya biashara. Wananchi wa Msumbiji wakija Tanzania hamna mahali popote wanapopita tunawapokea kiurafiki, lakini sisi Watanzania tukienda Msumbiji tunakamatwa wanapigwa, wananyanyaswa na kunyang'anywa mali zao. Je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuharakisha mazungumzo ya kuanzisha Kituo cha Uhamiaji katika kijiji au Makao Makuu ya Tarafa ya Lukumbule?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduru Kusini kulikuwa kuna vituo vitatu, Kituo cha Nalasi, Masuguru na Lukumbile lakini kwa bahati mbaya hiki kituo kimoja kilikuja kikatiwa moto baada ya kutokea machafuko ya wananchi. Hata hivyo, baada ya Serikali kuona umuhimu sasa wa kuwepo kituo ili sasa kuimarisha hali ya ulinzi pale, Serikali ikashusha Waraka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili sasa watusaidie kujenga kile kituo hili eneo la Lukumbile. Hivi ninavyokwambia tayari kituo kimeshaanza kujengwa na kimeshafikia katika hatua ya lenta. Sasa kikubwa tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara tunaenda kutengeneza mazingira sasa ya kuona namna na kupitia umuhimu wa kuwepo kituo hiki ili sasa tuweze kuweka kituo hiki ili wananchi waweze kuishi katika mazingira ya usalama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali la pili, hakuna Serikali yoyote duniani ambayo inapenda wananchi wake wapate tabu; wanyanyaswe, wapigwe, wadhulumiwe. Sasa kitu ambacho nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, kutokana na umuhimu wa

suala hili tunakwenda kuona namna ambavyo tutakapotengeneza bajeti yetu hii Wilaya ya Tunduru hasa katika hii sehemu ambayo wanahitaji Kituo hiki cha Uhamiaji tutaipa kipaumbele ili tuone namna ambavyo tunaweza tukapata kituo cha uhamiaji hapa ili wananchi waweze kuepukana na huo usumbufu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Felista Deugratus Njau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 87

**Kuwapatia Hati Wananchi wa Meko na Basihaya  
Dar es Salaam**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa hati kwa Wananchi wa Meko na Basihaya baada ya maeneo hayo kupimwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Felista Deugratus Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Meko liko katika Kata ya Kunduchi Manispaa ya Kinondoni awali eneo hilo lilitengwa kwaajili ya machimbo ya kokoto. Baada ya machimbo kufungwa Manispaa ilidhamiria kupima viwanja kwa ajili ya Kituo cha Biashara. Hata hivyo upimaji haukufanyika kutokana na eneo hilo kuwa limevamiwa na wananchi. Mwaka 2017 Manispaa ya Kinondoni ilimaliza

mgogoro na wavamizi kwa kuruhusu wananchi wapimiwe viwanja katika eneo hilo kupitia mpango wa urasimishaji wa makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ilikubalika kuwa wananchi watapimiwa viwanja katika maeneo yale waliyoyaendeleza na maeneo yaliyo wazi yatapangwa na kupimwa viwanja vya matumizi ya umma. Kazi ya upimaji ilianza tarehe Mosi Januari, 2019 na kukamilika tarehe 20 Januari, 2021 na jumla ya viwanja 840 vimepimwa na hatua ya umilikishaji zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Basihaya lipo katika Kata ya Bunju, Mtaa wa Basihaya ambako kuna Vitongoji vya Chasimba, Chatembo, Chachui ambavyo kwa sehemu kubwa uendelezaji wake umefanywa ndani ya ardhi inayomilikiwa na Kiwanda cha Saruji cha Wazo. Wamiliki wa Kiwanda cha Wazo walipeleka malalamiko Mahakamani baada ya kuona eneo lao limevamiwa. Mahakama kupitia Shauri Na. 129 la mwaka 2008 kati ya Haruna Mpangao na wenzake 932 dhidi ya Tanzania *Portland Cement* ilitoa uamuzi kuwa wananchi waliovamia katika eneo hilo waondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi ilichukua jitihada za kufanya majadiliano na mwekezaji ili kuangalia namna bora ya kutatua mgogoro huo ambapo iliamua wananchi walioendeleza katika maeneo hayo wasiondolewe bali walipe gharama ambazo atapewa mwekezaji ili akanunue eneo lingine kwa ajili ya kupata malighafi za kutengeneza saruji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshawapimia viwanja waendelezaji wote katika eneo hilo ambapo jumla ya viwanja 4,000 vimepatikana na kila mwendelezaji atatakiwa kulipia gharama zitakazotumika kumlipa mmiliki wa kiwanda. Wizara inaendelea kufanya majadiliano na mmiliki wa Kiwanda cha Saruji cha Wazo kuhusu gharama na fidia ya eneo lililoendelezwa na wananchi.



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felista Deogratus Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ifahamike kwamba kuhusu upimaji wa ardhi ndani ya nchi yetu mlolongo huu umekuwa na kigugumizi kikubwa na kupelekea Serikali kupoteza mapato, migogoro ya ardhi isiyokuwa na lazima na tatu wananchi kukosa dhamana ya kwenda kuchukua mikopo maana yake wananchi kupata umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu la kwanza; Ni lini Serikali itaweka utaratibu maalum wa kupima maeneo yote ambayo hayajapimwa kwa sababu Waziri alisimama kwenye vyombo vya habari akajinasibu akasema ndani ya mwezi mmoja mtu akishapimiwa atapata hati. Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu maalum wa kupima maeneo yote ambayo hayajapimwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa wananchi wa Basihaya wako tayari baada ya kukaa na Mwekezaji, Serikali na wananchi wa Basihaya wako tayari kulipa *premium*, kiwango ambacho kilikuwa ni makubaliano kati yao na *premium* ni kati ya 1% mpaka 1.5%. Ni lini sasa Serikali itakwenda kutoa hati katika maeneo hayo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felista Deogratus Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameuliza ni lini sasa Serikali itapima maeneo yote ili kuweza kuondoa pengine adha ambayo watu wanaipata. Naomba niseme

tu bajeti ambayo tunaendelea nayo imeainisha namna ambavyo Wizara imejipanga katika kuhakikisha kwamba maeneo yote nchini yanapimwa. Katika kufanya hilo pia tumeweza kushirikisha makampuni binafsi katika kufanya ule urasimishaji kwenye yale maeneo ambayo tayari yalikuwa yameshakaguliwa. Suala la kupima nchi nzima liko katika utaratibu wa bajeti ya Serikali na inategemea pia na upatikanaji wa fedha, lakini mpango upo ambao tutakwenda kukamilisha upimaji. Hili pia linahitaji ushirikiano na taasisi binafsi ambazo tumekuwa tukizishirikisha ambapo nyingi zimeonekana pia hazina uwezo wa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo kama Wizara tunatafakari namna bora ya kuweza kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ambalo amezungumzia habari ya umilikishaji katika maeneo yale, kwanza nataka tu niseme kwamba Mheshimiwa Felista anatakiwa kuishukuru sana Serikali kwa sababu maeneo yale ambayo anaomba watu kumilikishwa kisheria ilikuwa waondolewe, kwa sababu walikuwa wamevamia, lakini busara ya Wizara au ya Serikali ilipelekea kufanya mazungumzo ili wale watu waweze kumilikishwa na zoezi hilo linaendelea. Katika urasimishaji ile *premium* ambayo anaizungumza ni asilimia moja ambayo ni ya chini kabisa ukilinganisha na maeneo mengine ambayo wanalipa *almost* 2.5% na kabla ya hapo ilikuwa 15%, ikashuka ikawa 7.5%, ikaja 2.5% kwenye urasimishaji ni 1%. Kwa hiyo wanachajiwa kiasi cha chini kabisa kuweza kuwawezesha kupata umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la Hati, nadhani ninyi wenyewe ni mashahidi, Mheshimiwa Waziri pia ameweza kukaa ofisini na kuweza kuwapigia watu mmoja mmoja kuja kuchukua hati zao. Nimezunguka *almost* nchi nzima nikienda kugawa hati katika maeneo mbalimbali. Kuna hati ziko tayari lakini Watanzania hawaji kuchukua hati zao, lakini ukija nje wanasema hati hazitoki. Kasi ya utoaji hati kama tulivyosema ni ile ile ndani ya mwezi mmoja kama halmashauri imekamilisha taarifa zote, hati yako unaipata na zoezi hilo linafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania wale wote wanaohitaji kupata umiliki wa ardhi kama ambavyo ameongelea Mheshimiwa basi wawe tayari, pia ukishapeleka maombi yako uhakikishe umekwenda mpaka mwisho na umechukua hati yako. Wizara ndiyo *custodian* wa hati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa tumeshaelewa.

**NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Gwajima swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa nilipofika ofisini kwa Mheshimiwa Waziri akaniambia kwamba Meko tayari amepima viwanja 840 na akanijulisha kwamba amepima viwanja 4,000 Basihaya. Sasa kwa kuwa Chasimba, Chachui Chatembo na Kasangwe Burumawe, Kissanga na maeneo mengine ni maeneo ya Jimbo la Kawe na yaligubikwa na migogoro ya ardhi, sasa ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakwenda pamoja nami, Mbunge wa Kawe ili tukamalize migogoro iliyodumu kwa muda mrefu? (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo amempa Mheshimiwa Njau. Pili nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Kawe, Askofu Gwajima, mimi Askofu Gwajima nilikuwa simjui lakini amenitafuta kwa shughuli hizi za kero za wananchi wa Kawe hata kabla hajawa Mbunge, ilinilazimu kutoka kwenye kampeni, kuacha kampeni zangu Isimani kwenda kumsikiliza Dar es Salaam kwa sababu ya hiki. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Gwajima....

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mimi najua angeuliza Mheshimiwa Halima ningemjibu, ninyi siwajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Gwajima tukimaliza Bunge hili, nimepanga ratiba ya kwenda kukamilisha kero za migogoro ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatatua tatizo la Chasimba, Chatembo, Chachui kwa sababu mimi nilifanya kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwaonea huruma wale wananchi waliokuwa wafukuzwe. Kwa hiyo tutakwenda pamoja tutakwenda Basihaya, tutakwenda Chasimba na wananchi wanaoishi huko wajue kwamba nitakwenda na Mheshimiwa Mbunge Askofu Gwajima kuhakikisha kwamba jambo hili la kero za wananchi kule sasa linaisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ukumbuke tu kwamba unapotoka hapa Bunge likiisha unaelekea Mbeya Mjini kabla ya kuelekea Kawe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo hapa matangazo ya wageni waliopo Bungeni hayajanifikia bado, lakini yapo matangazo machache hapa.

Mheshimiwa Ummy Mwalimu Mbunge wa Tanga Mjini na pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, anawatangazia Wabunge wote wa Majimbo 50 ya Zanzibar kuhudhuria kikao leo tarehe 9 Februari, 2021, saa 7.30 mchana ukumbi wa Msekwa. Wabunge wa Majimbo kutoka Zanzibar mnaalikwa na Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya hicho kikao kitakachofanyika Msekwa.

Pia lipo tangazo la ibada Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wote walioko maeneo ya Bunge mnakaribishwa katika *Chapel* ya Bunge iliyoko maeneo ya *Basement* kwa ajili ya ibada leo tarehe 9 Februari, 2021 saa saba mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Aidha, leo Mtumishi wa Mungu Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima atahudumu katika ibada hiyo. Tangazo hili limetoka kwa Mwenyekiti wa *Chapel* ya Bunge Mheshimiwa Anna Lupembe.

Lipo pia tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mnaalikwa kushiriki katika mbio za kujifurahisha kilomita 10 ambazo zinaitwa *The Nineteenth Capital City Fund Run 10 Kilometers* zenye kauli mbiu Tunaanza Pamoja na Tunamaliza Pamoja zilizoandaliwa na Dodoma *Sports Company Limited*. Mbio hizi zitafanyika siku ya Jumamosi tarehe 13 Februari, 2021, kuanzia saa 12.30 asubuhi mpaka saa 2.30 asubuhi na zitaanza jengo jipya la *PSSSF* mpaka Chimwaga (*UDOM*).

Wabunge wote wanaotaka kushiriki mbio hizo wanaombwa kujiorodhesha eneo la mapokezi jengo la utawala. Tangazo hili limetoka kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwa sababu hii ni wiki ya mwisho, maswali mnayo mengi kwa ajili ya majimbo yenu na maeneo mnayowakilisha, niwasihi sana mpeleke maswali ya msingi kwa sababu maswali ya nyongeza si mara zote mtu atapata fursa. Maswali ya msingi una uhakika swali lako litafikiwa ili hata usipopewa swali la nyongeza usiwe mnyonge. Peleka maswali mapema na ukipeleka saa hizi itakurahisishia zaidi kupata majibu ambayo Serikali itakuwa nayo kuhusu kero ambazo wale unaowawakilisha wanazo katika majimbo yenu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU WA MEZANI:**

**HOJA YA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Miaka Mitano, yaani 2021/2022 mpaka 2025/2026 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Muongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU WA MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Mipango.

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba fursa kwa ajili ya kuchangia. Tumeletewa orodha ya wachangiaji hapa kutoka vyama vyote vyenye uwakilisha hapa Bungeni. Wabunge kutoka Chama cha Mapinduzi watachangia dakika tano kila mmoja, Mbunge kutoka ACT Wazalendo dakika kumi na CHADEMA pia watachangia dakika kumi kumi.

Kabla sijaanza kuwaitwa wachangiaji, ngoja niwasome wageni naona orodha imekuja hapa, kwa hiyo, inabidi watangaziwe kwenye Kamati yetu ya Mpango badala ya Bunge lakini wageni msiwe na wasiwasi watu ni walewale.

Wageni walioko Bungeni asubuhi hii, kwanza, ni wageni 22 wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ambaye ni

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni wanafunzi waliopata daraja la kwanza kidato cha pili kutoka Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Mchungaji Steven Mashoni. Ndani yao wapo watoto yatima wanne anaowafadhili Mheshimiwa Mbunge. Wageni mkitajwa kundi lenu mnasimama ili rahisi kuwaona. Karibuni na hongereni sana watoto wazuri kwa kufanya vizuri. Sasa hapa ni daraja la kwanza, kidato cha pili, tunaamini mtaendelea na daraja la kwanza kidato cha nne na cha sita na chuo kikuu mtafika namna hiyo, kila la heri. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 40 wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni wanafunzi wa Diploma ya Maendeleo ya Jamii, Chuo cha Mipango kilichopo Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Gerald Swai. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Ravia Faina ambao ni wananchi wa Jimbo la Makunduchi, Mkoa wa Kusini Ugunja. Wageni hao ni Ndugu Ali Boko, Ndugu Mohamed Mbaraka na Ndugu Ali Khatib. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 13 wa Mheshimiwa Iddi Kassim ambao ni wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Msalala Mkoa wa Shinyanga wakiongozwa na Ndugu Twaha Abdul. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Stella Fiyao ambao ni ndugu, marafiki na viongozi kutoka Tunduma Mkoa wa Songwe wakiongozwa na mume wake Ndugu Simon Fiyao. Wamekaa upande gani hawa jamani.

**MBUNGE FULANI:** Wamekosa nafasi.

**MWENYEKITI:** Haya huyo shemeji yetu tutamuona jioni.  
*(Makofi)*

Wageni 76 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Maaskofu, Wachungaji na Waombaji wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Gonda. Karibuni sana

na nataka kuamini hawa watakuwa sehemu ya hiyo ibada itakayoongozwa na Askofu Gwajima. *(Makofi)*

Wageni 58 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni Kwaya ya Elishadai kutoka Kanisa Anglikana Chadulu, Jiji Dodoma wakiongozwa na Ndugu Amani Mapopo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 38 wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambao ni Maaskofu, Wachungaji na Kwaya ya Kusifu na Kuabudu *(Praise and Worship)* kutoka Jiji Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Asheri Labani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Simon Songe ambao ni wapiga kura wake kutoka Busega, Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Mchungaji Yohana Ng'humba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 ambao ni Makatibu Kata wa CCM, Wilaya ya Bahi wakiongozwa na Katibu wa Mbunge Ndugu Hamisi Hamsini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni ambao wako Bungeni kwa ajili mafunzo na kundi la kwanza ni wanachuo 100 kutoka Chuo cha Mipango kilichopo Jijini Dodoma ambao wamekuwa kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili kutoka Jijini Dodoma; Ndugu Christopher Mwambola na Ndugu Moses Maroa ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wageni ambao tuko nao siku ya leo Bungeni, kwa hivyo tutaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ajiandae.



**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo katika siku ya leo. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai wake na leo tuko hapa tunaendelea kuwakilisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kuchangia kuhusu mpango huu kwanza nikipiga suala la uwekezaji wa ndani ya nchi. Tumekuwa tukitarajia mengi kutokana na utajiri wetu wa rasilimali nyingi zilizomo ndani ya nchi. Mipango na maneno, wenzetu Chama Cha Mapinduzi mnaongea sana, mnapanga sana, mipango hii ukichukua toka ilivyoanza mpaka leo kwa hakika tungekuwa hatupo hapa tulipo lakini tunapanga hatutimizi mipango yetu, sijui kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka sijaingia katika Bunge hili tumekuwa tukisikia suala la Liganga na Mchuchuma. Nilipoingia ndani ya Bunge hili nilibahatika kuwepo kwenye Kamati ya Uchumi, Viwanda, Biashara na Uwekezaji, ni kati ya mmoja wa mwanakamati tuliokwenda kutembelea maeneo yale. Kwa kweli katika kutembelea maeneo yale tuliiona shani ya Mungu ilivyo kubwa ya utajiri mkubwa wa chuma ambacho Mwenyezi Mungu ametujalia katika nchi yetu. Yamepangwa, yamepangwa lakini hadi leo tumeshindwa kutumia Mradi ule wa Chuma cha Liganga na Mchuchuma katika kuwaletea wananchi maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nchi yetu iko katika ujenzi wa miundombinu ya nguvu kweli kweli, nimshukuru Rais wetu kwa kusimamia ujenzi wa miundombinu katika nchi hii. Laiti mipango tuliyoipanga, Chuma cha Liganga na Mchuchuma kingeanza kuzalishwa leo hii ingekuwa hatuagizi chuma kutoka nje katika kujenga reli ambayo tunaijenga ndani ya nchi yetu. Waheshimiwa pigeni makofi kwa maneno haya mazuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebaki ni *story* lakini hatutashiba maneno, Watanzania wanataka vitendo, tuliyoypanga tuyaoneshe kuyatenda kwa vitendo. Mradi

ule wenzetu nchi jirani wanaulilia na kutuona sisi Watanzania ni watu wa ajabu sana kwamba tunajaliwa rasilimali ambayo ni mali kubwa kweli kweli duniani, ilitegemewa leo Tanzania tunaiuzia Afrika nzima chuma kutoka Liganga lakini matokeo yake imekuwa tunaletewa *story* kila mwaka. Nataka nimuombe Rais wangu, viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, isimamieni Serikali yetu itekeleze mradi huu muhimu kwa uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mnyonge mnyongeni haki yake mpeni na anayetenda jema msifu mchukie kwa sura yake na mengine lakini katika suala la kuchukua maamuzi magumu kwa maendeleo ya nchi Mheshimiwa Rais amefanya vema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais ni Waziri wa Ujenzi alitamani kupanua barabara kutoka Ubungo mpaka Kibaha, lakini bahati mbaya hakufanikiwa. Alipoingia madarakani ametekeleza mradi ule mpaka nikajuliza laiti leo ingekuwa wazo lile hakulifanyia kazi, basi kutoka Chalinze mpaka Dar es Salaam tungetumia saa ngapi? Bila shaka tungekesha, tungelala Kibaha lakini limetekelezwa. Sasa nimuombe Mheshimiwa Rais maamuzi magumu aliyoyachukua kwa kutekeleza mradi ule wa Kibaha mpaka Ubungo achukue maamuzi magumu pia kutekeleza Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa wafanyabiashara. Kama tunataka nchi yetu tuendelee lazima wafanyabiashara wetu wasaidiwe. Tatizo kubwa linalowakwaza wafanyabishara hasa wadogo wadogo ni utitiri wa kodi zinazowekwa na *TRA* katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunasema wafanyabiashara wakubwa wanaondoka lakini hata hawa wadogo nao watapotea kwa sababu kodi zimezidi ukubwa wa biashara zao. Ukiacha kodi, makadirio yasiyo na ukweli ni mengi. Wafanyabiashara wengi wanaofunga biashara ni mfanyabishara amefanya biashara yake anapelekewa

makadirio anaambiwa wewe unadaiwa milioni 500, ukiangalia biashara haifiki milioni 300, mfanyabiashara huyo kweli atakaa? Lazima atatafuta namna ya kuacha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuunge mkono sana Mheshimiwa Musukuma jana kwa jinsi alivyoyaona haya na akayaweka wazi. Kwa yale aliyoyazungumza na Kanuni zetu zinatumataza kurudia, nitaishia hapo lakini tuangalie utitiri wa kodi ulipo kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai tu, toka hapo nje, utaona hao wajasiriamali wanaouza nguo, vitenge na mashuka, wanakwamba mashuka kutoka Uganda, *why not* kutoka Kariakoo Dar es Salaam? Yameshuka bandari ya Dar es Salaam, yamesafiri yamekwenda Uganda, wafanyabiashara wetu imekuwa ni nafuu kwao kwenda kuchukua Uganda wakarudisha hapa kuliko kuchukua Kariakoo wakaleta hapa Dodoma, *why?* Bado hatukai tukajiuliza kuna tatizo gani? Tatizo nchi zilizotuzunguka wameweka kodi zinazolipika, sisi tunataka utajiri kwa wafanyabiashara hao kumi waliojikusanya, haitawezekana, tupanue wigo wafanyabiashara walipe kodi inayolipika ili wawe wengi nchi yetu ipate kodi nyingi na tuweze kuendelea. Nadhani hiyo imeingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala utawala bora, katika ukurasa wa 40, kifungu 2.6.3.3, naomba ninukuu kidogo: "Utawala bora, uwajibikaji na utoaji wa haki. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, Serikali iliendelea kupambana na rushwa, kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kujenga miundombinu ya utoaji wa haki kudumisha utawala bora". Naishia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nimsifu Rais kuwashinda nyie CCM. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake kwa kuiheshimu Katiba ya nchi hii. Kabla yetu alitangulia kuapa kuilinda na... malizia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa ni mlinzi wa Katiba. Uamuzi wake wa

kumtuma Mheshimiwa Humphrey Polepole (Mwenezi) awaambie wana CCM kwamba hataongeza kipindi cha utawala, ni ishara ya Rais wetu ya kuilinda na kuienzi Katiba. Atakuwa ni Rais wa kwanza katika ukanda wetu wa nchi za Afrika ambaye baadhi ya Wabunge wake wanamwomba aongeze muda lakini tayari ameweka msimamo wa wazi na alimtuma Mheshimiwa Polepole.

Mheshimiwa Polepole waambie CCM Mheshimiwa Rais hana shida ya kuongeza muda. Alikutuma na *video* zinatembea tunazona kwa nini unawaacha kina Mheshimiwa Sanga hapa wanaendelea kupotosha, kwa nini hamheshimu mawazo ya Mheshimiwa Rais? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita nilimwambia Mheshimiwa Ally Keissy, alinyanyuka na kujipendekeza hivi hivi, *nyi nyi nyi nyi!* Nikamwambia nchi hii ni ya kidemokrasia na Rais anaheshimu Katiba na Rais wetu ameshasema hataongeza muda. Kama mna wasiwasi hamna mtu wa kuwa Rais sisi wapinzani tunao. (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *why* Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni mzuri sana...

**MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Khatib, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Humphrey Polepole.

**MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge ambaye alikuwa anaendelea kuzungumza kwamba masuala ya Chama cha Mapinduzi yanazungumziwa kwenye vikao vya Chama cha Mapinduzi.

Hapa Bungeni Wabunge wana uhuru wa kutumia uhuru wa Bunge kuzungumza lakini kinachozungumzwa huku ndani hakiathiri msimamo wa Chama cha Mapinduzi ambao tumekwishakuutoa. Msemaji wa Chama ni Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na kama si yeye mimi husema kwa niaba yake, Mheshimiwa Rais hataongeza muda lakini isizuie watu kuzungumza huku Bungeni. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib, nadhani umeipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea si ni nzuri! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wale wenzangu ambao wanadhani kuja hapa wakasema Rais atake asitake, hataki sasa, mwamtafutia nini? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo na utawala bora, Mahakama imejenga majengo mengi lakini kujenga majengo ya mahakama, shule na hospitali lengo ni kutoa huduma kwa wananchi. Ili huduma zipatikane, ni lazima iambatane na mambo mengine, watendaji na vifaa ni muhimu katika kukamilisha majukumu ya Mahakama. Mahakama ni *industry* na ili iweze kuwa *productive* ni lazima ipate *material*. *Material* ya Mahakama ni Waendesha Mashtaka kupeleka ushahidi kwa wakati ili kuzifanya Mahakama ziweze kutenda kazi zake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlundikano wa mahabusu si utawala bora, nchi yenye utawala bora...

Mheshimiwa Mwenyekiti, unanipa dakika tatu za nyongeza?

**MWENYEKITI:** Hapana. (Kicheko)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Shukurani. Mheshimiwa Hussein Nassor atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isaac Mtenga na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango uliopo mbele yetu. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wenyewe kwa sababu ni dakika tano, nijikite sana kwenye ushauri na napenda Waziri wa Fedha ajaribu sana kusikiliza ushauri wangu. Mheshimiwa Rais alituita pale Ikulu sisi kama wafanyabiashara na wadau mbalimbali kutaka kujua changamoto tulizonazo kwenye upande wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimwelezea changamoto zetu ikiwemo tatizo kubwa lililoko bandarini kuhusu *TRA*. *TRA* kule bandarini wana usiri mkubwa. Usiri huu unasababisha watu kukwepa kulipa kodi na tozo mbalimbali, lakini pia unasababisha kupoteza mapato makubwa ya Serikali. Mfano, leo hii utakwenda China ama mtakwenda China watu watatu ama wanne mnaofanya biashara ya aina moja, mnakwenda kununua mabegi kila mmoja *container* moja, lakini mnapofika bandarini kila mmoja analipa kodi tofauti na mwenzake, hii ni kwa nini? Wajaribu kuangalia usiri uliopo bandarini, kuna usiri mkubwa sana. Kama alivyosema yule mchangiaji mwingine, leo hii Mtanzania anaona bora kufuata mzigo Uganda na kuuleta Tanzania kuliko kufuata mzingo Dubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Uganda mzigo unakuwa na bei ya chini kuliko Tanzania, wakati tumetumia bandari yetu, barabara yetu kusafirisha mzigo kwenda Uganda. Inakuwa hivyo kwa sababu hapa kuna utitiri wa mambo mengi, *TRA* wajaribu kuangalia tatizo hili lililoko bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine nitautoa kwa pale bandarini. Leo hii unaingia dukani ama madukani,

unaingia duka moja unakwenda duka linguine, unaingia kwenye duka hili mtu anakupa bei anakwambia hii ni ya risiti ya VAT; bei hii haina risiti haya yametokana na nini? Mwanzo wa kule bandarini. Biashara nyingi leo zimekufa kwa sababu kuna *double standard* ya kulipa kodi, nina Ushahidi, nimeingia duka moja nikaenda nikanunua mzigo wenye thamani ya milioni 35, nikapewa risiti ya milioni 1,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamwambia yule mama wewe hujipendi nipe risiti iliyo kamili, sheria gani inakulinda wewe ya kutoa risiti nusu, lakini cha ajabu ni kwamba mpaka leo hii mchezo huo upo na TRA walitangaza kwamba anayenunua ahakikishe anapewa risiti na anaomba risiti, cha ajabu leo hii mtindo huu wa kununua na kuuza hakuna anayetoa risiti. Fedha nyingi za mapato ya Serikali yanapotea, lakini cha ajabu, sheria hii hatujawahi kuipitisha Bungeni ya kwamba mtu akikamatwa hajatoa risiti ama amekamatwa amenunua na hakuomba risiti atatozwa faini ya kuanzia 30,000 mpaka 1,500,000, mambo haya yamepitishwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu leo hii kuna hawa Machinga (wafanyabiashara wadogo wadogo) wanauza bidhaa zenye thamani kubwa na hawatowi risiti, TRA hawaoni kama wanapoteza mapato? Nina ushahidi nimenunua brenda ya juisi ya shilingi 120,000 kwa mfanyabiashara huyu anayeitwa Machinga hajatoa risiti, lakini leo hii ukiingia *supermarket* hata ukinunua pipi unapewa risiti, wajaribu kuangalia sana TRA kuna maeneo wanapoteza mapato. Ushauri wangu wahakikishe wafanyabiashara kuanzia hao wadogo, wa kati na wakubwa waunganishwe kwenye mfumo wa ulipaji kodi EFD yaani wahakikishe kila mmoja anagawiwa hiyo mashine hata bure ili aweze kutoa risiti, tuna mapato mengi ambayo tunapoteza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia Mheshimiwa Waziri anasema tumevuka malengo, sasa hivi tunakusanya trilioni mbili kwa mwezi. Kwa uzoefu nilionao kuna trilioni zaidi ya tano ziko kule nje, zinapotea hivi hivi. Namwomba Mheshimiwa Rais kama itampendeza, sisi wafanyabiasha

ambao tunaitwa wa darasa la saba elimu, yetu ya msingi tumo wengi humu ndani, tunamiliki uchumi wetu, kama itampendeza achague angalau hata watu wawili hao wenye elimu ya darasa la saba wakawe Manaibu Waziri, upande wa Wizara ya Fedha ama Viwanda tuweze kuwashauri vizuri, haya tunayoyazungumza, kwa sababu tuko ndani ya *field* tunayaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Musukuma alitoa ushauri na namuunga mkono kwamba *TRA* watengeneze vijarida ama vitabu vya kuonyesha uhalisi na uhalali wa kulipa kodi. Waende wakajifunze Uganda, kwa nini ukienda Uganda unataka kufuata gari, unataka kufuata *TV* unaambiwa na Mamlaka ya Mapato yao, ukileta *TV* yako utalipa bei hii. Mtu anakwenda kununua bidhaa yake kule nje anajua nikifika hapa nitalipa kiasi fulani lakini kwa *TRA* ya Tanzania kuna usiri mkubwa. Nasema *TRA* kuna usiri mkubwa lakini ni wachache siyo wote, nawapongeza wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba watangulize uzalendo...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja, lakini na sisi wa darasa la saba muwe mnasakiliza michango yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Issac Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa David Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nianze kwa kukusahihisha



naitwa Mtinga, sio Mtenga. Mtenga ni Wachaga, Mtinga ni Wanyiramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara ya kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na leo hii nipo kwenye Bunge hili lakini pia niwashukuru wananchi wa Iramba Mashariki kwa kuniweka hapa na Chama changu kukubali wananchi wa Iramba Mashariki wanilete. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni dakika tano naomba niuelekeze mchango wangu kwenye kilimo. Sote tumesema hapa kwamba kilimo ndiyo ajira kuu kwa Watanzania, lakini kuna mambo mengi sana kwenye kilimo ila jambo ambalo limeonekana ni ufumbuzi na halijafanyika vizuri mpaka sasa, ni suala nzima la kilimo cha umwagiliaji. Mabonde tunayo mengi na mengi yameshawekewa miundombinu, lakini hata hayo yaliyowekewa miundombinu bado yanafanya kilimo kidogo sana na sehemu kubwa inabaki haitumiki na hayo mengine ambayo yanafaa pia bado hajawekewa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri katika kilimo; rafiki yangu Mheshimiwa Bashe nimemwona mara nyingi sana anaongelea *global family* na nimpongeze amepita maeneo mengi na kuona jinsi ambavyo Serikali imeweka fedha na wananchi bado hawatumii vizuri; nchi yetu tuna hazina kubwa ya watu waliosoma mambo ya kilimo, lakini pia tuna hazina kubwa ya watu waliofanya kilimo pamoja na kuwa hawajasoma. Sasa ningeshauri kwamba katika maeneo haya ya umwagiliaji, Serikali iwekeze kila kitu kwenye maeneo hayo, kuanzia miundombinu, lakini vile vile na kuweka na viwanda vidogo kwa maana ya kuya-*add value* yale mazao katika maeneo yale. Baada ya kukamilisha, wawakopeshe vijana kuanzia wale wasomi wa chuo kikuu mpaka vijana wa mtaani wa darasa la saba kwa kuwakabidhi maeneo yale na kuwasimamia, walime warejeshe ule mkopo na baada ya hapo maeneo hale yabaki kuwa ya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maeneo mengi na kama Serikali itasimamia kwa kuwekeza namna hii, nina hakika tutazalisha na wale vijana watakuwa wamepata ajira. Hii itatuletea kipato, itatuletea uhakika wa chakula, uhakika wa mazao ya biashara kwa ajili ya viwanda, lakini vile vile itatibu suala nzima la ajira. Kwa hiyo nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Bashe hiyo kazi aliyoianza aifanye vizuri zaidi aiendeleze na ahakikishe kwamba maeneo yale ambayo yamewekezwa yanafanya kazi iwezekanavyo na haya mapya fanyeni utaratibu wa kuwakopesha vijana wa nchi hii, wasomi wapo na wasiosoma wapo na wanahitaji wakabidhiwe vitu hivi kama mkopo, wakimaliza wanaendeleza na maeneo mengine yanaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka niende kwenye eneo lingine la ukuaji wa miji. Ni kweli Serikali yetu inawekeza kwenye miundombinu, leo hii ukipita Dar es Salaam unaona barabara za juu, unaona hizo *interchange*, lakini cha kusikitisha miji yetu haikui, miji mpaka sasa ina vibanda mjini, nyumba za ajabu ajabu, sasa mji haupendezi, mji una barabara za juu, lakini nyumba ni vimakuti vimejaa mjini na vibati vya ovyo ovyo, wakati huo huo watu wanaendelea kuwekeza nyumba za maana mbali na watu hawaendi kuishi huko. Kwa mfano, Kigamboni, nyumba za *NSSF* hazina watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kwamba wizara inayohusika katika miji yetu iwatambue wale watu wenye maeneo yale ya zile nyumba ndogo ndogo na vibanda. Ikishawatambua ifanye utaratibu wa kubomoa na kujenga upya mji, maghorofa ya kutosha, baada ya hapo wale watu wapate *unit title*. Kwa hiyo tutakuwa tumejenga mji na wale ambao maeneo yao walivunja watapata *unit title* kwenye yale maghorofa na watu wengine sasa watapata miji na hapo Serikali kwanza itapata kodi lakini mji utapendeza na miji yetu itaendana na miundombinu inayojengwa kwa sasa. Tukiendelea kuacha vibanda mijini tunakwenda kujenga mbali, matokeo yake tuna barabara nzuri lakini mtu akiangalia anaona vibanda viko mjini na miji yetu haiendelei kupendeza na tunazidi kukosa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwenye miundombinu, nchi hii sasa inaunganishwa na tunawaza kuunganisha barabara za wilaya na wilaya. Hata hivyo, katika Mkoa wangu wa Singida na hasa katika jimbo langu barabara inayounganisha Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Singida ambao unapita kwenye Jimbo langu la Mkalama ni muhimu sana ikaangaliwa. Tumejenga daraja kubwa la Mto Sibiti zaidi bilioni 28, sasa tulitumie daraja lile kwa kuweka barabara ya lami ili kuunganisha mikoa hii. Pamba yote sasa inayotoka kule inasafirishwa kupitia njia hii ya vumbi, naamini barabara hii ikijengwa kwa haraka na ipo kwenye Ilani, itasaidia sana kukuza uchumi na kuunganisha mikoa yetu na kuendeleza Mkoa wangu wa Singida na hasa Jimbo langu la Mkalama ambapo barabara hii inapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele imelia, dakika tano ni chache, naunga mkono hoja. Ahsante sana.  
(Makoff)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Jonas Mbunda ajjandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mapendekezo ya Mpango huu. Naomba pia nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama siku ya leo nikiwa na afya tele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kidogo kwenye sekta ya viwanda. Nilikuwa napitia hapa kwenye sekta ya viwanda; katika ukurasa wa 32, nilikuwa nasoma hapa kati ya mwaka 2015 – 2019, kuna viwanda vipya 8,477 vimeongezeka. Katika viwanda hivyo wameonyesha viwanda vikubwa, viwanda vya kati, viwanda vidogo na viwanda vidogo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la ajira katika kipindi cha mpaka mwaka 2015 lilikuwa ni 254,786; lakini 2015 – 2019, ajira zimeongezeka kufikia 482,601. Sasa ukiangalia

ukurasa wa 33 Mpango unasema baada ya Serikali kuomba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wameweza kutengeneza viwanda 35 ambavyo katika viwanda hivyo vimetengeneza ajira 250,000. Sasa nataka nifahamu kwanza je, hivi viwanda 35 ni tofauti na viwanda 8,477 na kama siyo tofauti, je, ajira zilizoongezeka ni ngapi? Ni hizi 227,000 zinazoongezeka katika 482,000 ama 250,000 ni ajira tofauti na hizi nyingine na 227,000. Hapa kidogo nimepata changamoto na nikaona bora niulize ili wakati Waziri anakuja ku-*wind up* atuambie *exactly* kati ya 2015 - 2019 ni ajira ngapi zimetoka kwa Watanzania kupitia sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda, mwaka 2015 - 2020 ndiyo ilikuwa *slogan* ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, lakini tunaona ni kwa namna gani bado hatukutimiza lengo ambalo tulikuwa tumekusudia, kama ambavyo mipango ilikuwa ilikuwa inaonyesha. Leo Serikali ilikuwa na viwanda vilivyobinafsishwa na mpango wa Serikali ulikuwa vile viwanda vilivyobinafsishwa kwa wale watu ambao walikuwa hawaviendelezi, viwanda vile vichukuliwe na Serikali. Nilitegemea sasa, baada ya Serikali kuzungumza na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ingekwenda moja kwa moja kwenye vile viwanda vilivyokuwa na tija wakawapa watu na viwanda vile vikawa havifanyi uzalishaji wangevichukua ili kuendeleza tija iliyokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea mfano, Kiwanda cha *General Tyre*, Serikali ina ubia asilimia mia moja, kiwanda kile ni cha Serikali. Kuna Kiwanda cha Urafiki, kiwanda hiki kilikuwa kinazalisha vizuri sana, *demand* ya nguo za urafiki huko uraiani ni kubwa kuliko tunavyofikiria. Cha ajabu, Serikali ina ubia wa asilimia 49 na mchina ana ubia wa 51, tuliishauri Serikali hapa kwa nini tusichukue kiwanda kile sisi wenyewe ili tuweze kupata faida, lakini pia kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma Kiwanda cha Urafiki kilikuwa kinaajiri Zaidi, kipindi ambacho hatujaingia ubia na Wachina, lakini tangu tumeingia ubia na Wachina, kiwanda hiki, ajira zimepungua kutoka zilizokuwepo

zimepungua kwa asilimia zaidi ya 70. Leo ninapozungumza kiwanda kile haki-*operate* na hata kama kinafanya kazi walioko pale ni wale viongozi wakubwa tu na kiwanda hiki ni cha kwetu sisi Watanzania, kwa nini tusiwekeze kwenye kiwanda hiki ili kuleta tija kwa sababu tayari Serikali ina ubia wa kutosha katika kiwanda kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali, viwanda vyote ambavyo tunadhani na tunaona na tunajua kwamba viwanda hivi vilikuwa vinaleta tija kwa Taifa, vinatoa pato kubwa kwa nchi, Serikali iweze kuvirejesha. Hii Mifuko ambayo Serikali inakwenda kuchukua fedha, fedha hizi ni za Watanzania, je, hivi viwanda vilivyowekezwa kuna uhakika gani kwamba, fedha hizi zitarudi kwenye Mifuko kwa wakati ili Watanzania wanaostaafu waweze kupata fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa Watanzania wengi katika Mifuko hii kulalamikia mafao yao, lakini leo tumechukua fedha tumekwenda kuwekeza kwenye viwanda 35, lakini kwenye Mpango vinaonyeshwa viwanda vitatu sijui vinne, hatujaonyeshwa hivyo viwanda 35 vyote ambavyo vimewekezwa, lakini tangu uwekezaji umefanyika, je, tumeona kuna tija katika uwekezaji na fedha hizi za Watanzania hawa zitarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali, badala ya kupelekapeleka tu fedha kwenye maeneo ambayo hayana tija, tuangalie viwanda hivi ambavyo tunaamini vina tija. Leo kiwanda cha *General Tyre* kifufuliwa nawaambia Watanzania wengi wana magari, tukaamua moja kwa moja hakuna kuagiza matairi kutoka nje, nawaambia hivi, kile kiwanda kitakuwa kina tija, kitaleta ajira, lakini pia kitaongeza mchango mkubwa kwenye pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda ambavyo vilikuwa ni viwanda vya magunia, sasa hivi hata haya magunia ya *sulphate* ambayo tunatumia wakulima kuweka vitu vyetu wanasema hayafai. Kwa nini viwanda vile

visifufuliwe ili magunia yetu ya kizamani yakarudi ili tuweze kupata vifungashio ambavyo vinatakiwa kuliko ilivyo hivi sasa, vifungashio vya sandarusi ambavyo watu wa mazingira wanapiga marufuku. Kiwanda hiki kingefufuliwa kingesaidia kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Kiwanda cha Nyuzi ambacho kilikuwa katika Mkoa wa Tabora peke yake. Kiwanda hiki ni kiwanda cha muda mrefu. Kilianza kujengwa hata mimi sijazaliwa lakini baada ya hapo kiwanda hiki, baada miaka 10 toka 1975 - 1985 kiwanda hiki kilianza kufanya kazi. Baada ya miaka kumi mwaka 1995, kiwanda hiki kilikufa na kilipewa mwekezaji; mwekezaji huyu ameshindwa kukifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika pale, Naibu Waziri wa Kilimo kaka yangu Mheshimiwa Bashe alifika pale, waliona hali halisi na ukweli uliopo. Serikali wawekeze kwenye viwanda vyenye tija, Tabora tunalima pamba, Mikoa ya Kanda ya Ziwa inalima pamba, ni rahisi kuchukulika pale na kupeleka Tabora kutengeneza nyuzi zetu kama ilivyokuwa hapo zamani. Ili kuipa uhai TABOTEX Watanzania wa Kanda ya Ziwa na Mkoa wa Tabora waweze kupata ajira lakini Serikali iweze kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mpango lakini pia mpango bila afya bora hatuwezi kufika. Hapa tumeona Mpango umesema kwamba vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua vimepungua kutoka 432 hadi 321. Vifo hivi ni vingi sana na vifo hivi vinatokana na umaskini wa wanawake wengi ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za matibabu. Vifo hivi ni vifo ambavyo vinajulikana ambavyo vimesajiliwa kwenye hospitali; niambie vifo vinavyotokea kwa watu wanaojifungulia nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi sasa hivi kutokana na gharama ya kujifungua wanawake wengi wameamua kujifungulia nyumbani. Hata hivyo, wanawake wengine wanapokwenda katika hospitali, anapofika maeneo ya hospitali hana uwezo wa kulipia ile hela wakati

akisubiri apate msaada wa hela, wanajifungua wakiwa njiani. Hayo tumeyashuhudia na tumeyaona. Kwa hiyo, vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua bado ni vingi, hatuhitaji hii takwimu, tunachohitaji katika Mpango huu vifo viondoke kabisa na siyo kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukizungumza sana kuhusiana na masuala ya afya, elimu na maji lakini miaka 61 ya uhuru wa Tanzania bado tunazungumzia afya, maji na elimu. Hebu ifike mahali tukiwa tunaingia kwenye Mpango hizi biashara ziwe zimeshakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi tajiri ambayo hatupaswi kwa sasa kukaa kuendelea kuzungumzia mipango ya afya. Afya tungenesema sasa tunaboresha ama magonjwa ya mlipuko kama Corona na magonjwa mengine yanayotokea ndiyo tungekuwa tunazungumzia sasa lakini siyo afya ya uzazi, mtoto, mama wala ya mwananchi yeyote; hizo zingekuwa ni historia. Toka miaka 61 ya uhuru mpaka leo bado tunazungumzia matatizo ya afya, tuache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato David Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Mbunda, Mheshimiwa Nape Nnauye ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa dakika tano kwa kweli kuchangia ni chache nitakwenda moja kwa moja katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajielekeza katika Sehemu ya Tatu ya Mpango huu wa Tatu inayozungumzia kukuza ushiriki wa sekta binafsi kwenye maendeleo ya kiuchumi. Mipango yetu ni kutengeneza ajira milioni 8 na katika kutengeneza hizi ajira asilimia karibu 80 tunategemea zitoke katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika Taarifa ya *World Bank* na ambayo imo katika Mpango huu ambao Serikali imeuwasilisha, hiyo Ripoti ya *Easy Way of Doing Business*, sisi Tanzania tuko nafasi ya 141. Pamoja na kuwa kuna kasentensi pale kanasema kwamba tumefanya vizuri kutoka 144, lakini kwangu mimi *if we are serious* kutengeneza ajira milioni nane mimi naona hatujafanya vizuri, lazima ilenge kwenda katika *digits* mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *East Africa* sisi tumeshindana tu na Burundi. Katika *SADC* sisi tunashindana tu na Zimbabwe. Sasa katika hii hali ya kuvutia uwekezaji na kutengeneza ajira milioni nane bila kutengeneza mazingira bora ya kufanya biashara, naona ajira milioni nane zitakuwa ni ndoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yako mambo ambayo lazima tufanye. Mheshimiwa Rais kwenye hotuba amesema tutengeneze mabilionea na tusiogope. Jambo la kwanza ambalo tunatakiwa tusiogope ni kusema uhalisia sahihi lakini suala la pili tusiogope hata sisi wenyewe kuthubutu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya kutengeneza mabilionea mimi nasikitika sana, kule Mafinga unakuta mtu kauza miti yake, milioni 300, 400, sisi kule uchumi tunamshukuru Mungu, inakuja sijui *Task Force, I don't know whatever you call it*, akaunti inafungwa. Mimi nilitarajia niulizwe kwamba wewe Cosato Chumi mfanyabiashara, kwa nini unafanya biashara akaunti haina hata milioni tano, lakini *don't ask me* kwa nini nina milioni 500. Wewe tafuta mbinu zako za Kiserikali, angalia je, hii milioni 500 ya Chumi ni safi au siyo safi? Ukinifungia akaunti *you cripple me down*, tutatengenezaje mabilionea na hizo ajira milioni nane? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii pale Mafinga tozo katika Sekta ya Mazao ya Misitu ziko 13, viwanda vitano vimefungwa. *Imagine* kama kiwanda kimoja kinaajiri watu 300, tayari watu 1,500 hawana ajira. Pia umekosa *SBL* na *PAYE*;



tutatengeneza kweli ajira milioni nane katika mazingira haya?  
(Makofi)

Kwa hiyo, katika kumsaidia Mheshimiwa Rais na Serikali, ni lazima kwanza tuwe wakweli wa nafsi. Ukweli wa nafsi ni lazima kutengeneza mazingira bora ya kufanya biashara. Mimi nasema ni wajibu wetu Wabunge na Serikali kwa ujumla kwa sababu wakati mwingine kweli tutasema *TRA* lakini mimi nimekwenda *TRA* wananiambia hii *SBL* ukiwa hujalipa zaidi ya tarehe 07, penati yake kwa kampuni ni 225,000, kwa *individual* 75,000. Pia hata kama umelipa ila hujafanya *online filing* kuna penati yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa angalia nimelipa lakini bado kuna penati, namuuliza Afisa wa *TRA* anasema bwana, Mkuu hii ni sheria tena na wewe ni Mbunge mlipitisha wenyewe. Kwa hiyo, wao *at some point* wanatekeleza sheria. Kwa hiyo, kuelekea *blueprint* na kutengeneza mazingira bora ya biashara yako mambo ni kisheria yaleteni humu turekebishe. Yako mambo ni Kanuni, Mawaziri wenye dhamana elekeeni huko ili lengo la kutengeneza ajira milioni nane iwezekane. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuelekea huko, pamoja na kutengeneza mazingira bora ya kufanya biashara yako masuala ya miundombinu. Pale Mafinga kwenda Mgololo wakati wa mvua unakuta *semitrailer* kumi zimepaki wiki nzima zimekufa barabarani haziwezi ku-*move*; umesimamisha uchumi. Yale malori yangesafiri kwenda na kurudi ungejaza mafuta, Serikali ingepata *fuel levy* maisha yangeendelea, lakini zipo zimesimama siku tano. Sasa kati ya mambo ambayo tunatakiwa tufanye ni pamoja na suala zima la miundombinu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa Mafinga ukishajenga barabara ya Mafinga – Mgololo kama alivyosema asubuhi ndugu yangu Mheshimiwa Kihenzile na barabara ya Mtwango – Nyololo, una-*speed up* uchumi. Kama Serikali ilikuwa inapata shilingi bilioni 10 matokeo yake utapata shilingi bilioni 50 mambo mengine yataendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika suala hili la kutengeneza mazingira bora ya kufanya biashara ni suala la umeme. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Kalemani, anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kazi nzuri angalieni umeme ni huduma, *at some point* ni biashara. Kule ambako kuna viwanda vingi watu wanataka kuzalisha mtapata pesa kama Mafinga, leta huo umeme. Leta umeme watu wawekeze, tulipe bili zikawapelekee watu umeme sehemu nyingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nakuomba kwa ridhaa yako...

**NAIBU SPIKA:** Muda umeshaiha Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naunga mkono hoja, naomba tuwe wakweli wa nafsi na Mungu atusaidie. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jonas Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa Bonnah Kamoli ajiandae.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya uhai. Vilevile naomba nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kunitewa kuwa mgombea na pia niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Mbinga Mjini kwa kunichagua kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye Mpango wa Awamu ya Tatu wa Maendeleo. Dhima ya Mpango wa Awamu ya Tatu wa Maendeleo ya

Taifa ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Hata hivyo tutajengaje uchumi huu? Ni lazima tuhakikishe kwamba nyanja zote zinazotakiwa zilete maendeleo zimesimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa kwenye suala la kilimo. Ukiangalia Mpango uliopita tulikuwa na malengo ya kukua kwa uchumi kupitia kwenye upande wa kilimo kwa asilimia 7.6 lakini uchumi huo ulikua kwa asilimia 4.4. Ukija kwenye uchangiaji wa pato la Taifa napo tumeshuka. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba kwenye suala la kilimo tumerudi nyuma lakini ukiangalia sehemu kubwa ya wananchi wa Tanzania wanashughulika na kilimo na wako vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya mwisho tunategemea kwamba tutakuja kupata maendeleo ya watu na kuondoa umaskini kwa kupitia kilimo. Tutakapokuja kugawa na kuona kila mwananchi anapata kiasi gani ili aweze kuonekana kwamba ameendelea kimaisha tutaangalia pamoja na idadi hiyo kubwa ya wakulima ambao wako vijijini na bado wanaishi katika maisha ya shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoishauri Serikali kwanza kabisa, kama walivyochangia wenzangu kwenye suala la mbegu tuhakikishe kwamba wakulima wanasaidiwa namna ya kupata mbegu bora. Pia Wizara ya Kilimo isimamie kuhakikisha kwamba wananchi wanapata pembejeo zenye ruzuku. Zaidi ya hapo wananchi hao wasaidiwe kupata masoko ya uhakika hasa wale ndugu zangu wakulima wa kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sasa tuweze kufika kwenye maendeleo, hasa kwenye suala la viwanda, kwenye suala la elimu naipongeza Serikali imefanya vizuri lakini hatujawekeza sana kwenye suala la elimu ya ufundi. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwenye suala la elimu ya ufundi ijitahidi kujenga vyuo vya *VETA* kwenye wilaya zetu ili suala la ufundi lifike kwa wananchi wetu na waweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili viweze kusaidia kwenye suala la maendeleo

ili tuweze kufikia uchumi wa viwanda na wananchi hawa waweze kupata unafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kupata maendeleo lazima pawe na umeme wa uhakika. Naomba niipongeze Serikali kwa kujenga miundombinu mingi ya umeme na kugawa kwenye maeneo mbalimbali lakini tatizo kubwa lipo katika upatikanaji wa umeme wa uhakika. Katika Jimbo langu la Mbinga Mjini, kila mara natumiwa meseji za kunijulisha kwamba umeme umekatika. Kwa hiyo, tutashindwa kabisa kufanya kazi za maendeleo kama tutakuwa hatuna umeme wa uhakika katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nape Nnauye, atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mheshimiwa Yahya Mhata ajjandae.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtama kwa kuniamini na kunipitisha bila kupingwa kuwa mwakilishi wao ndani ya Bunge hili, nakishukuru pia chama changu, Chama cha Mapinduzi, kwa kunipa dhamana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kwa kuwa muda hautoshi, naomba nizungumze mambo mawili. Mpango huu ni mzuri sana lakini utafanikiwa tu ikiwa kutakuwa na fedha za kuutekeleza. Fedha zinapatikana kutoka kwenye makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa sana inaendelea katika nchi yetu. Ukusanyaji wa kodi ni taaluma na katika historia ni taaluma ya muda mrefu sana. Changamoto tuliyonayo ni kwamba tumeamua kuacha kuwatumia wataaluma ambao ndiyo wakusanya kodi badala yake tunatumia *Task Forces* kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Task Forces* kwa sababu siyo taaluma yao, wanachofanya wanakwenda kuua biashara. Kelele hizi zote unazosisikia ni kwa sababu tumeamua kuacha kutumia taaluma ya ukusanyaji wa kodi, tumeamua kutumia *Task Forces* kukusanya kodi na kwa sababu siyo taaluma yao wanachoangalia ni kufikia lengo walilowekewa. Kinachotokea ni kwamba wanakwenda kwa mfanyabiashara, hawajali maisha yake ya kesho, hawajali kwamba wanatakiwa wakusanye kodi leo wamuachie uwezo wa kuzalisha ili wakusanye na kesho. Tunafurahia matokeo ya muda mfupi; ni kweli tumefanya kazi nzuri ya kukusanya kodi, lakini haya matokeo tunayoyafurahia ni ya muda mfupi sana kwa sababu idadi ya biashara zinazofungwa ni nyingi mno, kesho hatuna ng'ombe wa kumkamua maziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, hebu punguzeni habari ya *Task Forces* kukusanya kodi, siyo kazi yao, hawa wanakwenda kuua biashara. *TRA* ilianzishwa kwa kazi hiyo na watu wamesomea. Tukijiwekeza kwenye *Task Forces* kesho hatutakuwa na cha kukusanya kwa sababu siyo kazi yao. Nimeambiwa baadhi ya maeneo wanakwenda na *draft* ya kesi za uhujumu uchumi, wanawatisha watu, watu inabidi watoe fedha, wakitoa fedha wanafunga biashara zao. Sasa mwendelezo wa hiki tunachokifanya mwisho wake utakuwa nini? Ushauri wangu Serikali ondokeni kwenye *Task Forces*, rudini kwenye taaluma ya ukusanyaji wa kodi itatupa uhalali wa kuendelea kukusanya hiyo kodi kesho na kesho kutwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili, tumefanya vizuri sana kwenye kuungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu kwenye Sekta ya Elimu. Tumetoa elimu ya msingi bila malipo kwa kipindi cha miaka mitano; siyo kazi ndogo. Hata tulipofanya uamuzi huu tulijua ni kazi kubwa. Nampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutekeleza jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu; tumetekeleza kwa kipindi cha miaka mitano, tumefanya vizuri

lakini bila shaka umefika wakati tupitie changamoto tulizokutana nazo katika kipindi cha miaka mitano halafu tufanye marekebisho kwa baadhi ya maeneo. Hapa ntatoa mfano, tunatumia kigezo cha idadi ya wanafunzi kupeleka fedha, kigezo hiki nadhani kimepitwa na wakati, twende tutanue. Kwa sababu mtu mwenye watoto kumi na mwenye watoto 200 baadhi ya mahitaji yanafanana, ukimpelekea fedha ileile unamuua huyu mwenye watoto wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ni vema Serikali tupitie upya, tuangalie hivi vigezo tunavyovitumia vya kupeleka fedha kusaidia elimu bure. Jambo hili ni jema lakini tupitie upya tuliboreshe, tulifanye vizuri ili tuongeze vigezo vya kupeleka fedha. Fedha za utawala zizingatie mahitaji ya kiutawala. Fedha za kuangalia mwenendo wa watoto, *performance* yao zifuate hivyo vigezo vingine lakini tuongeze idadi ya vigezo; nadhani hili jambo litatusaidia twende mahali pazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Mhata, Mheshimiwa Boniface Mwita Getere ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Segerea kwa kunirudisha kwa awamu ya pili lakini shukrani za pekee ziwaendee wajumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika Mpango wa Miaka Mitano ambao Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameweza kuuwasilisha hapa. Napenda niweke mawazo yangu katika huu Mpango; napendekeza kwamba kuwepo na mpango kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwenye suala la miundombinu. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia kwa sasa hivi Mkoa wa Dar es Salaam unachangia mapato makubwa katika Taifa na ni mkoa wa kibiashara lakini pia

ndiyo Mkoa ambao una Manispaa sita katika mikoa yote ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba katika Mkoa wa Dar es Salaam miundombinu iliyopo sasa hivi mvua ikinyesha kwa nusu saa Dar es Salaam nzima inasimama. Katika kusimama huko mapato mengi yanapotea kwa sababu watu wanapokuwa hawafanyi kazi wanasubiri mvua iishe au kuna mafuriko ambayo yametokea, hakuna mama ntilie ambaye anapata wateja, hakuna bodaboda ambaye anatembea lakini pia kunakuwa kuna mambo mengi ambayo yanasimama kutokana na miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo ni kwamba katika huu Mpango wa Miaka Mitano Serikali ije na mpango wa kuhakikisha kwamba Mkoa wa Dar es Salaam unatengenezwa miundombinu ambayo itakuwa ya *permanent*. Kwa sababu kwa sasa hivi kila mvua inaponyesha Mkoa wa Dar es Salaam lazima tuchukue siku tatu au nne tunahangaika na mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika bajeti yetu hii ya mwaka. Mfano bajeti ya *TARURA*, kwa Manispaa ya Ilala wanapata bilioni tano, bilioni tano inatengeneza barabara moja na ukiangalia Wilaya ya Ilala kilometa 1,200 bado hazijawekewa lami. Kwa hiyo, tukifuata hii bajeti ambayo ni ya mwaka kwa mwaka katika Mkoa wa Dar es Salaam, hatuwezi kufikia malengo ambayo tunataka kuyafikia. *TARURA* wakipewa shilingi bilioni tano, wanatengeneza barabara moja. Mfano sasa hivi kuna barabara moja ambayo inatengenezwa; barabara ya Vingunguti – Barakuda ambayo ina kilometa 7.6. inatengenezwa kwa shilingi bilioni 7.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *TARURA* wanapata shilingi bilioni tano kwa mwaka kwa majimbo matatu, nikimaanisha Jimbo la Ilala, Segerea pamoja na Ukonga, ina maana haya majimbo mengine yote mawili yatakuwa yamekaa hayafanyi kitu chochote na wala hawana fedha

za ukarabati. Ukiangalia Mkoa wa Dar es Salaam, Kata ambazo ziko pembezoni mwa mji, *water table* yake iko juu sana. Kwa hiyo, barabara yoyote ambayo inatakiwa kutengenezwa na iweze kudumu, basi hiyo barabara inatakiwa iwe imepangiwa fedha nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie ni jinsi gani italeta mpango ambao unaweza ukaenda kufanya kazi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa sababu ukizungumzia Dar es Salaam, siyo sawa na Bukoba, siyo sawa na Kigoma na wala Shinyanga.

Kwa hiyo, sisi watu wa Dar es Salaam na wananchi wetu ambao wako Mkoa wa Dar es Salaam, wanachangia mapato makubwa katika Taifa. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali, ili tumalizane na hili jambo la mafuriko, maana kila mwaka tunapata mafuriko zaidi ya mara mbili au mara tatu. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili tumalizane na hili jambo la mafuriko, tunaomba Serikali ije na mpango ambao utaweza kumaliza mafuriko ya Dar es Salaam kwa mara moja. Hili jambo linaweza likatusaidia, wananchi wetu waweze kuendelea kufanya kazi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililokuwa nataka kuongelea ni kuhusiana na Miradi ya *DMDP* ambayo inaboresha makazi. Hii miradi *phase* ya kwanza imemalizika, sasa tunaenda *phase* ya pili, lakini mpaka sasa hivi hii miradi imesimama. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iweze kufanya mpango hii miradi iweze kuendelea kwa sababu ndiyo inayoleta matokeo ya moja kwa moja kwa wananchi. Kwa hiyo, naomba sana katika huu Mpango, Serikali ije na mpango maalum katika Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)



**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bonnah Kamoli. Mheshimiwa Yahya Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniface Mwita Getere na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Mpango huu, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Nanyumbu kwa kura nyingi walizonipatia katika Uchaguzi Mkuu ullopita. Nami nawaahidi wasiogope, niko hapa kwa ajili yao na nitawawakilisha kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika kuchangia Mpango huu wa Mwaka Mmoja na wa Miaka Mitano uliowasilishwa jana. Kwanza naomba nijielekeze katika sekta ya afya, jinsi gani itakavyoweza kuongeza mapato yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *medical tourism*. Tumeona jinsi gani sekta ya afya ilivyoweza kupiga hatua katika miaka mitano iliyopita. Tumeona zahanati karibu 1,198, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya 99, Hospitali za Rufaa 10 na Hospitali za Kanda tatu. Sasa hospitali hizi zinawezaje kuongeza uchumi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukulia mfano wa India, wameweza kutumia sekta ya afya kuongeza mapato katika nchi yao. Tunajua wagonjwa wengi walikuwa wanakwenda India. Ni wakati wetu sasa hivi nasi kutumia hospitali zetu kuwavutia wagonjwa kuja katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna balozi zetu katika Afrika. Tutumie balozi zetu kutangaza huduma bora za hospitali zetu. Hawa wakija, watakuja na dola, wataacha katika nchi yetu. Wakija kutibiwa watafanya *shopping*, wata-*stimulate* uchumi wetu. Kwa hiyo, ni vizuri balozi zetu zitumike kikamilifu katika kuitangaza nchi yetu hasa huduma za afya ambazo tumeziboresha zaidi. (*Mkofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nishawishi, katika zile wilaya ambazo ni pembezoni, mfano Wilaya yangu ya Nanyumbu tumepakana na Msumbiji, nilitarajia kabisa Hospitali yetu ya Wilaya ikapatiwa vitendea kazi vizuri ili wagonjwa wale wa mpakani waje kutibiwa katika nchi yetu. Wakija watakuja na dola, wataziacha ndani ya nchi yetu na halikadhalika uchumi wetu unaweza kukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni upande wa madini; tumeona jinsi gani Serikali yetu ilivyofanya katika kuhakikisha kwamba katika miaka mitano iliyayo inafufua Shirika letu la *STAMICO* ili kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kujikwamua kiuchumi. Hili eneo la madini ni zuri sana endapo litatumika katika kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Nanyumbu tunayo madini, lakini nina masikitiko makubwa kwamba yameachwa bila kuendelezwa. Wizara ya Madini imefungua duka la ununuzi wa madini, lakini nikawa najjuliza, duka hili linamnufaisha nani? Kwa sababu madini yapo, lakini kuna mgongano mkubwa kati ya Wizara ya Madini na Maliasili. Vijana wanataka kwenda kuchimba madini, wakienda wanakutana na *PFS*, wanaambiwa hakuna kuingia msituni. Wakienda wanakutana na *TAWA*, hakuna kuingia. Sasa kuna *contradiction* hapo, madini yapo lakini hizi Wizara mbili zinagongana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hizi Wizara mbili zitusaide vijana wetu ili waweze kufanya shughuli zao, wafuate taratibu gani mahali ambapo pana madini lakini yapo ndani ya msitu? Madini yale lazima yakachimbwe, kwa sababu madini hayapatikani kiholela, hayapatikani barabarani, yapo ndani ya msitu au mbuga. Kwa hiyo, naomba hizi Wizara mbili, nami nawashauri sana, madini haya yasipochimbwa, yatachimbwa kwa njia ya udanganyifu. Kule kwetu mpakani tusipoangalia, wale majirani zetu watakuja kuyachukua na hatutapata chochote. Naomba sana tutumie nafasi hii kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira kwa hizi Wizara mbili kufanya kazi kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kilimo. Kilimo chetu sisi watu wa Kusini hasa Wilaya yangu ya Nanyumbu tunalima sana korosho. Mwaka 2020 tumeathirika sana na uzalishaji wa zao la korosho, lakini Wizara haijaja na majawabu kwa nini zao la korosho halikuzalishwa? Nilitegemea Wizara ya Kilimo itueleze uzalishaji umepungua kwa sababu ya moja, mbili, tatu; vinginevyo tunawavunja nguvu sana wakulima wetu. Wamefuata taratibu zote lakini korosho hazikuzaa na Wizara imekaa kimya. Kwa hiyo, tunategemea Wizara itusaidie.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni ufuta. Tumeza ufuta kwenye vyama vya msingi, hatujalipwa fedha zetu. Wakulima hawajalipwa. Wizara itusaidie, vyama vya ushirika vinatungusha. Tunaomba wakulima wale walipwe fedha zao ili iwa-*motivate* mwakani walime tena.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu. Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile ajiandae.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Bunda kwa kunipa nafasi hii. Naishukuru Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kufanya kazi nzuri sana kwa Awamu hii ya Tano iliyopita na kusema kweli wamefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa, lakini moyo wake wa kutufanya

sisi tuwe humu ndani kwa kuwa na kauli moja tu ya kusema *corona* ipo na itaendelea kuwepo lakini sisi tutaendelea kufanya kazi. Kwa heshima yake na kwa Mwenyezi Mungu, tutafika huko tunakokwenda. Niwaambie, hili suala la *corona* halitaisha, litaendelea kuwepo, kwa hiyo, mkiendelea kuogopa, mtaogopa mpaka mnaisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze habari ya viwanda. Nimesikia wenzangu wengi wanazungumza kuhusu viwanda. Katika karne hii ya viwanda na teknolojia kubwa hatutegemei huko tunakokwenda kuwa na viwanda ambavyo vitaajiri watu wengi. Kwa sababu duniani kote kuna aina mbili za viwanda ukiacha mambo ya cherehani na vitu vingine. Kuna *capital intensive industry* na kuna *labour intensive industry*. (Makofi)

Mhshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, viwanda hivyo viwili, *capital intensive* ni kiwanda chenye kutumia mitaji mikubwa, lakini wafanyakazi wachache; na *labour intensive* iliyokuwa inatumika kwenye karne ya 19 kurudi nyuma inatumia mtaji mdogo lakini wafanyakazi wengi. Huko tunakokwenda hatutakuwa na viwanda vya *labour intensive*, kwa sababu teknolojia yenyewe inakataza kuwa na viwanda vingi kwa eneo moja kwa maana ya *climatic change*. *Greenhouse gases* inakuwa kubwa na watu wanaleta matatizo mengine ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukubali huko tunakokwenda, kwenye nchi yetu tuwe na viwanda hata vya kanda tano vikubwa ambavyo vinaweza kufanya kazi nzuri. Mtu mmoja aliniambia ukileta kiwanda cha nyanya hapa ukawa unasaga tani 500 kwa siku, hakuna nyanya hapa Tanzania. Hakuna sehemu wanalima nyanya za kutosha kwa kiwanda hicho. Kwa hiyo, *labour intensive* ni kiwanda kikubwa kinachojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuna Kiwanda cha Ngozi cha Arusha, tunataka kiwe kikubwa, lakini *stores* zake zijengwe Mara, Shinyanga na Mwanza. *Stores* zile ziwe za kutunza ngozi na kusafirisha kupeleka kiwandani. Hivyo

ndivyo viwanda tunavyovitaka sasa hivi. Viwanda ambavyo ajira yake ni Watanzania ambapo watoto wetu wanaotoka mashuleni wawe wanaajiriwa kufanya kazi ya kukusanya ngozi, kuwa *agents* wa ngozi na mazao. Kwa hiyo, hivyo ndiyo viwanda. Tunataka kuwa na kiwanda kikubwa cha *capital intensive*, tunaweza kukiweka hata Singida au Mwanza Kiwanda cha Alizeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna yale mambo ya kilimo tuliyazungumza sana, lakini nashangaa sijui kuna giza gani limetokea Tanzania. Tunazungumza mazao ya mafuta Tanzania, lakini alizeti inalimwa kila mahali. Yaani tumeshindwa kutamka tu kwamba tunataka tani ngapi za alizeti na soko liwepo tuweze kufanya kazi hiyo vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema viwanda vya sasa kusema kwamba vitaajiri watu wengi, itakuwa ndoto. Kwa hiyo, tutengeneze mazingira ya viwanda vinavyofanya kazi, lakini ajira yake iwe wajasiriamali, siyo kwenda maofisini kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze habari ya maji; na hili Waziri wa Maji anielewe na Waheshimiwa Wabunge wanielewe vizuri. Itakuwa ni ndoto kusema kwamba tutapeleka maji vijijini kwa *style* tuliyonayo. Lazima maji tuyafanye kama *REA*. Lazima twende tukajifunze *REA* ilifanyaje ikapeleka umeme? Tunaposema Kijiji A kina umeme, inawezekana kuna kaya 200 ndiyo zina umeme, kaya 600 hazina umeme, lakini tunasema kijiji kina umeme. Mtu anaweza kwenda kwenye friji akapata umeme pale; kufanya *welding* akapata umeme; tufanye maji kama umeme, yapite mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa mfano mmoja pale kwangu Bunda. Kutoka Bunda kwenda Nyamuswa kwangu ni kilometa 25. Hesabu iliyopigwa kwa *force account* inakuwa ni shilingi milioni 800 badala ya shilingi bilioni mbili. Ukinunua mabomba mita 112, ukinunua yale matenki, ukiweka *DP*; tunataka mabomba yapitie barabarani, ukifika kwenye kijiji waweze *DP* tatu au nne au

sita, yanaendelea hivyo hivyo. Kama yanakwenda Dar es Salaam kutoka Dodoma, kila kijiji barabarani kinapata umeme. Mabomba yaende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mabomba ni ndogo sana, lakini ukipeleka kwa sasa tulivyo tunavyotumia manunuzi hatuwezi kupeleka maji vijijini, lazima maji tubadilishe. Hata hiyo tunayoita *RUWASA*, muundo wake ni shida. Kwa sababu gani? Mkoani mtu aende kupata fedha kutoka wilayani, lazima *DP* tenda yake ifanyike mkoani. Kuipata hiyo hela kutoka mkoani ni ndoto. Kwanza ukiongeza hela, hakuna kitu kinachoendelea hapa ndani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima niishauri Serikali, Waziri wa Maji anafanya vizuri sana...

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri Mheshimiwa Rais anamteua kijana mzuri sana, anafanya kazi nzuri, nawapongeza wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnielewe, marafiki zetu humu ndani ni Mawaziri, huko nje ni kesi. Waziri akikupindisha, umeshaanguka huko pembeni pembeni huko. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile na Mheshimiwa Mohamed Monni ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nianze kwa kusema kwamba jana Mheshimiwa Gambo aliuliza swali ambalo lilikuwa linahusiana na tozo mbalimbali ambazo zimeongezwa kwenye Hifadhi zetu za Taifa. Nami nikataka

kuongeza kidogo mawazo yangu hapo kwamba wakati *COVID* inaingia duniani, tuliwashauri watalii tukasema *don't cancel your trip to Tanzania, postpone.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba wako watu walikuwa wamelipa, fedha zao zilikuwa tayari kwenye *account* za wateja; na kwa kuwa wali-*postpone* wanatarajia siku watakapokuja watahudumiwa kwa gharama ile ile waliyolipia mwaka 2020. Sasa haya mabadiliko yaliyofanywa, nataka kuwaambia Wizara ya Maliasili na Utalii wafahamu kwamba mteja aliyelipia mwaka 2019 aka-*postpone* safari akitarajia kuja Tanzania kukamilisha safari yake anatarajia kuhudumiwa kwa gharama ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukumbusha hapa pia kwamba liko tatizo kubwa kwamba tunataka kufikia watalii milioni tano, jambo jema kabisa, lakini watalii hawa wanalipia muda na ukarimu. Ukarimu wanaolipia ni pamoja na *consistency* ya makubaliano mnayokubaliana tangu siku hiyo unam-*convince* kuja Tanzania mpaka siku anapopata huduma na kuondoka. Mabadiliko yoyote katikati baada ya kulipia yanafanya watalii wengi zaidi wasije kuliko waliokuja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka kuongeza jambo lingine moja. Sasa hivi *requirement* ya *airline* ni kwamba tunatakiwa tufanye *COVID Test*. Hii inafanyika nchi nzima lakini *laboratory* iko Dar es Salaam. Mtalii anahitaji siku tatu mpaka nne kwenda kufanya *COVID Test* Arusha kusubiri majibu na baadaye kupanda ndege kurudi kwao. Matumizi haya ya muda kwa watalii hayasaidii Tanzania kuongeza idadi ya watalii. Tufanye mabadiliko, tupeleke watumishi kule, tuchukue *test* tuwapelekee wataalam waweze ku-*test*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, liko tatizo hapa linazungumzwa kuhusu tatizo la *TRA*. Nawapongeza sana kwa kukusanya fedha nyingi, lakini iko shida. Nimemsikiliza mtu mmoja wa *TRA* kwenye *TV* akiwa anahojiwa *TBC*, anasema

sawa biashara zinafungwa, lakini zinafunguliwa nyingi zaidi. Tumesema kwa miaka mitano, kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hii kitu *inaitwa Task Force*. Tulifanya Mkutano na Mheshimiwa Kalemani pale Geita, tukaita wafanyabiashara wa Mkoa mzima wa Geita. Wanalalamikia *TRA* makadirio yao siyo rafiki. Kwa nini siyo rafiki? Inawezekana ni kwa sababu ya *target* kwamba ni kubwa kuliko *survey* ilivyofanyika ya uwezo wa walipa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna tatizo na *Regional Manager* wa *TRA*, wasaidizi wake huku chini, wanaweza kukukadiria shilingi milioni 400, mwisho mkaishia shilingi milioni 30. Maana yake ni nini? Kuna room hapa katikati ya *negotiation* na Serikali inapoteza fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Task Force* inafanya jambo moja. Wanakuja wanafanya *special audit*, wakishafanya wanakwambia unatakiwa kulipa shilingi bilioni tano. Wakati huyu mteja ana-*appeal* wanazuia *account*, wanachukua fedha zote kwenye *account*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikuta kuna fedha kwenye *account* ya mfanyabiashara leo, kwa mfano, biashara ya utalii; fedha siyo zake, ni za wateja wanaosubiri huduma. Unapozuia maana yake unamzuia asitoe huduma kwa huyo mtalii, unazuia asilipe mishahara, unazuia asiendelee kufanya kazi. Ushauri wangu kwenye jambo hili, unapofanya *special audit*, ukagundua huyu mtu anatakiwa kulipa shilingi bilioni tano, akakata rufaa, wewe kabla hujatoa majibu ya rufaa ya aliyekata rufaa, umeshazuia *account*, umemnyang'anya *passport*, umepeleka maaskari pale kuzuia biashara. Kodi haitafutwi hivyo. Huwezi kutafuta kodi wakati *compliance tax payers* duniani wanabembelezwa. Dunia nzima ukiwa na *compliance tax payer* unawapa *stimuli* wakati wa shida ili waweze ku-*survive* walipe kodi. Sisi tunachokifanya tunatumia nguvu nyingi ku-*meet target*, matokeo yake tunawafanya watu wengi wana-*exit business*, tunafikiri wanaongezeka, lakini watu wanapungua. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri kwamba lazima tutafute namna bora ya kukusanya kodi, namna bora ya kuwalea wafanyabiashara tuliona. Leo na hapa getini wapo, wafanyabiashara walikuwa wanaingiza vitenge; analipa shilingi milioni 125, karudi ghafla anakuta *container* shilingi milioni 350, ameacha kulipa. Kesho yake atakachokifanya, akilipa anafunga duka, anatafuta machinga, anagawia watu barabarani. Akishindwa anahamia nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kuisaidia Serikali kukusanya kodi, lazima Wizara ya Fedha watusikilize, tunazungumza na wananchi. Inawezekana hawana taarifa sahihi. Biashara zinakufa na watu wana...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga, lakini acha nikuruhusu. Unasemaje Mheshimiwa?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuongeze Mheshimiwa Kanyasu kuhusu wafanyabiashara wa Kariakoo. Kwa kweli hilo ni tatizo kubwa kwa sababu sasa hivi ma-*container* mengi sana ya vitenge yako bandarini inapata labda miezi minne au mitano wameshindwa kulipa kodi kutokana na hilo ongezeko kubwa sana la kodi. Kodi imefikia mpaka milioni 400 kwa *container* moja wakati siku za nyuma walikuwa wakilipa milioni 165 au 160. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanaweka zuio, wafanyabiashara tayari walikuwa wameshaweka *order* viwandani kule China. Mzigo unafika bandarini tayari kuna ongezeko la karibia shilingi milioni 200 na kidogo. Kwa hiyo, sasa mizigo hiyo iko bandarini mpaka sasa hivi hawajui

wafanye nini. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali iangalie jinsi ya kuwapunguzia kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikubali kabisa Taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hilo jambo limeshafika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, tuwe na subira. Hao wafanyabiashara wameshapita ngazi nyingi wamefika sehemu wameshawaona viongozi, naamini watachukua hatua hata Naibu Waziri hapa alishaonana nao. Kwa hiyo, tujipe muda kidogo Serikali iweze kulifanyia kazi jambo hili maana isije ikaonekana miezi yote hiyo sasa hawajashughulikiwa kabisa ama hawajaona mtu yeyote lakini sasa wamepata fursa hiyo naamini Serikali itafanya kwa sehemu yake.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni atafuatia na Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka ajiandae.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu, wapiga kura wangu wa Jimbo la Mufindi Kusini na chama changu kwa heshima ya kunifikisha hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa ufupi mambo machache juu ya Mpango ambao umewasilishwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri. Eneo la kwanza napenda kupongeza Mpango uliopita kwani tumefanya vizuri sana kwenye eneo la diplomasia. Tumefanya vizuri sana kwa maana tumeona matokeo makubwa kama vile unaona sasa uanzishwaji wa zile Kampuni ya Twiga ambapo Serikali ina asilimia 16, bomba la mafuta la kutoka Hoima – Tanga, haya ni matokeo ya sera nzuri sana ya diplomasia ya uchumi na usimamizi makini wa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha Mpango atusaidie. Tunafanya kazi nzuri sana ya kuhamasisha watu wa nje kuja kuwekeza nchini, ni upi mkakati sasa wa sisi Watanzania kuhamasisha wafanyabiashara wetu, kuwapa mikopo na ruzuku waende wakawekeze kwenye nchi zingine? Tungetamani kuona magazeti yetu, vyombo vya habari vyetu na kampuni zetu, kama *Clouds* na wengine wanakwenda kwenye nchi zingine za nje ili kuweza kuongeza uwekezaji na mapato kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili napenda kuchangia kwa ufupi sana kwenye eneo la kilimo. Tunafahamu asilimia 7 ya ardhi ya China wanaitumia kwenye kuzalisha asilimia 22 ya mazao duniani. Sisi kwetu sekta hii inatusaidia kwa asilimia karibia 63 na mimi nijikite kwenye mazao makuu mawili ya chai na parachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba katika mazao ya kimkakati ambayo yametajwa ni vyema tukaweka na sheria kabisa ili kuyatambua na kuyawekea ruzuku maalum. Kwa mfano, kwenye zao la chai ambapo moja kati ya wilaya zinalima ni pamoja na kwetu kule Mufindi Kusini. Ukitazama kwenye zao la chai sisi hapa kama Tanzania tumezalisha karibia tani 37,000 lakini tunazouza nje ya nchi ni kidogo sana. Wenzetu Wakenya wanazalisha karibia tani 432,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza najiuliza, pamoja na diplomasia yetu nzuri katika masoko ya dunia, ni kwa nini chai yetu inapelekwa kwa kiasi kidogo nje ya nchi? Changamoto ni nini?

Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atusaidie pia Mpango wa kuweza kusaidia zao kama la chai ili ikiwezekana zitolewe pembejeo kwa wakulima, wahamasishwe watu wa kuweka viwanda vya kutosha katika eneo hili lakini zaidi ya yote mkakati wa namna ya kutoa huduma za ugani kwa sababu ndizo zinazongeza gharama kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni eneo la parachichi. Naomba zao hili liingizwe katika mazao ambayo tunayaita ni ya kimkakati kwenye nchi yetu. Kwa Mikoa kama Mbeya, Njombe mpaka Iringa ni zao ambalo tunaliita *green gold* yaani dhahabu ya kijani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa tunapeleka nje ya nchi tani 8,500. Wenzetu Wakenya peke yao walipeleka tani 68,000 ikawaingizia pesa za kigeni dola milioni 128 lakini ukiichimbua zaidi sehemu kubwa zimetoka nchini kwetu. Ni upi mkakati wa Wizara, kwa sababu hapa haiwezekani maparachichi yanatoka kwenye maeneo yetu yanapelekwa Kenya halafu yanakwenda nje ya nchi inaonekana Kenya ndiyo inazalisha kwa kiasi kikubwa zaidi, shida ni nini?. Napenda kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri anisaidie kwenye eneo hili pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama China asilimia 40 ya soko la China, Kenya ndiyo wanapeleka lakini sisi tunafahamu kihistoria, Tanzania mahusiano yake na China ni makubwa kuanzia uhuru. Tunakosea wapi? Kwa nini watuzidi kete? Ukifuatilia nchini kwetu miradi ya ujenzi wa barabara na ya maji, kampuni za China zimejaa hapa. Kwa nini diplomasia yetu ya uchumi isitusaidie kupeleka mazao kama haya kwao, urafiki wetu una faida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwenye viwanda. Kwanza napenda kuomba maeneo ambayo ni nyeti kwenye viwanda kama Mufindi Kusini yatangazwe kama ni ukanda maalum wa viwanda ili pengine msukumo wa kipekee uweze kuwekwa. Nimefurahi *commitment* ya Serikali asubuhi ya leo na kwa kweli nimpungeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi alipotamka kwamba katika bajeti itakayokwenda kuanza sasa tutakwenda kujenga barabara ya Mtwango – Nyololo kilometa 40, Mafinga – Mgololo kilometa 75.6. Barabara hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kengele tayari.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Mohamed Monni, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka na Mheshimiwa Cecil Mwambe ajandae.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya upendeleo kabisa maana nimeomba muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba niseme maneno yafuatayo. Nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye muda wote amenipa uhai na afya ya kuwa hapa. Pili, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Chemba kwa kunipa kura nyingi za kutosha. Tatu, kwa sababu ya muda nakishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunipa uteuzi na hatimaye kuwa Mbunge na leo niko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie kidogo kwenye elimu. Naishukuru Serikali sana kwa sababu ya elimu bure. Hata hivyo, zipo changamoto ambazo zimesababishwa na elimu bure na moja kubwa ni miundombinu. Tumekuwa na idadi kubwa sana ya wanafunzi wanaoingia kila mwaka. Changamoto ambayo tunapata hasa zile Halmashauri ambazo hazina uwezo kuna matamko yanakuja kwamba lazima muwe na madarasa, madawati lakini Halmashauri zenyewe hazina uwezo wa kujenga madarasa lakini pia hazina uwezo wa kununua madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nittoa mfano mmoja wa athari ambazo zinatokana na haya matamko. Miaka mitatu au minne iliyopita Halmashauri ya Chemba lililazimika kutumia fedha zote za *own sources* kuhakikisha inanunua madawati lakini mpaka leo tunadaiwa kila mahali. *CRDB* wanatudai,

watu walio-*supply* vyuma wanatudai toka mwaka 2016 mpaka leo. Sasa mimi nafikiria lazima kuwa na mpango maalum wa kuhakikisha tunakuwa na mfuko ambao au kuwa na mkakati wa kuhakikisha Serikali inachangia kwenye zile Halmashauri ambazo hazina uwezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo sio rahisi sana lina madhara makubwa sana kwa Halmashauri hizi mpya. Ziko Halmashauri zina uwezo zinakusanya shilingi bilioni 9 mpaka 12 kwa mwaka hata ukiwaambia wajenge hospitali wanaweza! Sasa tumekuwa na changamoto kubwa sana hiyo. Naomba sana Serikali iangalie namna bora kwenye hizi Halmashauri ambazo hazina uwezo wasitamke tu, tutafukuza Wakurugenzi, ma-*DC* lakini ukweli ni kwamba fedha hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano wa hali iliyotokea na sasa hivi ni hivyo hivyo. Sasa hivi tumeambiwa tujenge madarasa, tununue madawati, Halmashauri yangu zaidi ya asilimia 40 watoto wanakaa chini. Tungependa kila mtoto akae kwenye dawati lakini mimi Mbunge nina uwezo wa kununua madawati ya shule zote za Halmashauri? Haiwezekani! Tumeaambiwa tununue madawati, fedha hakuna na ni kweli fedha hakuna, nini cha kufanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopanga hii mipango lazima i-*reflect* hali halisi iliyopo huko. Tusipofanya hivyo mipango yetu itakuwa tunaongea tu. Bahati nzuri niseme ukweli kwamba nimesikia michango mizuri sana ya Wabunge, nilikuwa nafikiria tofauti na hali sasa sijui kama Mawaziri wanachukua hiyo mipango inayoelezwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba niongee kuhusu kilimo. Mimi ni mkulima mzuri kabisa. Hata tunayoyaongea kwamba tumetumia shilingi bilioni 180 kwenye kilimo mimi ambaye ni mkulima mkubwa pale Chemba sijawahi kuona kitu hicho. Pia huo mkakati wetu wa kilimo ukoje? Mimi mwenyewe nikilima hata kutafuta soko mpaka niende Nairobi, sijawahi kuona Afisa Kilimo wala mtu yeyote anayenifuta kuniuliza sasa ndugu yangu umelima

tufanye ABC, changamoto kubwa ni masoko ya mazao haya.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni kubwa mno. Tunaongelea kulima, tunaongelea kilimo cha umwagiliaji, Jimbo tu maji ya kunywa hawana, sasa huu umwagiliaji utakuwaje? Hatuna uwezo wa kujenga mabwawa ili tupate maji ya kunywa halafu tunafikiria tujenge kwanza mabwawa kwa ajili ya kilimo. Hii inanipa changamoto kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali na wakati mwingine najiuliza hivi nani ana wajibu wa kutafuta soko la mazao tunayolima? Tunasema asilimia 75 ni wakulima, mimi nalima lakini watu wengi walioko vijijini, leo utasikia gunia la ufuta Sh.90,000 lakini kesho Sh.40,000.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Mariamu Madalu Nyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

**MHE. MARIAMU M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwani ni mara yangu ya kwanza leo kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuiona siku hii ya leo. Pili, naomba niwashukuru wazazi wangu, familia yangu, watu wangu wa karibu, Chama changu cha Mapinduzi na wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa kunipa moyo na kuniadini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Awamu ya Tatu wa miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Katika Mpango huu, mambo muhimu yamezingatiwa kama

kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara; kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2016/2017 na 2020/2021, tumeona jitihada kubwa za Serikali za kuwashirikisha wanawake katika nyanja mbalimbali ili kuleta usawa na kuondoa ukatili wa kijinsia, kuongeza fursa za kiuchumi, kuwajengea uwezo wa kufanya biashara, upatikanaji wa mitaji, upatikanaji wa masoko na upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati sasa wanawake wa mikoa yote wapate fursa sawasawa wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ili na wao waweze kujikimu kimaisha pamoja na familia zao kwa kuwapatia mikopo hiyo yenye riba nafuu na fursa nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapendekezo ya Mpango wa Tatu, naomba kushauri mambo matatu yafuatayo. Moja, ianzishwe kanzi data itakayokuwa na vikundi vya wanawake nchini kimkoa ikionesha madaraja ya vikundi, mahitaji yao na namna ya kuyafikia mahitaji hayo kwa mfano mikopo yenye riba nafuu. Mbili, itolewe taarifa ya Benki ya Wanawake iliyohamishiwa Benki ya Posta, ni namna gani fursa za mikopo kwa akina mama zinatolewa kwa madaraja tofauti na fursa hizo zinapatikanaje kupitia benki hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nitamke kama ifuatavyo. Wanawake hawa ili waweze kuchangia uchumi wanatakiwa wajengewe uwezo wa kujiamini kwa kuendeleza juhudi zao za kujitegemea na hatimaye waweze kuchangia Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*



**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa namna ya pekee kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai kurudi hapa tena leo kwenye Bunge la Kumi na Mbili. Nikishukuru chama changu cha Mapinduzi, Chama ninachokitumikia sasa hivi ambacho ndicho chenye Ilani na walinikabidhi Ilani wakati wa uchaguzi mkuu na nilishinda kwa kishindo Jimbo la Ndanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana pia ushirikiano ninaoupata kutoka kwa Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi. Nimesimama hapa nikiwa na furaha kwa sababu kati ya mambo ambayo nilikuwa nayatamani siku zote ni kusimama na kuitetea Ilani ya Chama cha Mapinduzi na mipango mizuri ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri sana ndugu zangu wa upande wa pili, Waheshimiwa Mawaziri pia ikiwezekana tuwagawie wale ndugu zetu Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuna mambo mengine wanayabishia kwa sababu hawajayaona, hawajasoma na hawayafahamu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ya msingi ambayo napenda kuyachangia leo kwenye Mpango huu. Suala la kwanza kabisa ni kuhusu reli ya Kusini. Tunataka hapa Waziri wetu aje kutueleza nini mpango madhubuti wa Serikali kuhusu reli ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumesikia wengi wanaongea, suala la Liganga na Mchuchuma, kama ambavyo nimesema toka mwanzo kwamba liko hata kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tunaomba sasa likafanyiwe kazi na litekelezwe kwa ajili ya kuongeza uchumi wa watu wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la barabara. Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi – Nachingwea – Liwale na kipande cha barabara ambacho huwa hakitajwi kinaenda kuunganisha Malinyi ili kuwafanya watu wa Mikoa ya Kusini kwa maana ya Mtwara, Lindi na Ruvuma kufika kirahisi Makao Makuu ya nchi badala ya kupita njia ndefu ya Dar es Salaam. Kuna barabara pia ya Nanganga - Nachingwea – Ruwangwa mpaka Liwale pia na yenyewe tunaomba ifanyiwe kazi na tupate hapa majibu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wastaafu, limeongelewa hapa ndani na Wabunge wengi sana, wa ngazi mbalimbali wakiwemo wanajeshi, walimu kuhusu stahiki zao na haki zao za msingi na kumekuwa na ucheleweshwaji mkubwa sana wa malipo yao wakati huu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali kwa kina kabisa ije itueleze mikakati yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nataka nijikite hasa kwenye suala la kilimo. Sisi kule kwetu ni wakulima wa korosho na ni zao la kimkakati la Kitaifa katika yale mazao matano makubwa. Niombe sana Serikali izingatie sasa kuona tunawasaidia hao wakulima wa korosho ili waweze kusaidia kuongeza uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa ambayo huwa yanajitokeza kila mara wakati wa kilimo. Msimu uliopita wa korosho tumeona wakulima wanahangaika sana kupata magunia. Katika karne ya leo kunakuwa na shida ya vifungashio vya korosho yetu tunayotaka kuiuza. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iweke msisitizo na Waziri wa Kilimo aje kutueleza hapa mikakati yao ya kuhakikisha magunia na pembejeo kwa maana ya *sulphur* inapatikana kwa wakati kwa ajili ya wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka mwaka juzi katika mjadala hapa iliondolewa ile pesa kwa ajili ya tozo ambayo ilikuwa inakwenda kusaidia kufanya utafiti pamoja na kuongeza mambo mengine kwa wakulima. Tuiombe sasa

Serikali kutafakari upya kama ambavyo imefanya kwenye kurejesha ile pesa ambayo ilikuwa inakusanywa na *TRA* kwa ajili ya mabango imekwenda tena kusaidia halmashauri. Kama inawezekana basi, waone namna ya kuwasaidia wakulima, hii pesa ingeweza kurudi kwenda kulipa yale madeni ya zamani ambayo wanadai watu wengi waliotoa huduma kwenye zao hili la korosho na sekta nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia hapa Mbunge mmoja anasema zao la korosho limeshuka kidogo uzalishaji wake, ni kwa sababu ya kukosa utafiti, kukosa dawa kwa wakati na uwezo mdogo wa wasimamiaji. Mazao haya ya kimkakati yanasimamiwa na vyama vya ushirika. Sisi kimsingi tulichoka, pamoja na nia njema ya Serikali kutaka kuboresha, lakini tuone sasa unapatikana mfumo thabiti kabisa utakaokwenda kupata viongozi bora, waadilifu na waaminifu kwenye vyama vyetu vya msingi na kwenye vyama vikuu ili kuweza kuwasaidia wakulima. Tumeona sasa hivi chaguzi mbalimbali zinafanyika ndani ya vyama hivi, lakini kimsingi watu wa *COASCO* hawajafanya kwa uhakika kabisa mahesabu kwa sababu, wanapobadilishana uongozi kwenye vyama hivi kumekuwa na utaratibu wa kurithishana madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madeni makubwa sana ya wakulima sisi tumeyakuta. Tumetoka kwenye Bunge lililopita tumeingia kwenye Bunge hili bado madeni hayo yapo. Kwa hiyo, niombe Serikali au Waziri wa Kilimo awaagize watu wa *COASCO* kabla viongozi hawa hawajamaliza kukabidhiana madaraka yao pale, basi kimsingi wahakikishe kabisa wanafanya ukaguzi, ili kuweza kukabidhiana ripoti zilizo safi, lakini tufahamu watu wa kuweza kuwawajibisha pale panapotokea upungufu katika maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema kwamba, kwenye zao la korosho kuna mambo mengi sana, kwa hiyo, tunahitaji kabisa kimsingi, sisi kama wakulima tunaotokea eneo la wakulima wa korosho, tukutane na Mheshimiwa Waziri katika sekta hii ili tuweze kumshauri vizuri kwa sababu, mambo mengi tunayafahamu kule nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa mara ya kwanza toka niingie kwenye Bunge hili, kwa sababu huko nyuma nilikuwa siwezi kuunga mkono kwa sababu tulikuwa tuna ilani ambayo tunaitekeleza. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mheshimiwa Amandus Julius Chingulle ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia mapendekezo ya huu Mpango. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na timu yake. Kwa kweli, wamekuja na mpango ambao ni wa kibunifu sana hasa kwa dunia ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia dhima nzima ya huu mpango ambao ni ushindani kwa kweli, unabeba kitu kikubwa zaidi ambacho duniani kote sasa hivi ushindani sio wa bidhaa peke yake, lakini mataifa yanashindana kuangalia *resources* zao walizonazo ni namna gani wazitumie vizuri na sisi kwa Tanzania Mwenyezi Mungu ametujalia *resources* nyingi sana ambazo kwa kweli ni za kishindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwa uchache tu kwa ajili ya muda, ukianza uzalishaji wa madini yetu. Kwanza nashukuru Serikali kwa kutunga Sheria ya Madini, lakini yale madini tutayatumia namna gani ili yatuletee kipato na kuongeza pesa za kigeni? Nina imani Waziri wa Fedha anahitaji *FDIs* nyingi. *FDIs* atazipata kutokana na mazao yetu ya madini. Kwetu Mbeya, Wilaya ya Mbeya ambayo na Mheshimiwa Mwenyekiti na wewe ndio unakotokea wilaya hiyo, sisi hatujaanza kuzalisha, lakini tuna madini yanaitwa *niobium*. Inawezekana likawa ni jina geni sana kwa Wabunge, lakini madini ya *niobium* ni madini adimu sana na huo mgodi ambao unaanzishwa utakuwa wa kwanza Afrika na wa nne duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoiomba Serikali ni namna gani kufuatia mpango huu iweke hii mipango

kwenye mpango wa muda mfupi, lakini iweke vilevile kwenye mpango wa miaka mitano kwa sababu, haya madini yanategemewa yanaweza kuvunwa kwa miaka zaidi ya 30 mpaka 50. Sasa hayo madini yanatumika kwenye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo madini kwa kiasi kikubwa yanatumika kwenye kuimarisha vyuma, kwa hiyo, yataendana pamoja na madini ambayo tunayazalisha ya chuma cha Liganga. Hawa wawekezaji wanataka waanzishe hiki kiwanda cha kwanza Afrika, kwa hiyo, watachimba na kuchenjua, ili bidhaa hii ambayo inaitwa *niobium* ambayo ni ya kwanza kwa Afrika iweze kuzalishwa hapa kwetu na rasilimali kutoka mataifa mengine yaje hapa kwetu yaletе hiyo rasilimali na sisi tuwe wazalishaji wakubwa. Haya ndio madini yanayotakiwa kwa leo ili tuweze kujenga madaraja ya baharini, madaraja ya ziwani, reli *SGR* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukiangalia wataleta nini; hawa wanaleta *FDI* ya karibu zaidi ya bilioni 250 ambazo kila mwaka zitazalisha zaidi ya dola milioni 220, ukiangalia hiyo ni asilimia kubwa sana. Sasa ningepomba katika mikakati ya namna hii Wizara ziwe zinashirikiana isiwe kitu cha Wizara moja. Hizi ni *opportunities*, hizi ni fursa na haya madini kadri miaka inavyokwenda na teknolojia inavyobadilika si ajabu yakawa mawe ya kawaida tunayoyaona kama tunavyoyaona haya ya hapa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala zima la kilimo cha pareto. Nalo ni zao ambalo inawezekana watu wengi wakashangaa, lakini pareto tunayolima Tanzania kwenye Wilaya ya Mbeya ni ya kwanza Afrika na ya pili duniani. Inatumika kutengeneza dawa za kuuu wadudu, lakini zaidi zaidi inatumika sasa hivi kwenye kutengeneza dawa za kuhifadhi nafaka na hii ni *organic*. Sasa viwanda vya namna hii inatakiwa viwekwe kwenye kipaumbele, ndio tunavyovihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Kilimo iangalie kwa kipekee namna gani tuweze kuvutia viwanda

vitakavyozalisha dawa zinazotokana na pareto. Kwa vile hatuna mshindani, wenzetu jirani zetu wanakuja kuchukua kwetu *raw materials* kutoka Tanzania, wanatengeneza hiyo *raw materials*, wanasafirisha kwenda nje. Sasa hivi Uganda na Kenya pamoja na Rwanda ndio wamekuwa wateja wazuri sana kwa wakulima wangu kule Mbeya kwenye mazao haya ambayo sisi yanakuwa ni *semi processed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara iangalie namna gani tuchukue majukumu ambayo yataisaidia nchi yetu kupunguza pengo la pesa za kigeni. Pesa za kigeni zikipungua hatari yake ni nini? Hata ile kuingia kwenye uchumi wa chini wa kati ni rahisi tukaporomoka mara moja. Sasa hivi tuna dola 1,080 ambayo iko chini kabisa. *Exchange rate* kama sio tulivu ina maana tunaweza kuporomoka tukarudi tulikotoka. Sasa tuki-*take advantage* hii kwa fursa tulizonazo...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, kengele imegonga.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa ajiandae.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa naomba nimpongeze Waziri wa Fedha kwa uwasilishaji uliotukuka wa rasimu ya mpango. Mimi binafsi kama Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti pamoja na wenzangu tulipokea mapendekezo yale na tuliyafanyia uchambuzi wa kina. Nashukuru na pia, naipongeza Serikali kwa kuchukua mawazo yet una kuyajumuisha katika rasimu ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wowote ule unahitaji rasilimali fedha na Waheshimiwa Wabunge hapa wameongea mambo mengi sana ya kimkakati, jinsi gani tutapata fedha kwa ajili ya kuwezesha Mpango wetu utekelezeke kwa kiwango cha juu. Naomba nijikite kwenye suala la udhibiti wa mapato. Mambo yote haya yaliyoongelewa na Wabunge mambo mazuri yatakuwa hayana maana sana kama tutashindwa kudhibiti mapato yetu tutakayoyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la *GePG*, yaani *Government Electronic Payment Gateway*. *GePG* ni mfumo wa Serikali wa kukusanya mapato kielektroniki. Naweza kusema kwamba, Serikali imeshindwa kudhibiti mapato yetu kupitia mfumo huu kwa kiasi kikubwa. Ni kweli, mfumo huu umeisaidia Serikali kuongeza mapato yake, lakini vilevile inabidi tuufanyie kazi zaidi kuhakikisha tunadhhibiti mapato yetu mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu tumewaamini na tumewaachia sekta binafsi watusaidie kukusanya mapato haya, hususan sekta ya simu, makampuni ya simu na mabenki mbalimbali, lakini inavyoonekana makampuni haya binafsi yamewekeza sana kwenye rasilimali watu pamoja na teknolojia ukilinganisha na wafanyakazi wa Serikali wanaohusika moja kwa moja na mifumo hii. Kwa hiyo, kuna mwanya mkubwa sana hapo wa kupoteza mapato kwa sababu ya tofauti ya kiufahamu wa mifumo hii. Naishauri Serikali iweze kuwekeza kwa rasilimali watu na teknolojia kwenye mifumo hii ili basi tuweze kuitumia mifumo hii kwa ufasaha na ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala la mawasiliano. Naweza kusema kwamba, sekta hii ya mawasiliano ni moja ya sekta ambazo zinachangia kodi kubwa na uchumi wa nchi hii, lakini Serikali yetu sijaona jitihada zake za dhati kuisaidia sekta hii ili iweze kukua zaidi na Serikali iweze kukusanya mapato zaidi kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kodi kubwa, tozo mbalimbali na masharti mengi yanayowekewa sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutolea mfano tu, kuna maeneo mengi ya vijijini, kwa mfano kule Longido kuna Kata ya Nondoto Matale, hata Wilaya ya Meru kuna Kata ya Ngabobo, hakuna mawasiliano ya simu, lakini sekta hii mdhibiti, ndio kazi yake kubwa kuhakikisha kwamba, sehemu mbalimbali zinapata mawasiliano, hususan sehemu za vijijini. Kampuni hizi za simu zinakatwa tozo ya asilimia tatu katika mapato yake inaenda kwenye mfuko unaitwa *USCAF (Universal Fund)* na lengo kubwa la Mfuko huu ni kuendeleza mawasiliano sehemu za vijijini na mijini. Sasa napenda kujua kwamba, Mfuko huu unafanya kazi gani hasa kama kuna sehemu nyingi tu za nchi hii ambazo hazina mawasiliano ya kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Mpango wa Serikali. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia na mimi kuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi ya kuwa mgombea na hatimaye kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Nachingwea kwa kura nyingi za kishindo.

Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mwenyekiti wetu wa chama kwa kazi kubwa aliyoifanya akisaidia na Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wamezunguka nchi nzima kunadi llani ya CCM wakishirikiana na viongozi wetu waandamizi wa chama na hatimaye Wabunge wengi tukarudi ndani ya Bunge, wengine kwa mara ya kwanza kwa kishindo kikubwa. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana. Wengi tumeingia ni kwa matumizi hayo, kwa harakati hizo za viongozi wetu wakuu, lakini zaidi ya hayo kutokana na kazi nzuri iliyofanywa ya kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na *comrade* wetu, jemdari wetu, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Pamoja na kazi hiyo nzuri, pamoja na pongezi hizo ambazo nimempatia Mheshimiwa Rais, sasa nijielekeze kuchangia kwenye Mpango huu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye halmashauri nyingi ikiwemo ile ambako mimi natokea, uchumi wetu ni kilimo. Pamoja na Serikali imeelekeza hapa maelekezo yake kwamba, itawekeza zaidi na kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, bado nishauri kuna migogoro mingi ambayo iko kwenye maeneo mengi na hasa wafugaji na wakulima. Nikitolea mfano kwa Jimbo langu la Nachingwea kuna mwingiliano mkubwa baina ya wafugaji na wakulima. Niishauri Serikali tutenge maeneo maalum yatakayowawezesha wafugaji kwenda kukaa kwenye eneo ambalo sasa litakuwa na miundombinu yote kwa maana ya maji na malisho badala ya kufanya ufugaji wa sasa wa kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunapokuwa tunazungumzia kilimo ni eneo mtambuka, wakulima wetu wengi wanalima kilimo cha kizamani sana, wanatumia jembe la mkono. Kwa kweli katika hili niombe sana Serikali iwekeze vya kutosha ili wakulima wetu waondokane na kilimo kile cha kizamani, waende sasa kuingia kwenye kilimo cha kisasa. Katika eneo hilo basi tuongeze kwenye rasilimali watu kwa maana ya wale wataalamu wetu wa kilimo waende zaidi kwenye vijiji vyetu, wakatoe elimu zaidi na kuwasaidia wakulima wetu ili waweze kulima kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania yetu ni Tajiri, tuna madini, lakini tuna maliasili ya kila namna, Mwenyezi Mungu ametujalia sana. Katika hili yako maeneo ambayo bado hatujayafanyia kazi kwa upande wa madini. Nikitolea mfano kule kwetu eneo la Nditi, Kiegeyi, bado tumeomba vibali,

tumeomba leseni ya uchimbaji kwenye maeneo yale, lakini bado Wizara haijaitilia mkazo . Nashukuru Mungu nilizungumza na Mheshimiwa Waziri wa Madini akaniahidi atatembelea kule Nachingwea...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MMWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Agness Mathew Marwa.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia rasimu ya Mpango. Wizara hii imeweka mambo mengi sana ambayo ni mazuri na naamini kabisa ni mwendelezo wa mafanikio ya miaka mitano iliyopita ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye rasimu hii nimeona wakizungumzia viwanja vya ndege, kikiwemo kiwanja cha Mkoa wa Mara. Kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Mara ningeishauri Serikali katika Mpango wake kipewe kipaumbele na ikiwezekana wakiangalie kwa macho ya ziada kwa sababu, kule kwetu Mkoa wa Mara ndipo alipotoka muasisi wa Taifa hili, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa hiyo, ni sehemu nzuri ambayo ingelikuwa ni ya mfano na hasa ukizingatia Mkoa wa Mara tunachangia Taifa hili pato kubwa sana kutokana na madini, lakini pia utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara tuna kiwanda ambacho kiko Musoma Mjini, Kiwanda cha *MUTEX*. Kiwanda cha *MUTEX* kimekufa muda mrefu sana. Kiwanda hiki kilikuwa kinatengeneza kanga nzuri sana na kubwa ambazo ukiangalia watu wa kule Mkoa wa Mara tumejaliwa zile kanga zilikuwa zinatutosha vizuri tu. Kwa hiyo, niseme na

sasa hivi pia ni vizuri zaidi kile kiwanda kikiangaliwa kwa jicho la ziada ili kifunguliwe kwa manufaa ya kuongeza ajira kwa vijana na watu mbalimbali ambao wanaweza kupata ajira na kupunguza upungufu wa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wazee wetu wa muda mrefu sana ambao wanaitwa wastaafu walifanya kazi kipindi hicho kiwanda kile kikiwa Serikalini. Wana madai yao ya muda mrefu sana ni miaka sasa, kila wanapoenda mahakamani wanakata rufaa, wanashinda, wanakata rufaa wanashinda, nimwombe sana baba yangu, Mheshimiwa mpendwa wetu sana Rais, naamini kabisa ataiangalia siku ya leo; akawaangalie wale wazee wetu wa Kiwanda cha *MUTEX* kwa jicho la huruma, walipwe mafao yao ya muda mrefu kwa sababu, kuna wengine wao wameshafariki, kuna wengine wamepata ulemavu, lakini hata wale waliopo hali zao sio nzuri sana. Naamini anajali wanyonge na wale ni kati ya wanyonge ambao naamini kabisa *daddy* atanisikiliza leo na ataenda kuwaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la maji; Mkoa wa Mara wilaya zetu zote zimezungukwa na Ziwa Victoria, lakini baadhi ya wananchi wetu wanalia sana shida ya maji kutokana na miradi mikubwa ambayo Serikali imeshaiandaa kwa ajili ya Mkoa wa Mara. Pia, kwenye rasimu nimesikia wakiitaja, kwa kweli nawapongeza sana wako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Mkoa wa Mara ni mkoa aliotoka muasisi ulitakiwa uwe mkoa wa mfano, asiwepo mwananchi hata mmoja analalamika shida ya maji. Hivyo basi, ningepomba miradi hiyo mikubwa inapopita; upite Bunda, upite Serengeti, upite Tarime, upite Rorya, upite Musoma Vijijini, upite Musoma Mjini, lakini upite maeneo yote lengo ni kwamba, kutoa haki sawa na hasa kwa wale ambao wamekaa karibu na uaridi. Wanasema unapokuwa karibu na uaridi unanukia. Sisi wenyewe Mkoa wa Mara ndio wenye uaridi ambalo ndio maji ya ziwa, pamoja na kuwa Taifa zima ni haki yetu na ni haki yao, lakini sisi hasa Mkoa wa Mara tuwe wa mfano tusikose maji nyumba hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la miradi mikubwa ya umeme. Huu mradi wa umeme umekuwa kwa wananchi na hasa wananchi wa vijijini umekuwa changamoto sana huu mradi wa umeme wa shilingi elfu 27. Wananchi kila wanapoenda kwenye ofisi zao, wanaambiwa kwamba, bajeti bado haijaandaliwa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana, pamoja na kazi nzuri anazozifanya, nimwombe aangalie hili suala kama ni bajeti sisi Wabunge tutampitishia harakaharaka ili hili suala liende kwa wananchi wakapate huu umeme wa shilingi elfu 27 kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu.

**MWENYEKITI:** Muda wetu umeisha.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Waheshimiwa Wabunge niwataje wachache tutakaoendelea nao mchana: Mheshimiwa Hassan Mtenga, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mheshimiwa Mwamtumu Dau, Mheshimiwa Halima Mdee. Tutaanza nao hao mchana.

Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba kwa sasa Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge nina matangazo mawili; kwanza kuna tangazo la wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, hawa wanatoka TAMWA. Sijui kama wako humu ndani? Siwaoni, pengine hawakupata fursa ya kuingia. *(Makofi)*

Pia kuna tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Spika. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi mnatangaziwa kwamba, mnatakiwa Ukumbi wa Spika, ghorofa ya kwanza, jengo la utawala tukiitoka tu hapa ndani.

Kwa hiyo, saa saba hii ndio kikao kinaanza, kwa hiyo, tuelekee huko Mheshimiwa Spika ameitisha hicho kikao. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukiitoka hapa tuelekee Ukumbi wa Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni, leo.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa  
wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) na  
Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka  
2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa  
Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa  
Mwaka 2021/2022**

**NAIBU SPIKA:** Katibu tena.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango, Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na michango ya Waheshimiwa Wabunge waliokuwa hawajapata nafasi ya kuchangia tulipokuwa tumeanza asubuhi. Tutaanza na Mheshimiwa Hassan Mtenga atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Abdallah na Mheshimiwa Reuben Kwagilwa ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, nianze kutoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambazo anazifanya. Pili nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waziri Mkuu lakini kwa pamoja niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mtwara Mjini ambao wameniwzesha kufika kwenye Bunge hili kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze kwenye maeneo mawili. Kabla sijaanza kuzungumza ni vema nikatoa shukrani kubwa sana, Jimbo la Mtwara Mjini tumepata miradi

mingi sana. Tuna mradi wa Hospitali ya Rufaa ambayo itagharimu zaidi ya shilingi bilioni 122, tuna barabara ya kiwango cha lami ambayo inatoka Mtwara - Masasi na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi nataka tuzungumze kuhusu *Mtwara Corridor*. Hii *Mtwara Corridor* inawezekana hatuielewi vizuri na italeti maendeleo gani. Mheshimiwa Rais amewekeza fedha kwenye bandari ya Mtwara takriban shilingi bilioni 157, lengo na madhumuni ni bandari ya Mtwara iweze kufanya kazi na ilete tija kwenye uchumi wa taifa. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais ameamua kutengeneza barabara ya kutoka Mtwara - Newala ambapo itakuwa ni kiunganisho kikubwa sana kwenye zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu umefanyika juu ya reli ya kutoka Mtwara hadi Mbambabay. Kama upembuzi yakinifu umefanyika na tunapozungumza upembuzi yakinifu ni kwamba tayari mamilioni ya shilingi yametumika kwenye kuangalia dhana nzima ya awali. Niishauri Serikali muda sasa umefika wa kutoa maamuzi ambayo yako sahihi ya kuanza kuijenga reli hii ambayo itaweza kutuletea uchumi kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia uchumi wa nchi, yako mambo matatu tunatakiwa tuyaangalie. Tunazungumzia barabara ambayo ni kiunganisho, viwanda ambacho ndiyo kiunganisho namba moja lakini lazima tuwe na watu kama hatutakuwa na watu hatutakuwa na mashamba na hatutakuwa walimaji. Kama hakuna barabara ambazo ziko sahihi hatutaweza kupitisha mazao yetu kwenye barabara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu niiombe tena Serikali, tuna barabara ya kutoka Mtwara - Dar es Salaam, kwa muda mrefu sasa imekuwa inafanyiwa *service* za mara kwa mara na kutengeneza barabara ya lami kilometa moja inatugharimu fedha nyingi sana. Barabara hii imekuwa inaharibika mara kwa mara kwa sababu malori yanayopita

ni makubwa na yenye uzito mkubwa. Tuna kiwanda cha Dangote, *cement* yote zinasafirishwa kwa njia ya gari. Tuna zao la korosho ambapo zote zinasafirishwa kwa njia ya barabara. Tumejenga bandari na tumewekeza pale shilingi milioni 157 ni kitu gani kinashindikana bandari ya Mtwara isifanye kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la elimu ni vema nikampongeza sana Mheshimiwa Rais. Tunapozungumzia elimu bure kwenye shule za msingi na sekondari suala hili limeleta chachu kubwa kwa wananchi kwa ujumla wake. Hata hivyo, ni vema nikasema kuna mgawanyiko katika fedha ambazo tunazipeleka kwenye shule za sekondari na msingi. Mwanafunzi mmoja shule ya msingi anapelekewa Sh.6,000 na mwanafunzi mmoja kwenye shule ya sekondari anapata Sh.10,000...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, kengele imeshagonga

**MHE. HASSAN S. MTENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dooh, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Reuben Kwagilwa na Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini nikishukuru Chama cha Mapinduzi na wananchi wa Jimbo la Lindi Mjini kuniwezesha kurudi tena katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kutuletea Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa. Pamoja na hayo, amefanya kazi nzuri kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita



katika kuhakikisha kwamba tunakuza uchumi wa taifa letu. Hakuna asiyejua, kila mmoja anajua kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. Mpango huu umeweka kipaumbele katika kukuza uchumi wa bahari pamoja na uvuvi. Mwenyezi Mungu ametujaalia nchi yetu tuna bahari na maziwa. Eneo la bahari tuna kilomita za mraba 64,500 lakini upande wa maziwa tuna kilomita za mraba 62. Katika maeneo haya ndiko kunapatikana samaki na ufugaji wa samaki, kilimo cha mwani, uzalishaji wa madini ya chumvi, gesi na mafuta, utalii wa fukwe za bahari pamoja na michezo mbalimbali ya bahari. Katika uwekezaji huu wa *blue economy*, eneo hili La bahari ni la Muungano, naomba kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba tunazipitia sheria pamoja na miongozo na kanuni ili tuweze kufanya kazi vizuri katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kutekeleza miradi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kuhakikisha kwamba tunakwenda kusimamia uchumi huu wa bahari. Tunahitaji kuwa na wataalamu wenye kujua na wenye uzoefu ili tuweze kukuza uchumi huu wa bahari. Niishauri Serikali kupeleka wataalam wetu nje ya nchi kwenda kusoma ili waweze kupata ujuzi mzuri tuweze kuja kutekeleza haya ambayo tunayakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, tunahitaji pia uendelezaji wa sekta hii ya bahari uende sambamba na uwekezaji wa miundombinu yake. Tunahitaji kujenga bandari kwa ajili ya shughuli za usafirishaji na uvuvi. Hatuwezi kutumia bandari ya Dar es Salaam, leo inashusha mzigo wa *sulphur* halafu kesho inashusha samaki, hapana haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba Serikali yetu inaendelea kujenga bandari zitakazotumika kwa shughuli za uchumi huu wa bahari. Tunaweza kupanua na kujenga bandari kule

Bagamoyo lakini tukajenga bandari kule Mkoani Lindi. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumepanua huduma hii ya bandari na kuendelea na uwekezaji huu wa uchumi wa bahari. Pia tunahitaji meli zinunuliwe ambazo zitakwenda kufanya kazi katika kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tungeweza kujenga chuo ambacho kitakwenda kusimamia masuala mazima ya uchumi wa bahari pamoja na uvuvi. Pale Lindi tuna maeneo mengi ya ardhi na tuko tayari kutoa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki. Kwa hiyo, naishauri Serikali kujipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kusimamia uchumi huu kwa ajili ya kuongeza kipato cha nchi yetu ili tuweze kuwahudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ya bahari tunayo na rasilimali watu tunayo na Watanzania tuna afya nzuri ya kufanya kazi. Ni sisi Serikali sasa kujipanga katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kukuza uchumi huu wa bahari pamoja na uwekezaji kwenye eneo la uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona Waziri anapokuja kutoa taarifa yake ya kazi ya kipindi cha mwaka mmoja na kuonyesha kwamba mapato ya Wizara yake yameongezeka kwa kutoza faini, hii siyo sahihi. Tunategemea Mawaziri wasimamie tuone mapato yanaongezeka kupitia miradi ya kimkakati katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Reuben Kwagilwa atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Mwantumu Dau ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii. Moja kwa moja nijielekeze kwenye kuchangia lakini sababu dakika tano ni

chache sitaingia ndani sana ila nataka nitoe ushauri mmoja kabla sijatoa maelezo yangu ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ambao nataka nitoe, kuna suala hapa limezungumzwa sana nalo ni la maji. Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Maji Na. 5 ya mwaka 2019, Sheria hii ya Maji ya mwaka 2019 ndiyo ilianzisha RUWASA lakini kana kwamba haitoshi ikaenda mbele ikaleta Mfuko wa Maji wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuwa anazunguka kufanya kampeni kwenye hotuba yake amekiri, namnukuu anasema: "*Hata hivyo, napenda nikiri nilipokuwa kwenye kampeni moja ya changamoto kubwa niliyoelezwa na wananchi ilikuwa ni shida ya maji hususan maeneo ya vijijini*". Kwa sababu Mheshimiwa Rais ameshaliona hili, nashauri Serikali iirejeshe hapa ile Sheria ya Maji, Na. 5 iliyotungwa na Bunge letu ya mwaka 2019 ili tuirekebishe kidogo. Marekebisho yake yaweje? Tumeweka pale *source* ya fedha za huu Mfuko; tumesema tutatoza shilingi 50 kwenye *petrol* na shilingi 50 kwenye *diesel*. Nachoomba ili tuweze kuisaidia *RUWASA* lazima sheria ije hapa tuitengeneze iweze ku-*state* ni asilimia ngapi iende kwenye maji katika hiyo shilingi 100 inayotozwa kwenye *petrol and diesel*. Kwa sababu tukiiacha hivi miradi ya mjini inatumia fedha nyingi kuliko miradi iliyopo vijijini. Kwa hiyo, kuna haja ya kufanya hayo marekebisho ya hiyo sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la jumla sana mimi nataka tu niseme kwamba ndugu zangu unapopanga la kwanza unatumia takwimu na pili unatumia *assumptions*. Kwenye hili eneo la takwimu tusipojizatiti vizuri kuboresha namna ya upatikanaji wa takwimu kwenye nchi yetu kila tunapopanga tutakuwa tunajikuta tuko nje ya malengo. Kwa hiyo, ni vema tuboreshe sana eneo hili la takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye huu Mpango ambao ndiyo mpango wa mwisho kuelekea *Vision* yetu ya 2025 kama Taifa kukamilika wakati nimekuwa nikiusoma mara kwa mara na kuurejea sijaona mahali ambapo Mpango huu

umeweka *provision* kwamba baada ya *Vision 2025* kukamilika inayotekelezwa mwishoni kwenye huu Mpango ni kitu gani kitafuata? *Vision* nyingine itakapotengenezwa, sijaona *provision* kwenye Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tunapopanga ni vema tukajua *financing mode* ya hii miradi tunayoipanga *especially* hii miradi ambayo tunaita *flagship projects*. Ukifanya tathmini vizuri kwenye Mpango ullopita utagundua tulikuwa na miradi karibia 20 na yote ni mikubwa. Miradi 20 yote hii hatuwezi kui-*finance* na kodi za wananchi za kwetu za ndani. Kwa hiyo, ni vema tujikite kama taifa na ni wakati muafaka sasa tukubali tu kwamba ili tuitengeneze hii miradi ni lazima tutafute *sources* nyingine, namna nyingine ya kuitekeleza ama kwa *partnership* au kwa kukopa lakini tuifanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huohuo lazima twende na tahadhari, tumejaribu kufanya *partnership* pale Liganga na Mchuchuma na mradi huu umezungumzwa sana tokea tuko shule na bado mpaka leo haujatekelezeka. Naishauri Serikali yangu sikivu kama hili la Liganga na Mchuchuma limeshindikana kwa mwekezaji huyo tuliyenaye, ni vyema tukaenda mbele tukatafuta mtu mwingine kwa sababu dunia kwa sasa ni chuma na mafuta. Ni bidhaa mbili tu zinazotawala soko la dunia za mafuta na chuma. Kwa hiyo, tunapochukua muda mrefu miaka 7 toka 2014 tunafanya mazungumzo tunajichelewesha tu wenyewe. Tunahitaji tu-*mobilize* fedha kutokana na hii miradi ya kimkakati ambayo tunayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, mimi ya kwangu yalikuwa hayo machache. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau, Mheshimiwa Fakharia Shomari ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia

nafasi ya kuchangia katika Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii. Kwanza kabisa, nimpongeze Rais kwa usimamizi mzuri wa miaka mitano hii kwa ambacho kimefanyika, ni *very impressive*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nataka nijikite kwenye suala la mchango wa sekta binafsi. Nimejaribu kupitia hapa Mpango, naona sekta binafsi tunategemea ichangie *almost 40.6 trillion shillings* na nikafanya *average* kwa mwaka ni *8.12 trillion*, huo sio mchango mdogo sana kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu ambacho nimekuwa najjuliza, nimekaa sekta binafsi kwa muda mrefu, labda kwa upande mwingine ningepomba Serikali pia ihusike kwenye ku-*support* sekta binafsi. Kwa nini nasema hivi? Ni kwa sababu unapoiweka sekta binafsi kwenye Mpango halafu huishirikishi mipango kidogo inakuwa gumu maana tunawaacha wanakuwa *separate* halafu baadaye tunaenda kukamua maziwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nayasema haya? Sasa hivi nimetoka kwenye Kamati tulikuwa na semina nikajaribu kuuliza swali kwa watu wa *TANTRADE* kwamba nyie kazi yenu kwa sehemu kubwa ni kuhakikisha mnatafuta masoko na mnashauri. *How many times* mmechukua muda wa kwenda kushauri sekta binafsi, maana nitaenda nitamkuta Mheshimiwa Musukuma na biashara yake ya mabasi naanza kuchukua kodi pale, lakini Mheshimiwa Musukuma amekuwa anaongea humu anasema darasa la saba ndiyo matajiri au ndiyo mabilionea tunaweza kuona kama anafurahisha lakini *reality* ipo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kitu kimoja kifanyike, ni lazima Serikali ijikite kwenye kuhakikisha tunashirikisha sekta binafsi kwenye mipango yetu, maana wapo matajiri au wafanyabiashara ambao leo hawajui hata Ilani ya CCM inalenga nini lakini wapo kule. Wale watu wanakopesheka kwenye mabenki na wana uzoefu wa

biashara, kwa hiyo, tukiwatumia vizuri wanaweza wakatusaidia kwenye kukuza uchumi. Maana hapa *basically* tunachojaribu kukiangalia ni nini? Tunajaribu kuangalia *possibility* ya ku-raise pesa kutoka sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ambacho nashauri ni kitu kimoja, tuangalie Serikali iweze kuwatafuta hawa watu, tusiwatafute kwenye makundi maana wafanyabiashara wa Tanzania kwa sehemu kubwa kila mmoja anaficha mambo yake, hakuna mtu ambaye yuko tayari kufunguka. Ukiita semina ya wafanyabiashara hapa hakuna ambaye yupo tayari kufunguka, lakini tukijaribu ku-*identify* labda wafanyabiashara kumi *potential*, tukaangalia huyu mtu uwezo wake ni mkubwa katika *industry* fulani na bado benki anaweza akakopesheka. Huku mfanyabiashara kupata bilioni 300, bilioni 400 benki unampelekea *idea* ya biashara maana tunahangaika na viwanda hapa, kuna mwingine yupo kwenye mabasi lakini anaweza akajenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute kupitia *TANTRADE*, iende imshauri, tuwatembelee hawa watu tusikutane nao tu wakati tunatafuta kodi maana haya mambo hata kwenye halmashauri zetu huko yaani Afisa Biashara ni kama Polisi, yeye atatembelea duka lako, atatembelea sehemu yako ya biashara anakagua leseni au anakagua vitu vingine. Wapate muda wa kuwatembelea watu hawa, ujue huyu mtu ana shida gani, *sometimes* mtoe hata *out* maana *private* ukijaribu kuangalia wanaotu-*train private* aliongea mtu mmoja aliyekuwa anachangia asubuhi, kwamba *investment* hata kwenye Makampuni ya Simu na Serikalini huku ni tofauti, yaani unayemweka am-*audit* mtu wa *private*, mtu wa *private* anajua zaidi kwa sababu wale watu wame-*invest* hela nyingi Zaidi, sisi tumekuwa tunasafirishwa tufanye kazi *private*, tunasafirishwa sana na makampuni nje, sio kusema yule mtu hakusafirishi tu bila manufaa, anataka uelewe ili kurudi umfanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hali kadhalika hata watumishi wetu umma watafute muda wa kukaa na watu wa *private*, wawaulize matatizo yao ni nini.

Wawatembelee hata ofisini, wawatoe hata *out* jioni wakae sehemu waongee hizi bajeti ziwepo, maana hawa watu washirika, mtu wa kukuchangia trilioni 40 kwa miaka mitano huwezi tu kuwa unakuta naye kwenye *tax collection*, hapana lazima tuwatafute tushirikiane nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limekuwepo, watu wengi sana wameongelea habari ya *TRA*, niombe Serikali. Nimekuwa kwenye biashara, tunafanya kazi na Serikali, una-*supply* mzigo au *contractor* anafanya kazi, baada ya hapo kuna *raise certificate*, ipelekwe wizarani, baadaye iombewe hela hazina ije ilipwe, inachukua *almost* miezi miwili au miezi mitatu ndio hela inakuja. Hela inafika kuna maelekezo sasa hivi kwamba kabla ya kumlipa mkandarasi au *supplier* yoyote yule, uanze kwanza kuwauliza *TRA* kwamba huyu mtu anadaiwa. Sasa hata yule niliyefanya naye biashara taasisi ya umma naye amegeuka *tax collector*, leo hanilipi hela yangu kwamba kama nadaiwa ile hela anaihamisha moja kwa moja inaenda *TRA*. Jamani nafanya kazi na wewe, ni mfanyabiashara unajua ofisi yangu, nilipe kwanza maana sisi tunakopa kwenye mabenki, hawa ndio *partners*, sasa leo ukichukua bilioni yote na mtu wa *TRA* anakwambia unadaiwa, *sometimes* anakwambia ile ilipe kwanza, ikishalipwa kwanza tutakuja tuta-*negotiate*, hela haiwezi kuingia kule ikarudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachoomba, *TRA* wasiwe Polisi, hawa ni *partners*, ni watu wa kufanya nao biashara, tuwashirikishe lakini tushirikiane nao maana wako *registered*, kila mfanyabiashara tunajua alipo na hizi trilioni 40 ndio hao wanaotakiwa wazichangie lakini tusiwa-*discourage* kwenye biashara. Nasema hili kwa sababu haya mambo yanatokea sana hawa watu wanakata tamaa kuendelea kuwekeza hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nije nalo, kwa sababu ya muda nilikuwa najaribu kupitia, nikaangalia historia ya *Northern Ireland*, wale watu wakati wanataka kuanzisha viwanda...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha Mheshimiwa, lakini unaruhusiwa kupeleka mchango wa maandishi, kwa hiyo usiwe na wasiwasi.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantumu Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar na Mheshimiwa Almasi Maige ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya wakati huu. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kunirejesha tena kwa mara ya pili katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikupongeze wewe maana kipindi kile tulikuwa pamoja tumefanya kazi pamoja, pamoja na Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze na Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kunitua na kuniamini na kunirejesha tena katika Bunge hili Tukufu. Kwa kweli tushukuru Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mfupi, tuna mengi ya kusema, lakini tutapopata ndio tumefanikisha. Mpango huu umefika kwa wakati muafaka na Mpango huu mambo yake mengi yaliyokuwamo humu yamejikita pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Rais, yameendana pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia kuhusu Mpango huu, kwanza huu Mpango nataka kusema umefika wakati muafaka na hili suala langu ambalo ninalolitaka kulisema hapa hivi sasa na suala hili la muda mrefu na suala hili linanikereketa, nikienda nikirudi bado lipo ndani ya nafsi



yangu, lakini hivi sasa hivi nataka kulitoa katika Mpango ambao uliofika hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusu sehemu ya Muungano, sehemu ya Muungano kuna magereza ya Zanzibar pamoja na magereza ya Bara. Magereza ya Zanzibar na magereza ya Bara, magereza ya Bara yanafanya kazi kwa wakati wake na magereza ya Zanzibar yanafanya kazi kwa wakati wake. Naomba kwa Mpango huu ili kuunganisha huu Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, je, haiwezekani magereza haya yakaweza kuunganishwa, ikawa kitu kimoja kama ilivyo Polisi na Jeshi? Hilo lilikuwa linanikereketa na leo hii limefika mahali pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kusema kuhusu suala la afya; suala la afya na wagonjwa na sukari, shinikizo la damu pamoja na *pressure*. Magonjwa haya yametawala nchini, yako mengi, haya magonjwa hayaambukizi, lakini ni magonjwa sugu, yanaumiza na wala hayana dawa. Maana kuna wenzetu ambao wamepata maradhi haya wanyonge, maskini, hawana kipato cha kuweza kujiwezesha ili kujitibu magonjwa hasa shinikizo la damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa una sukari, ukiambiwa usile hiki, usile hiki unaweza ukapona, ukaifuata miiko yake, lakini shinikizo la damu gumu. Kwa hiyo naomba Mpango huu pamoja na Serikali yangu iweze kuwaona wagonjwa hawa wa sukari, *pressure* pamoja na shinikizo la damu ili wawezeshwe wapate dawa za kuweza kujitibu ili waendeleo na wao kufanya kazi zao kama tunavyozifanya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Chuo cha Hombolo; hiki chuo kizuri nilikwenda nikakitembelea, kizuri sana na kina mambo yote ya sayansi na teknolojia. Hata hivyo, hiki chuo kiko mbali. Sasa umbali wake ni nini? Ni kuhusu barabara ya kuendea Hombolo kwani ni mbovu, chafu, haifai. Naomba barabara ya Hombolo kwa Mpango, Mwenyezi Mungu akatujalia, basi barabara ile mwaka huu

iwezeshe, itengenezwe ili watoto na siye tuweze kuwapeleka kule ili waweze kwenda kusoma katika kile Chuo cha Hombolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu suala la ukosefu wa nyumba za askari; ukosefu wa nyumba za askari ni mkubwa hasa kwa Mkoa wetu wa Kusini, Mkoa wetu wa Kusini una wilaya mbili, Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini, lakini Wilaya ya Kusini ni mkoa bora, ni mkoa mama ambao unaweza kuchukua watalii wakawa wanakwenda kutalii katika wilaya ile, lakini nyumba za askari hakuna na wala hawana mahali pa kukaa, wanahangaika hangaika isipokuwa kituo kidogo kipo Paje, pale kidogo lakini Jambiani hakuna Kituo cha Polisi, naomba napo kiende kikajengwe kituo cha polisi...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kengele imeshagonga.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** ...ili na wao waweze kujisikia. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia Shomar atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye kuumba mbingu na ardhi, vilevile kukushukuru na wewe Mwenyekiti ambaye ndio Naibu Spika na Mheshimiwa Spika na uongozi wote wa Bunge pamoja na Waziri Dkt. Mpango kwa huu Mpango wake uliokuwa mzuri, bora na uliotukuka, pamoja na Chama changu Cha Mapinduzi kilichoniwezesha kufika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kidogo ukuaji wa pato la Taifa ambalo limeendelea hadi kufikia 6.9 na vile kufika katika kundi la uchumi wa kati. Kwa kweli ni jambo jema na jambo kama hili linataka kupigiwa upatu kila leo ili wale waliokuwa hawasikii wasikie na wale waliojifanya

hawaoni, waone na wajue kwamba tuko vingine sisi Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuelezea pia mkakati uliokuwa umewekwa na Taifa ambao ni mkakati mkubwa, kwa mfano, ujenzi wa reli ya kati kiwango cha *standard gauge*; mradi wa kufua umeme wa maji; uboreshaji wa mashirika ya ndege; ujenzi wa barabara na madaraja, ni jambo la faraja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna deni kubwa hapa, tuko Dodoma ambapo ndio Makao Makuu ya Nchi, lakini hatuna uwanja wa ndege wa kuridhisha na uwanja wa ndege ndio unaoleta maendeleo ya nchi, Kiwanja kipo miaka 15 nyuma, lakini bado tunang' ang' ana na kiwanja kidogo, kiko katikati ya mitaa ya watu, sasa hili Mheshimiwa Dkt. Mpango aliangalie, nini tatizo wakati hapa ni Makao Makuu ya Mji na mikoa mingi imepakana? Kuna mikoa mingine haina viwanja vya ndege itakuwa rahisi wakitua Dodoma wakaweza kufika katika mikoa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo nataka katika mipango yetu tunayopanga, mpango ni mzuri lakini unakuwa na upungufu mdogo mdogo ambao tuukumbuke ili tuweze kuushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ambaye katika ukurasa wake wa 31 alielezea elimu stadi kazi za ufundi wa vijana wakimaliza elimu waweze kujajiri; hili nimelikubali mia kwa mia. Elimu yetu kwa kweli tunaosomeshwa *school* ni ya kukariri ili upate shahada, ukimaliza kama umepata *degree* umepata *Master* ndio umemaliza, lakini kama utampa elimu stadi ya ufundi, akimaliza anajua anakwenda kufanya nini. Kijana huyu hata kama atakuwa ni fundi cherehani, lakini anajua nikiondoka nakwenda kufanya kazi fulani, kama nitakwenda kutengeneza baiskeli au kutengeneza magari. Hayo yote tunayafanya mtu aende ajibagize bagize kwenye magari mabovu afundishwe, lakini kama atapata toka *school*

itamsaidia na ajira zitakuwepo, hatutoweza kutegemea ajira ya Serikali kwa sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale vijana watakaobahatika, watabahatika na tutakaobakia tutafanya kazi zetu wenyewe za kuzalisha mali kwa kufanya kazi nyingine hata kama kutakuwa na viwanda, wakati mtu unampeleka kiwandani, hana stadi ya elimu anaenda kufanya nini? Ina maana itakuwa umempeleka mahali akaanze kufundishwa, ambapo kile atakachofundishwa atakuwa shambaganga tu lakini sio uwezo wa kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye uchumi wa *blue*, uchumi wa *blue* ambao tunaiongelea bahari na bahari ina mazao mengi na bahari kuna wazee wetu wanafanya kazi kwa kutumia urithi wa babu, baba na mjomba, lakini haijui vipi bahari ilivyo. Sasa ningeshauri elimu ya bahari ingeanza kufundishwa kuanzia elimu ya msingi mpaka tunamaliza vyo, unamjua mtoto ushampanga, anajua bahari ikoje na anajua mazao ya bahari yanapatikana wapi. Sasa Serikali wakati itakapojitahidi kutafuta vifaa na watoto wameshasomeshwa, wanajua nini wanachokifanya, litakuwa ni jambo jema, ina maana tutaitendea haki *blue economy* na kila mmoja atajua anachokifanya. Ushauri wangu napenda masomo ya uchumi wa blue wasomeshwe vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya mpango na kwa sababu muda ni mchache nitajikita kwenye mambo mawili tu, nayo ni elimu na lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni zao la shule ya ufundi, tulisoma sisi kutoka Moshi *Technical*, kutoka Ifunda tukaenda *technical college*, tukatengeneza watu wanaoitwa *FTC (Full Technician Certificate)* na hawa ndio waliojenga viwanda, waliofanya kazi kwenye viwanda mpaka vilipokufa, lakini sasa elimu ya ufundi imekuwa hadithi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea uchumi wa viwanda, kama hakuna mafundi wa kutengeneza mitambo ndani ya viwanda hivyo, vitakufa. Ni sawa na magari yetu haya, kama hatuna *garage* ya kupeleka na mafundi wakawepo huko, magari hayawezi kuwa magari. Tulikuwa na mfumo mzuri sana wa elimu, kutoka shule za sekondari ufundi, *form one* mpaka *form four* unasoma umeme, unaenda *technical college* unasoma umeme, unamaliza *FTC* unarudi tena kusoma *engineering*, umeme miaka kumi mtu huyo anafanya kazi kiwandani kwa kujiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limekufa toka marehemu Mungai alipofuta vyyo vya kati hapa akafuta na *FTC*, sasa tunafanya nini tunaendelea kukuza *VETA* na nashukuru sana *VETA* zinatengeneza mafundi wa vijijini, kwa hiyo uchumi utakwenda vijijini watatengeneza magari kule, watatengeneza mavitu ya umeme na kadhalika, kwa hiyo, watapata hela vijijini na uchumi utakua vijijini. Hata hivyo, hawa hawatafaa kiwandani, wako chini au ni wa ngazi ya chini ya ufundi unaoitwa *artsan*. Baada ya *artsan* kuna *FTC* halafu ndio kuna *engineer* pale juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kazi ndiyo huwa unafanyika hivyo, *engineer* anafanya kazi na watu *technicians 25*, *technician* mmoja na *Artsans 25*, ndipo unakuwa mfano wa ufundi. Sasa viwanda hivi ambavyo tunakusudia vikuze uchumi, lazima tuwe na elimu ya ufundi ambayo itaendana sawasawa na uchumi tunaoutaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba chuo cha ufundi kiazishwe upya, *DIT*, sio chuo cha ufundi sio *technical college*

imekuwa *academic institute*, Dar es Salaam *Institute of Technology* haitengenezi watu wa *FTC blue color* tunatengeneza *white color*. Kwa hiyo, *degree*, narudia tena *degree*, hazitatusaidia kukuza uchumi na ndio maana ziko nyingi mtaani zinatafuta kazi. Tunataka *technicians*, fundi sadifu na fundi mchundo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hatua ya pili, lugha ya kufundishia, kote duniani, hakuna nchi iliyoendelea kwa kutumia lugha ya watu wengine. Tunataka Kiswahili kitumike kwenye lugha ya kufundishia, shule ya msingi mpaka *secondary school*. Hivyo wanafunzi watakuwa na fursa ya kujifunza taaluma, sio kujifunza lugha. Tunataka Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kichina vifundishwe kama lugha katika shule zetu, lakini lugha ya kufundishia elimu iwe Kiswahili. Na-*declare interest* nitaleta katika Bunge lako hoja ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige, ku-*declare interest* ni nini kwa Kiswahili? (*Kicheko*)

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, nataka kuelezea maslahi yangu ya hapo baadaye kwamba, nitaleta hoja binafsi kama Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia elimu yetu. Nilifanya *research* ndogo au tafiti mdogo tu utafiti mdogo wa Kiswahili kinafaa kufundishia au hakifai, watoto wanielezee jinsi ya kupanda muhogo, darasa la saba wote wakapata, lakini wote nikawaambia andikeni sasa Kiingereza, wakaandika wote wakakosa, hakuna hata mmoja aliyepata hata chini ya 20 hawakupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya mama ndiyo inayomfundisha mtoto, tafiti nyingi zimefanyika, watu wengi wanapinga Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia, hawasomi tafiti zilizofanyika, lakini pia wanakumbuka mambo ya nyuma. Nimekaa Uingereza miaka saba, watu wote mtaani kwangu wanaongea Kiingereza lakini hawajui kusoma wala kuandika. Hapa ndivyo ilivyo, watu wengi wanasema huyu mtoto anaongea Kiingereza kama maji kasoma, kumbe hajui chochote, lazima Kiswahili kitumike kama lugha ya

kufundishia. Sasa hivi limekuwa jambo gumu sana, tunasoma darasa la kwanza mpaka la saba Kiswahili, halafu tunabadilisha kama masafa ya redio kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Watoto wakifika kidato cha kwanza, wanaanza kujifunza Kiingereza kwanza na wakati huo wanasoma masomo, wanafeli, watoto wengi tumewaacha nyuma sio kwamba hawana elimu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja za msingi kabisa hizo. Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki ajiandae.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niungane na Watanzania wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. John Pombe Magufuli. Mheshimiwa Rais amefanya kazi nyingi kubwa na wataalam wa Kiswahili wanasema mwenye macho haambiwi tizama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi zinatoka ndani ya nchi na nje ya nchi. Ukiwa nje ya nchi unaposema tu unatoka Tanzania kwanza lazima upokee salama na pongezi za Mheshimiwa Rais. Utaambiwa tunampenda sana Mzee Magufuli, anafanya kazi na amekuwa ni mfano ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Afrika na duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashukuru wananchi wa Njombe kwa ridhaa yao ya kunirudisha tena mjengoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye suala nzima la kilimo. Mikoa ya Kusini kwa asilimia kubwa sana wamejikita kwenye masuala ya kilimo na Mkoa wa Njombe kuna kilimo cha mazao mengi kama viazi, mbao zinakwenda mpaka nje nchi ndani ya Jumuiya ya Africa Mashariki ambapo kuna masoko mengi sana lakini pia kuna suala nzima la mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano eneo la mahindi na pembejeo wamefanya kazi nzuri lakini tuendeleo kuangalia bei za mbolea ni namna gani tutaweza kufanya ili mbolea iendeleo kuzalishwa nchini ili bei ipungue. Sasa hivi mfuko mmoja kwa mbolea ya kukuzia ni Sh.50,000 hadi tumalize kilimo, mkulima anakuwa amewekezq sana. Kwa hiyo, eneo la pembejeo za kilimo hususani zao la mahindi, naomba tuendeleo kuliboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nipongeze kwa masoko ambayo yako na masoko mengi sasa hivi ni soko huria lakini kwa kweli tunahitaji kuona *intervention*, ni namna gani tunahakikisha wananchi wakishalima zao hili la mahindi wanapataje masoko ya uhakika. Nilete salama kutoka Mkoa wa Njombe, nadhani Waziri wa Kilimo ananisikia, yupo hapa jirani yangu wanaomba mahindi yakanunuliwe. Kuna mahindi mengi sana, ili yasiweze kupotea kutokana na upotevu unaotokea mara baada ya kilimo na kwenye hotuba imesekana wakati mwingine 40% ya mahindi wakati mwingine yanapotea (*postharvest*) basi tuone namna ya kuyanunua mahindi haya. Kuna mahindi mengi wanaomba SGR, NFRA ikiwezekana wakayanunue na wawaunganishe wakulima wa Mikoa hii ya Kusini na maeneo mbalimbali kama *World Food Program*, *FAO*, tuna kambi nyingi za wakimbizi wanahitaji chakula cha kutosha tuone namna gani ya kuunganisha eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine naanza na pongezi ni suala nzima la elimu. Sasa hivi uandikishwaji wa watoto umetoka asilimia 93 mwaka 2015 sasa hivi tuko takribani asilimia 110. Tunapoelimisha vijana wengi maana yake wanakuwa na ubunifu, wanaweza wakabuni bidhaa



na huduma mbalimbali na kuzalisha. Kwa hiyo, eneo hili ni muhimu lakini sasa tuangalie na vyuo vya maendeleo, kuna maeneo ambayo tuna miradi ya mkakati (*flagship projects*) tunahitaji vyuo vya maendeleo ambavyo vitasaidia ku-boost miradi ile. Kwa mfano, maeneo ya Miradi ya Mchuchuma na Liganga, *Mwalimu Nyerere Hydroelectric Power*, tuhakikishe tunavyo vyuo vya kutosha ili kuimarisha vijana ili waweze kupata ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ludewa mpaka sasa hawana chuo cha VETA. Nitumie nafasi hii kwenye mpango huu tuone namna gani tunaweza tukatumia *force account* ili waweze kuweka VETA pale ambayo ita-boost Miradi ya Mchuchuma na Liganga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nipongeze sana Mradi wa Mchuchuma na Liganga upo kwenye Ilani na pia umeelezwa vizuri sana kwenye Mpango. Pamoja na hiyo, tuangalie suala zima la fidia kwa wananchi kama tumeshalikamilisha siyo tu katika Mradi huu wa Mchuchuma na Liganga lakini na miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika maeneo ya madini kuna suala la wachimbaji wadogo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mheshimiwa Aleksia Kamguna ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wote ambao walisema kuna umuhimu kama Taifa kupima ardhi yote. Wakati wa Uchaguzi Mkuu CHADEMA tulisema *is very possible* kupima ardhi na kutoa hati kwa

wananchi kwa sababu kuna *potential* kubwa sana kupitia kodi ya ardhi kwa nchi kuweza kupata mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wote ambao wanaitaka Serikali ije na mpango mahsusi wa kuhakikisha sekta binafsi ya Tanzania inashamiri. Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye tathimini ya mpango wake wa 2011-2015 na mpango unaokuja anakiri kuna changamoto ngumu sana kwenye sekta binafsi, ushiriki wao hauridhishi. Lazima tujiulize maana lazima unapofeli ufanye tathmini kwa nini ni ngumu kwenye eneo hili muhimu tunalotarajia lichangie zaidi ya 40 trilioni kwenye mpango wetu huu mpya tumeshindwa kulivutia kuwa ni sehemu muhimu wa maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia ndugu yangu hapa akisema wasiosikia na wasikie, wasioona na waone, ndugu yangu tunapofanya tathmini ni muhimu tuwe wakweli pia. Mimi niwashauri Wabunge hawa kwa sababu ni mkongwe kidogo, tukija na *mentality* ya kusifia *SGR*, *Stigler's Gorge* na madaraja ya Dar es Salaam, hatuwezi kulisaidia taifa kwa sababu hivyo vitu vitatu *is no longer breaking news*. *Stigler's Gorge* ilianza kuzungumzwa miaka mingi sasa hivi inajengwa asilimia 25, *SGR* tulianza kuzungumza tokea enzi hizo iko kwenye mipango imeanza kutekelezwa kidogo na nyienyeie Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kikubwa, Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango katika Kitabu chake cha Maendeleo; tathmini yake mwenyewe kwenye kitabu chake, amekiri kwa maneno yake na nitarejea na mengine jana walirejea Waheshimiwa Wabunge. Katika ukuaji wa uchumi bado hatujafika, pato la kila mtu bado hatujafika, mapato ya kodi ya Serikali kwa mwaka *vis-à-vis* pato la taifa bado hatujafika, uwiano wa mapato kwa pato taifa bado hatujafika, kiwango cha umaskini bado hatujafika, uwekezaji wa mitaji kutoka nje bado hatujafika, uzalishaji wa umeme bado hatujafika, usambazaji wa umeme bado hatujafika, vifo vya kina mama na watoto na huduma za maji vijijini bado hatujafika, kilimo bado hatujafika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali, Mheshimiwa Mwigulu tuliza mzuka, kama Serikali yenye wataalam wa uchumi na wa kupanga wanaweka mipango, wanashindwa kutimiza malengo, afadhali mengine wanaweza wakawa wamefika kidogo, inakaribia lakini mengine ni mbingu na ardhi *then* tuna shida na wataalam wetu. Wakati tunaelekea kwenye Mpango wa Tatu lazima tufanye tathmini, nimesema hivi mimi ni mkongwe unanisoma vizuri, Wabunge hapa wakati wa maswali asubuhi, swali la maji ulitoa maswali ya nyongeza mpaka unataka kutoa maswali ya ziada ya nyongeza huku umesimama lakini mimi niliyekuwepo wakati wa Mpango wa Kwanza huu wa miaka mitano (2011-2016) kati ya mwaka 2012-2014 asilimia 27 ya manunuzi ya nchi yalikuwenda kwenye maji. Fedha iliyotumika kwa miradi ya maji kwa CCM hii kwa kipindi hicho tu na siyo maneno yangu mimi, ni maneno ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyefanya *special auditing* akasema kati ya shilingi 2.7 trilion zilizokuwa *injected 49 percent* ya miradi haifanyi kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnapokuja hapa SGR, *Stigler's Gorge, what is that!* Ndiyo maana watu wanatushangaa, lazima tu-move. Serikali ikiwa madarakani aidha umechaguliwa au umeingia kiunjanja, ni jukumu lako wewe kuhudumia wananchi. Kuhudumia wananchi siyo hisani viongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kuamini na kuwa na *mentality* kwamba kuhudumia Watanzania ni hisani, ndiyo maana kuna vijana wadogo hapa wanatushangaa tokea wako *primary* wanaona wazee wazima tunaongelea *Stigler's Gorge*, wanakuja *secondary* wanaona tunazungumzia SGR, wanakuja Bungeni wanakuta ngoma ile ile, wanajifunza nini kutoka kutoka kwetu?

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Umeshaanza Mheshimiwa Jenista

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui tumsaidieje Mheshimiwa Halima Mdee, hii miradi yote ambayo ya vielelezo, ni miradi ambayo kwa maamuzi thabiti ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, utashi wa kisiasa wa Rais John Pombe Joseph Magufuli, ndani ya miaka mitano tu ya Serikali yake miradi hii imeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ilikuwa haijatekelezwa siku za nyuma si imeanza sasa kutekelezwa! Kuanza kutekelezwa kwa miradi hii kunaonyesha ni kwa kiasi gani Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga kuleta maendeleo endelevu ya Taifa la Tanzania. Kwa nini Mheshimiwa Halima asikubali jambo hilo? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, unaipokea taaria hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Jenista alikuwepo kwenye Serikali zote hizi, Magufuli alikuwepo kwenye Serikali zote hizi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, ngoja kidogo, kwa Kanuni zetu hawa ni Waheshimiwa kwa hiyo wataje vyeo vyao.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Jenista alikuwepo kwenye Serikali zote hizi, Mheshimiwa Magufuli alikuwepo kwenye Serikali zote hizi na Serikali ya Awamu ya Tano iliahidi kwenye Mpango uliopita kupunguza kiwango cha umaskini kutoka asilimia 28 mpaka asilimia 16, mmeweza kupunguza kwa asilimia 2 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka kusema hapa *mentality* ya kufikiria unapotoa ama unapotekeleza wajibu ni hisani, ndiyo haya unafikiria likijengwa daraja pale eti wananchi wa Tanzania wamesaidiwa, hawajasaidia kwa sababu mnakusanya kodi. Ninachowashauri hapa tukiwa tunaeeleka Mpango wa Tatu tufanye tathmini tuone tumekosea wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila mtu anajisifia, ooh, kuna ujenzi, sikiliza miaka mitano ya Mpango huu ujenzi imepewa trilioni 8 sasa kwa nini sekta ambayo mmewekeza trilioni 8 isikue? Hiki kilimo ambacho kila mtu anakizungumzia hapa na jana amezungumza aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Muhongo kwamba kama tunataka hiki kimuhemuhe cha kusema nchi yetu ni tajiri kiwe *reflected* kwa wananchi kule chini tuwekeze kwenye maeneo yanayogusa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kilimo *average* ya kutoa bajeti ya maendeleo ni *17 percent* kwa miaka mitano iliyopita. Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango mwenyewe anasema eti miaka mitano kwenye kilimo tumetoa shilingi bilioni 188, hatusemi Serikali ilime, hapana, tunasema itengenezwe miundombinu wezeshi. Nchi hii ina utajiri wa umwagiliaji, hivi tutapoteza nini kwa mfano, hawa wakulima wetu wadogo wadogo tukisaidia kuweka mifumo thabiti ya umwagiliaji? Leo ni aibu asilimia 90...

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, kuna taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashungwa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, Halima ni Mbunge mbobezi na mzoefu na anajua uchambuzi wa bajeti unavyokwenda. Uchambuzi wa bajeti unavyokwenda na unavyopangwa kwa utaratibu wa *circle* lakini utaratibu wa Serikali, bajeti ya kilimo haihesabiwi kwenye fedha zinazopelekwa kwenye Wizara ya Kilimo peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Kilimo, Halima anajua, ningemwomba Halima anapoweka hii hoja mezani aeleze bajeti ya kilimo iliyokuwa *budgeted* kwenye Wizara ya TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, achukue bajeti zote za kisékta zinazoenda kuzungumzia sekta ya kilimo kwenye sekta mtambuka fungamanishi, akizichukua zile zote atakuja kupata bajeti halisi ya kilimo ambayo ilikuwa imetolewa na Serikali katika kipindi anachokisema.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuipokea kwa sababu mimi nafanya rejea ya hotuba ya Mchumi mwenyewe wa nchi, Waziri Mpango. Sasa kama Mchumi wa nchi anasema tumetenga shilingi bilioni 188 mimi ni nani? Mheshimiwa Jenista Mhagama ni nani wa kubishana na Mchumi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachoshauri kupanga ni kuchagua. Tuna nia ya kusaidia Watanzania wenzetu lazima tuangalie sekta zinazogusa wananchi walio wengi.

**MBUNGE FULANI:** Muda hauishi? *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sekta hii tumeipuuza sana lakini bado kwa heshima kubwa inachangia pato la Taifa kwa asilimia 26.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Gwajima tulia.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa kabla hajamaliza.

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja. Mheshimiwa Halima Mdee, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sawa namwambia atulie.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba mchangiaji aliyepita amekiri kuna mambo yamefanyika na ametaja zile asilimia. Kwa hiyo, ni sahihi kabisa Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Rais kwa kazi nzuri aliyofanya kwa sababu hata yeye amekiri kwamba kuna kazi inafanyika, kwa hiyo, ni halali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki atafuatiwa na Mheshimiwa Aleksia Kamguna, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani ajiandae.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ili leo niweze kusimama

hapa na niweze kuchangia katika Mpango huu ambao umeletwa katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wanananchi wa Tarime, wapiga kura wangu kwa kura nyingi walizonipa ili niweze kuwakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Najua wana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi lakini pia wana imani kubwa na mimi, niwahakikishie kwamba nitawatendea haki kuwakilisha vyema kuhakikisha kwamba mji wetu unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichukue nafasi hii kushukuru chama change, Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na kuiteua kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi na hatimaye tukapata ushindi mnono katika jimbo ambalo lilikuwa limekaa upande wa pili kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Nikianza upande wa elimu, Serikali imefanya kazi kubwa ikiwemo ujenzi wa miundombinu muhimu katika shule zetu zaidi ya 3,904 kwa mwaka 2019/2020. Vilevile imetoa elimu bure kwa shule za msingi na sekondari na imetoa pesa nyingi kugharamia masomo hayo ambayo imewezesha watoto wetu kupata elimu kwa wingi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu mchango wangu nitauielekeza sana upande wa ukusanyaji wa mapato. Ili nchi iweze kusimama na iweze kutekeleza miradi ambayo imepangwa katika kipindi cha mwaka huu au miaka inayokuja lazima iwe vizuri katika ukusanyaji wa mapato ili uweze kupata fedha ya kutosha kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mashaka kidogo kuhusiana na ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu na hii nipeleke kwa TRA. Mfano katika Jimbo letu la Tarime Mjini



hakuna mahusiano mazuri kati ya *TRA* na wafanyabiashara. Mfano *cement* katika Mji wetu wa Tarime inauzwa Sh.24,000 ambapo *cement* inayotoka katika nchi jirani ya Kenya inauzwa Sh.16,000. Kipato cha watu wa Tarime bado kipo chini na wanahitaji kujenga na ukiangalia *cement* inayotoka katika nchi jirani inauzwa bei ya chini tofauti ya Sh.8,000. Hivyo basi, naomba Mamlaka ya Mapato na Bunge hili Tukufu tuangalie namna gani tunaweza kufanya ili hizi kodi ambazo ni kubwa zinazopelekea wafanyabiashara kukwepa kodi ziangaliwe upya. Waziri Mpango aweze kuleta hoja hapa ili hizi kodi ziweze kuangaliwa upya ziweze kusababisha wafanyabiashara walipe kodi bila kukwepa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisikitisha ni kwamba badala ya *TRA* kutoa elimu kwa wafanyabiashara na kwa wananchi inatumia nguvu kukusanya kodi. Mfano kama mfanyabiashara au wale wanaoendesha bodaboda amekwenda kuchukua *cement* moja Kenya analeta huku, wanatumia gharama kubwa kufukuza vijana hawa na mwishoni vijana hawa wamekuwa wakiumia na wengine hata kufariki wakitumbukia kwenye mitaro na kujigonga pembezoni mwa barabara. Naamini njia pekee ambayo tungeweza kufanya ni *TRA* kukaa chini na wafanyabiashara waone umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari bila kufukuzana nao. Pia kutoa elimu kwa wananchi, mfano, ukienda kununua *spear* dukani unaambiwa bei mbili; ya kwanza unaambiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge hoja mkono lakini pia nina mambo mengi ya kusema. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aleksia Kamguna atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mheshimiwa Sylvia Sigula Francis ajiandae. Mheshimiwa Aleksia.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Sigula Francis, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nimshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ni Mjumbe namba moja wa Chama Cha Mapinduzi na wajumbe wengine kwa kupendekeza jina langu kurudi kwenye kinyang'anyiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa sababu ndicho chama kinachotekeleza ilani na mambo yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia dada yangu Mheshimiwa Halima akipongeza watu mkawa hamumuelewi. Amesema Awamu ya Tano yapo yanayofanyia mazuri, ndicho alichosema, msipate shida sana, wataelewa tu, wamekuja na wataendelea kuja wala msipate shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasimu hii ya Mpango iliyoletwa kuna mambo ambayo *at least* nataka niishauri Serikali. Ukisoma maelezo ya rasimu ya Mpango wa 2021 na ile yenyewe ya 2021-2026, kwenye suala la kilimo ambalo tumelizungumza na mimi nagusa sana kilimo kwa sababu asilimia 98 ya jimbo langu ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Waziri wa Mipango, tunapokwenda kuileta bajeti yenyewe ya mpango kabisa Wizara yetu ya Kilimo ambayo ukisoma Bajeti ya mwaka 2019/2020 ilitengewa asilimia moja tu ya bajeti kuu. Kilimo ambacho kwa maelezo yenyewe ya mpango yanasema kinaajiri watu zaidi ya asilimia 65, sasa *reflection* yake Watanzania wanaotegemea kilimo ni wengi bajeti inayokwenda kwenye kilimo ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda kusoma hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo amekielezea kilimo kwa mapana yake sana ukurasa ule wa 13 ameelezea vizuri sana. Nami hapa nataka Waziri wa Kilimo anisikilize vizuri sana. Mwaka 2017/2018 waliondoa fedha ya *export levy* ambayo ilikuwa inawapelekea wakulima pembejeo. Rais kwenye ukurasa huu wa 13 ametoa maneno ambayo nadhani Wizara ya Kilimo wana kitu cha kufanya na nataka ninukuu ili yawe mwongozo kwa Wizara. Mheshimiwa Rais anasema; "Kwa msingi huo, kwenye kilimo tunakusudia kuongeza tija na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kibiashara. Lengo ni kujihakikishia usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwandani na pia kupata ziada ya kuuza nje. Ili kufanikisha hayo tutahakikisha pembejeo na zana bora za kilimo ikiwemo mbegu, mbolea na viuatilifu vinapatikana." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Wizara wanatakiwa waende kwenye *extra mileage* na ndiyo maana tunataka mpango u-*reflect* na bajeti zao. Mheshimiwa Rais ameshaonesha dira hii kubwa, hii dira iwafanye watu wa kilimo sasa, kwa wakulima wetu tatizo la pembejeo tuone limekwisha, wakulima wetu tuone suala la dawa limekwisha. Rais amekwenda mbali mpaka matrekta, matrekta haya ya wakulima yanaishia mijini tu. Ukienda vijijini hakuna mtu anajua trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wizara ya Kilimo waende mbali zaidi. Hii nchi ina ardhi ya kutosha. Wakulima hawa wanapaswa sasa waache kutumia jembe la mkono. Tunapokwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda ni lazima twende mbali ambako wakulima tutawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo hiki zao la korosho ndiyo zao pekee duniani lenye makato makubwa na mengi kuliko zao lingine. Sasa Wizara hapa wana jambo la kutusaidia. Kwenye korosho peke yake mapato yanafika 745, ukiacha hayo ambayo wanayaona kwenye mjengeko wa bei wa 226, lakini ukienda ukaangalia *export levy*, ukaenda ukaangalia ndani kuna waendesha maghala shilingi 38. Jumla ya makato tu kwenye korosho ni zaidi ya

745, hakuna zao lolote Tanzania ambalo lina makato makubwa kama korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima wafike mahali waone kwamba wakulima hawa wa korosho waende kwenye makato wanayoyakata kwenye pamba, alizeti, mahindi kuliko mzigo huu mkubwa. Tutaendelea kulalamika bei ya korosho ni ndogo kumbe makato makubwa wanayachakata Serikali. Tuone namna ya kuendelea kuyapunguza makato ya wakulima hawa kwa sababu yamekuwa mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Rais alivyokuja kwenye kampeni alishatuhidi watu wa kusini, kuna barabara ile ya kutoka Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala na ipo ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Tuone sasa tunapokwenda kwenye bajeti barabara hizi zinatengewa fedha za kutosha ili tunapofika 2025, *story* ya barabara kwa eneo lile iwe imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji; tumekuwa kwenye tatizo la maji kwa muda mrefu sana. Kuna wakati amekuja Makamu wa Rais akatuhidi tungepata fedha za Mradi wa Maji wa Makonde. Badala yake tumerudi hapa miaka mitano Mradi wa Makonde umesogezwa umekuja kwenye miji 28. Tuone sasa Serikali inatenga fedha kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Makonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sylvia Sigula Francis, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nianze moja kwa moja kwa kuchangia mapendekezo ya Mpango uliopo mbele yetu. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha. Kwa kweli

ukiusoma mpango utaona kabisa dhamira ya dhati ya kutupeleka katika uchumi imara tunaoutarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kwa ajili ya muda nijielekeze katika Sekta ya Uvuvi. Tunapoteza sana mapato katika Sekta ya Uvuvi. Nasema hivi kwa sababu Tanzania tumebarikiwa. Tuna maziwa ambayo tungeweza kuyatumia yakatusaidia kutengeneza ajira nyingi lakini pia kukuza uchumi. Kwa sababu tukiangalia vipaumbele vyetu tunasema kipaumbele ni kukuza uchumi na pato la Taifa, lakini kwenye Sekta hii ya Uvuvi tunapoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hapa naona kwamba tutapanua Bandari za Kigoma na Tanga lakini pia kuboresha miundombinu. Nitoe mfano mdogo tu; tumekuwa na tatizo, japo limeahidiwa kwenye ilani, Meli yetu ya Liemba, kuanzia mwaka 2017 haifanyi kazi. Kwa kweli tumepata hasara na uchumi umezorota. Kwa hiyo maboresho haya yatakwenda sambamba na kuipatia Serikali mapato lakini pia tutatengeneza ajira nyingi kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Meli yetu hii ya Liemba na Ziwa Tanganyika, linawanufaisha watu wa Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa. Kwa hiyo kuwepo kwa fursa hii ya meli kutaweza kuchochea maendeleo kwa haraka, lakini pia kukuza kipato na uchumi. Pia tukiangalia Ziwa letu Tanganyika hili tunashirikiana na wenzetu wa Burundi na Kongo. Kwa hiyo kuwepo kwa meli hii kutachochea sana kipato na uchumi, lakini pia Serikali itaweza kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia pia naona kabisa kutokuwepo kwa meli hii kumezorotesha uchumi. Vijana wengi wamekosa ajira lakini pia hata usafirishaji wa mazao ambayo yanapatikana Kigoma, Katavi na Rukwa umekuwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali katika mpango wetu huu ni Mpango mzuri sana na ukiupitia Mpango mzima unaona kabisa tutatoka hapa kwenda /eve/ nyingine. Niombe marekebisho haya ya bandari hizi, upanuzi

huu ufanyike kwa haraka ili Serikali isiendelee kupoteza mapato yanayotokana na Sekta hii ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais nilijielekeza katika Sekta ya Sanaa na kwa sababu muda ulikuwa mchache nilishindwa kusema; siyo vibaya sana kujifunza kwa wenzetu wanaofanikiwa. Nimepata kusoma Makala moja, tunaambiwa wenzetu wa Nigeria mwaka 2013 suala la Sanaa lilichochea maendeleo sana na liliweza kuchangia zaidi ya robo ya bajeti yao katika Serikali yao. Kwa hiyo na sisi tunaweza tukatengeneza fursa nyingi kupitia huko, lakini tukubali kujifunza kwa waliofanikiwa, siyo dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye hotuba hii Mheshimiwa Dkt. Mpango amekiri kwamba pamoja na mengine tuliyoyafanya kumekuwa na changamoto. Nimeona kuna baadhi ya Wabunge wamefanya kama kebehi, lakini niseme tunapokubali changamoto au unapokiri changamoto siyo udhaifu ila ni uimara, kwa sababu changamoto ndizo zinazokujenga. Kwa hiyo wanaobeza naomba tu niseme wanakosea kwa sababu kukiri changamoto pia kunakuimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niendeleo hapo, kwa sisi watu tunaopakana na maziwa haya, nikiizungumzia Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, tunaona kabisa kupitia maziwa haya tunaweza tukatengeneza viwanda vikatusaidia kuwaajiri vijana wengi. Hata hivyo, lazima tukubali, lazima niishauri Serikali na Wizara husika; lazima tuwekeze katika Sekta hii ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto, hatuna vifaa imara vya kuvulia. Bado tuna changamoto vifaa tulivyonavyo haviwezi kutusaidia kuendesha viwanda hivi vya uvuvi. Kwa hiyo niombe sana, bado tuna kazi ya kufanya, lazima tuwekeze ili tuweze kupata matunda bora sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mipango hii ya maendeleo ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu. Niwashukuru pia wale wote ambao wameweza kutambua juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kueleza kwamba asilimia 75 mpaka 80 ya Watanzania wanaishi kijijini na ni maskini. Tushukuru Serikali kwa kutuingiza kwenye uchumi wa kati ila pia tuiombe iongeze fursa, kazi ya Serikali ni kuandaa mazingira mazuri ya biashara ili watu waweze kupata kipato na pato la Taifa liweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pia nimshukuru dada yangu, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, amezungumzia changamoto ya bei ya mbolea. Ni kweli; kwa mfano kule kwetu Ludewa mfuko mmoja wastani unauzwa kati ya 56,000 mpaka 65,000 na kwa ekari moja mkulima anatomia mifuko siyo chini ya minne ambapo mavuno yake anapata sanasana roba kumi. Sasa akija kuuza hizi roba kumi, roba moja shilingi 40,000, kwa hiyo anapata mapato ya shilingi 400,000 wakati amewekeza gharama zaidi ya shilingi 400,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie namna sasa, nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amekaa na wataalam wa kilimo na kuweka mikakati. Hii ni ishara njema na nimwombe yale ambayo ameahidi aweze kuyatekeleza kwa sababu Wabunge wengi humu tunatokea maeneo ambapo wananchi wetu ni wakulima na wanategemea hasa jembe la mkono. Kwa hiyo naamini atawatoa jembe la mkono wakulima wale ambao asilimia kubwa wako vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na vituo vya utafiti, lakini vituo hivi vijengewe uwezo zaidi ili viweze kutoa taarifa nzuri na taarifa hizi zisibaki kwenye makabrasha,

wawashirikishe wataalam wa kilimo kwenye halmashauri zetu, zinaweza kusaidia katika kuongeza tija. Vile vile kwenye ile mikoa yetu ambayo inajishughulisha na kilimo kungekuwa na vituo ambavyo vinafanya uchunguzi wa udongo, zile maabara. Kwa sababu mwananchi anaweza akawa anatomia mbolea ambayo saa nyingine haihitajiki kwenye udongo wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyokuwa kwenye Mkutano wa *RCC* Njombe, watu wa madini waliwasilisha taarifa kwamba Wilaya ya Ludewa ina leseni 104 za madini ambazo hazitumiki zimekuwa zikihuishwa tu. Kwa hiyo waliomba kwamba kwa kuwa eneo hili linaweza kutoa ajira nyingi kwa Watanzania na Wanamkoa wa Njombe na kanda nzima ile ya nyanda za juu; leseni hizi ziweze kufutwa, maeneo haya yagawiwe kwa wachimbaji wadogo ili waweze kuongeza kipato chao na kipato cha Taifa kiongezeke. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, aliahidi kwamba atalishughulikia na atafanya ziara Ludewa; nimshukuru sana. Wananchi wa Ludewa wanamsubiri kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wanaomba kwenye eneo la makaa ya mawe pale kuna leseni kubwa mbili ambazo zote zimeshikiliwa na Serikali. Sasa si halmashauri mapato pale ni hafifu sana, milioni 800 na sisi tulitamani Mheshimiwa Waziri wa Madini angetumegea kidogo halmashauri pale tuweze kuwekeza kwenye uchimbaji ili pato letu la halmashauri liinuke, tuweze kuhudumia wananchi. Tukihudumia vizuri wananchi maana yake watakuwa na kipato kizuri watafungua biashara na Serikali itapata mapato kupitia kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Sheria ya Kodi ya Mapato, *TRA*. Kuna kodi moja inaitwa *Capital Gain Tax*; mwananchi anavyonunua au kuuza ardhi hii kodi inatozwa kwa mujibu wa Sheria ya Mapato ya Mwaka 2004. Kodi hii siyo rafiki, wananchi wengi ambao wananunua ardhi wanashindwa kuhamisha umiliki wa viwanja vyao. Kwa hiyo naomba iangaliwe vizuri.



Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka na Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ili kuchangia leo Mpango wa Tatu. Kwanza kabisa nianze kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Msalala. Lakini pia leo nitachangia katika maeneo matatu; eneo la kwanza nitachangia eneo la kilimo, na eneo la pili nitachangia eneo la madini na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyofanya katika Taifa hili. Kila mmoja ni shahidi wa mambo ambayo kimsingi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ametufanyia sisi Watanzania. Tuna haja kubwa ya kumpongeza Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Msalala limegawanyika katika maeneo mawili; eneo la kwanza ni kilimo. Asilimia 50 ya jimbo langu ni kata ambazo kimsingi zinafanya shughuli za kilimo, lakini kumekuwa na tatizo katika suala zima la utoaji wa vibali ambacho kitawaruhusu wakulima hawa baada ya kupata mazao mengi waweze kusafirisha kwenda kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliowekwa na Wizara ya Kilimo ni kuhakikisha kwamba wakulima hawa wanaweza kuomba kibali kwa kutumia njia ya mtandao. Ni ukweli usiopingika kwamba katika maeneo yetu, hasa ukizingatia maeneo ya Kata za Mwaluguru na Mwanase, ni maeneo ambayo hayana mawasiliano. Nimwombe Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Waziri wa Kilimo waweze kuona namna gani wanakwenda kushirikiana na Waziri wa Mawasiliano ili kuweza kuhamisha mawasiliano ambayo yatawafanya basi sasa wananchi hawa, wakulima

hawa, waweze kupata huduma ya mtandao ili waweze ku-*apply* kibali hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe sasa Wizara iweze kubadilisha utaratibu huu wa wananchi kuomba kibali kwa kupitia njia ya mtandao, kwani tunaamini kuwa wananchi wengi hawawezi kuingia kwenye mtandao na kujaza taarifa za kuomba kibali hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kwa sasa kumeibuka tabia ya kwamba kila maeneo wanaweza kuanzisha mazao mbalimbali ikiwemo korosho na mengine. Niseme tu kwamba sisi wananchi wa Shinyanga ni wakulima wa zao la pamba, lakini kumeibuka tabia ya sasa hawa Maafisa Kilimo kuanza kutuletea mazao mapya. Niombe Waziri wa Kilimo yuko hapo, Naibu Waziri wa Kilimo yuko hapo, waone namna gani sasa wanaweza wakahakikisha kwamba wanatu-*support* ili tuweze kwenda kwenye kilimo cha pamba kwa kutupatia fedha na mitaji na matrekta yetu yaingie kwenye zao la kilimo cha pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la madini. Jimbo langu la Msalala ni jimbo ambalo kimsingi lina Mgodi mkubwa wa Bulyanhulu. Nimwombe Waziri wa Madini yuko hapo, Mheshimiwa Doto Biteko, kwanza niwapongeze kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuhakikisha ya kwamba wameweka makubaliano na Kampuni ya Twiga. Ni ukweli usiopingika kwamba wanasimamia vizuri shughuli hizi za madini na usimamiaji wa utoroshaji wa madini. Hata hivyo, nimwambie tu Mheshimiwa Waziri kwamba kampuni hii kwa sasa nadhani imeanza kuja na mfumo mwingine ambao kimsingi kama Taifa tunakosa mapato lakini kama halmashauri tunapoteza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hii imeanzisha kampuni mbili ambayo moja iko Marekani inaitwa *TSL*. Uwepo wa kampuni hii Marekani kama Taifa tunapoteza mapato. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kampuni hii ipo *USA* maana yake kazi kubwa ya kampuni hii ni kutangaza tenda tu na zabuni mbalimbali katika makampuni makubwa makubwa.

Kwa nini kampuni hii isweze kurudi hapa nchini, Makao Makuu yake yakawa Dar es Salaam ili kama nchi tuweze kupata mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Kampuni hii imeanzisha mtoto wa kampuni ambayo inaitwa *TSR Service*, iko Dar es Salaam. Uwepo wa Kampuni hii Dar es Salaam inatufanya Halmashauri kupoteza zaidi ya shilingi bilioni 20 fedha za *Service Levy*. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kushirikiana yeye na Waziri wa Viwanda waone ni namna gani sasa wanaweza kuzishauri kampuni hizi ziweze kuja kuwekeza na kuanzisha ofisi zao katika maeneo ya kazi hususan Bulyanhulu. Uwepo wa kampuni hii Dar es Salaam unasababisha ukosefu wa ajira kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Atashasta Nditiye, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava na Mheshimiwa Haji Amour Haji ajiandae. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Atashasta Nditiye, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava na Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Benardetha Mushashu ajiandae.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo kwenye Bunge letu Tukufu. Pia nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Muhambwe kwa kuniwezesha kurudi kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye kitu kimoja tu ambacho napenda nikichangie kama kuisaidia Serikali yetu katika kuinua kipato. Hivi karibuni kwenye hotuba hii ambayo mimi binafsi naiona ni nzuri sana, kumekuwa na maelezo mengi sana ya Waheshimiwa Wajumbe na Wabunge kwa ujumla ya kuelezea jinsi ambavyo hawaridhiki na fedha iliyotengwa kwa ajili ya *TARURA* na wakawa wanapendekeza kwamba sasa tuangalie uwezekano wa kuhakikisha kwamba tutachukua pesa kutoka *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri. Kwanza kabisa, hakuna kosa kubwa tutakalofanya kama tutakapojaribu kuondoa hiki kidogo ambacho wanacho *TANROADS* kwa njia yoyote ile. Isipokuwa kitu ambacho tunaweza kufanya ni kuhakikisha tunatafuta vyanzo vizuri na sahihi kwa ajili ya *TARURA*. Tunajua umuhimu wa *TARURA* kwa barabara zetu kuanzia vijijini mpaka barabara kuu na tunajua jinsi ambavyo wana-*struggle*, ukweli ni kwamba bajeti yao huwa ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nije tu na mpango na niutoe kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha auangalie kama utaweza kufaa. Mwaka 2020 kwenye kipindi kama hiki niliweza kuhudhuria kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti na nikaitoa kama *proposal*, ni jinsi gani tunaweza tukatumia sekta ya mawasiliano kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kutosha kwa ajili ya kuwasaidia *TARURA* kuweza kufanya shughuli zao kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hicho ambacho bado nasimamia kwenye wazo langu hilo, tuliwapendekeza watu wa Wizara ya Fedha kwamba tuongee na makampuni ya simu, tuweke tozo kidogo kabisa ambayo itawezesha

TARURA kupata fedha. Tukawapa pendekezo; na nitaomba mnisikilize kwa makini, tuliwaelekeza tukawaambia bwana, tukiweka senti 25 kwa kila *megabyte* moja; sasa hivi Watanzania waliosajiliwa kwa kutumia *line* za simu wako milioni 50; na kati ya watu milioni 50, watu milioni 24 imesomeka kwamba wanatumia mitandao ya *internet* kwa njia mbalimbali na shughuli mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema tuchukue tu *sample* ya watu milioni 10, tusichukue yote milioni 24, tuchukue watu milioni 10 ambao wanatumia *internet*, nikasema tuweke tozo ya senti 25, isifike hata shilingi moja, tuweke senti 25 kwa kila *megabyte* moja. Nikasema kwamba kwa *gigabyte* moja ambayo ni *megabyte* 1,000, tukiweka hapo kwa senti 25, tutakuwa tumechangia Serikali shilingi 250 kwa gigabyte moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda mbali zaidi na nitaleta hiki kitu kwa maandishi kwa sababu najua itaisaidia Serikali. Kwanza kabisa, niwahakikishie Serikali, tusiwe waoga, hayo makampuni ya simu yamekuwa na ushirikiano mzuri sana na Serikali na yamekuwa yanachangia sana kwenye Serikali na hawawezi ku-*complain*. Isitoshe hakuna bei elekezi ya mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine katika kutoa huduma kwa wateja wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitumia watu milioni 10 ambapo kila mmoja anatoa shilingi 250, *let's say* kwa wiki moja, tuchukulie tu kwamba kwa wiki moja mtu atatumia *gigabyte* moja, tutakuwa tumetengeneza shilingi bilioni 2.5. Uki-*manipulate* hiyo hesabu kwa muda wa mwezi ni shilingi bilioni 10 na kwa mwaka mzima ni shilingi bilioni 120 kwa bajeti ya shilingi bilioni 273 ya TARURA tutakuwa tumewaongezea kiasi cha pesa...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa kengele imegonga lakini tufafanulie jambo moja. Hiyo senti 25 inalipa kampuni

kwa ile *gigabyte* iliyoniuzia mimi au unapendekeza nikatwe mimi halafu kampuni ya simu ikusaidie kukusanya?

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mteja ndiyo akatwe senti 25 kwa *megabyte* moja halafu zile kampuni wazipeleke Serikalini kama fedha ya Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Benardetha Mushashu ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nitumie nafasi hii kukishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi na wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini kwa kura nyingi na za heshima walizotoa kwa chama chetu na kuniwezesha nami kuwa mwakilishi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma vizuri mapendekezo ya Mpango, nimesoma vizuri mpango huu, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa na hatua kubwa ambayo tumepiga mpaka sasa. Ila nilipokuwa nasoma Mapendekezo ya Mpango huu wa Awamu ya Tatu kwenye ukurasa wa 87 nimekutana na vipaumbele pale viko vitano. Ukisoma kuanzia kipaumbele cha kwanza, cha pili na cha tatu, huoni namna ambavyo unaweza ukaikwepa sekta ya kilimo kwenye kuendeleza na kukuza uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri sana Serikali, kwenye suala la kilimo, tunayo mambo mengi sana ya kufanya na mengi yameshazungumzwa, mimi naomba nizungumzie sana eneo la soko. Ni lazima Serikali ijitahidi kuweka uhakika wa masoko kwa wakulima wetu wanaolima

kwenye nchi yetu hii. Tukiweka uhakika wa masoko tutasaidia viwanda vyetu, tutatengeneza ajira, tutaongeza pato kwa wale wakulima wanaolima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa tunamwuliza Waziri Mkuu kuhusu mkakati tulionao kwenye mazao ya kimkakati, nikatoa mfano wa zao la mkonge. Wananchi wameitikia na wanalima sana, lakini tusipokuwa na uhakika wa soko kwa ajili ya mazao haya, mwisho wa siku wananchi watakuja kuishia kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya njia ya kuweka uhakika wa soko ni kutengeneza viwanda na kushawishi wawekezaji kuwekeza kwenye sekta ya viwanda. Tunavyo viwanda kwa mfano kwenye zao la mkonge, tulikuwa na viwanda vya magunia, sasa hivi havifanyi kazi vizuri. Asubuhi kuna mtu amezungumza hapa kwamba wale wawekezaji ikiwezekana wanyang'anywe lakini ni lazima tujiulize hivi viwanda vya magunia vilikwama wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya magunia ni makubwa sana, lakini uzalishaji wa magunia ni mdogo, kwa nini? Ni gharama za uzalishaji. Siyo hivyo tu, pia magunia yetu yanakumbana na ushindani kutoka kwenye magunia yanayozalishwa kwa kutumia mazao mengine na bidhaa nyingine kama *jute*. Ukiangalia India na Bangladesh, wao wana *subsidy* kwenye *jute* na wanajitahidi sana kuwekea mfumo mzuri wa kununua mazao yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *East Africa Community*, Sheria za Ushuru wa Forodha zinatoa nafuu ya kodi kwa bidhaa ambazo zinaingia kwa ajili ya kuchukua mazao na kutoa bidhaa na kuzipeleka nje kwa ajili ya ku-*export*. Haya yote ukiangalia yanafanya magunia ya *jute* yanakuwa na bei rahisi wakati magunia yanayozalishwa na mkonge yanakuwa na bei kubwa. Ukienda kwenye ushindani hatuwezi kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo linguine, tumejiwekea malengo, tumepiga hatua kidogo kwenye

umwagiliaji na tumejiwekea malengo mpaka 2025 tufike hekta 1,200,000. Naiomba Serikali, lazima tuangalie miradi mikubwa ya umwagiliaji itakayotusaidia kuweza kuhudumia eneo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo tulikuwa nao Tanga, Bwawa la Mkomazi, mradi mmoja tu una uwezo wa kuhudumia hekta zaidi ya 6,000, lakini kwa zaidi ya miaka 10 wananchi wamekaa na matumaini wanasubiria miradi hiyo haitekelezwi. Naomba tuweke nguvu kwenye maeneo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la miundombinu. Kilimo kinafanyika vijijini, lakini miundombinu ni mibovu sana. Leo tunasema tuongeze uzalishaji kwa kuongeza maeneo ya kulima, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Waziri wa Kilimo wanajua, kwenye chai peke yake kwa mwaka, zaidi ya kilo milioni nne tunazipoteza, zinachelewa kufika kiwandani kwa sababu ya miundombinu na zinapotea. Thamani yake ni karibu shilingi bilioni 2.8 kwa sababu ya miundombinu. Naungana na Mheshimiwa Nditiye, tunahitaji kuwa na nguvu na mkakati wa ziada kwenye suala la miundombinu, kutafuta fedha kuongezea *TARURA* ili wananchi wetu wapate uhakika wa kupeleka mazao kwenye masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Benardetha Mushashu na Mheshimiwa Jackson Kiswaga Jackson ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Pangawe, nipo hapa kwa ajili ya kuchangia Mpango wa Taifa wa mwaka 2020/2021 pamoja na Mipango yote miwili.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nami sina budi kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasilisha Mpango huu ambao ulikuja na *theme* ya uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Sasa mpango huu kwa kweli nauunga mkono na kwa kweli nasema kwamba jitihada kubwa zimefanyika katika Serikali hii ya Muungano na mambo mengi ambayo nimeyaona katika Mpango uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wowote ule wa dunia kitu kikubwa ambacho unaangalia ni suala la amani. Amani yetu tuliyokuwa nayo katika nchi yetu ya Tanzania inatosheleza kuweza kufanya uchumi wa aina yoyote. Bahati nzuri katika nchi yetu ya Tanzania, kwa mujibu wa jinsi tulivyo katika maumbile yetu, maana yake tuna uwezo wa kufanya kitu chochote. Tukija katika suala la elimu, tuna uwezo wa kuwasomesha vijana wetu na kuweza kufikia katika hatua kubwa sana ya kimaendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu nilichokuja nacho kwa pamoja katika ushirikishwaji wa nchi mbili kwa pamoja ni suala la utalii. Bahati nzuri nchi yetu ya Tanzania ikiwemo Tanzania Bara pamoja na Visiwani ina kitu ambacho ni cha kimaumbile ambacho tukija katika suala la kiutalii, tuna uwezo wa kuziunganisha nchi hizi mbili zote tukasema kwamba tuwe na utalii wa pamoja ambao ni kwa maendeleo ya nchi zote mbili. Kwa sababu kwa maumbile ya nchi yetu, kwa upande wa Bara tuna mbuga ambazo tunaweza tukazitangaza kwa pamoja na zikaleta matunda kwa ajili ya maendeleo ya watu wote. Kwa upande wa visiwani kule, tuna utalii unaotokana na fukwe pamoja na bahari tuliyokua nayo, tukizishirikisha nchi hizi, maana yake kwa Tanzania tutaleta uchumi ambao ni endelevu na mkubwa sana. Vilevile kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeunga mkono ile azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ule uchumi wa bluu ambapo ndiyo *theme* ambayo kwa sasa hivi inazungumzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwamba kuna vitu vitakuwa vinaonekana kwamba siyo shirikishi, lakini

kimaumbile yake na kwa mujibu wa nchi yetu ilivyo, hivi ni vitu ambavyo ni shirikishi. Kama tutaweza kuunganisha utalii wa Tanzania ukawa ni utalii tunaoutangaza kwa pamoja, nadhani tunaweza tukafanya kitu ambacho ni kikubwa sana kwa mujibu wa maumbile ya nchi yetu ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa rai katika Mpango huu, pamoja na kwamba yamezungumzwa mengi; kulizungumzwa suala la utalii hasa kwa upande wa vivutio vya mbuga, ila mimi napenda zaidi tukauzungumzia katika utalii wa fukwe, tukaipa nguvu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuichanganya ili tuwe na utalii wa pamoja. Pato litakaloweza kupatikana maana yake litaweza kuleta tija kwa nchi zetu zote mbili. Hii itaweza kufanikisha ule umoja wetu ambao tumekuwa nao katika nchi zetu kuweza kuwa shirikishi hasa katika maendeleo ya pamoja. Tanzania ni moja, watu wa Tanzania ni wamoja. Hiki siyo kitu cha ubishi. Maendeleo yoyote yale ambayo yataweza kufanyika kwa upande wa Bara, ikiwa ni kilimo maana yake faida itakuwa ni ya kwetu sote (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono Mpango wa Maendeleo, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Shukurani sana. Mheshimiwa Benardetha Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Kiswaga Jackson na Mheshimiwa Josephat Kandege ajiandae.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu anavyoendelea kutulinda na kutubariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kagera walionichagua kwa kura nyingi. Nakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi kwa kuiteua na leo hii ni Mbunge katika Bunge la Kumi na Mbili. Ahadi yangu kwao ni kwamba nitaendelea kuwatumikia wananchi wote kwa nguvu zangu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ulioletwa ni mzuri, tunachangia ili tuboreshe; na kwa sababu ya muda nitajikita kwenye eneo moja la kilimo. Lengo moja la Mpango huu ni kuchochea maendeleo ya watu. Kama tunataka kuchochea maendeleo ya watu, basi inabidi tuwekeze nguvu nyingi katika maeneo ambayo yana watu wengi na katika Tanzania tuna maana ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Hatuwezi kupata maendeleo yanayotarajiwa kama tutaendelea kulima kwa jembe la mkono na kwa kutegemea mvua, ambacho ni kilimo cha kujikimu inabidi sasa twende kwenye kilimo cha biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza, ili tuweze kunufaika na Mpango huu, kwanza, kila mkoa uhakikishe kwamba unatenga maeneo makubwa kwa ajili ya kilimo, watafutwe wawekezaji wa nje na ndani waweze kuwekeza kwenye mashamba makubwa ya kilimo. Vilevile wananchi wawezeshwe kupata mitaji kwa bei nafuu. Kwa maana kama wanapata mikopo kutoka benki, basi riba isizidi asilimia 10, iwe chini ya asilimia 10 kusudi waweze kuzitumia hizo hela kutafuta zana za kilimo bora na waweze kulima kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta zana nyingine ni ghali sana, kwa mfano, matrekta makubwa, *excavators*, *vesta*, *weeder* na vitu kama hivyo. Ingekuwa ni vizuri kila Halmashauri ikawa na mfuko wakanunua vifaa hivyo; vikundi vidogo vidogo na watu binafsi wakawa wanakodishwa kutoka kwenye Halmashauri, nao wakaweza kulima kilimo kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufanya kilimo kikubwa inabidi vilevile tuwe na kilimo cha umwagiliaji. Kuna *schemes* mbalimbali humu katika Tanzania ambazo nyingine zilizhakufa, tuzifufue lakini vilevile tunaweza kuanzisha nyingine mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Vituo vya Utafiti kama *TARI*, *TACRI* na vile vya usambazaji mbolea, lazima watusaidie kuhakikisha kwamba tunakuwa na mbegu bora. Kwa sababu

hata ukilima shamba kubwa namna gani, kama mbegu uliyokuwanayo siyo bora, huwezi kupata tija yoyote. Kwa hiyo, tunaomba wapewe bajeti ya kutosha kusudi waweze kuzalisha mbegu zilizo bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafute wawekezaji, tuwashawishi, tuwatengenezee mazingira mazuri waweze kuwekeza kwenye viwanda vya kuongeza thamani ili kusudi yule mkulima wa Kahawa kutoka Mkoa wa Kagera asiuze kahawa ghafi; akaange, apaki, auze au asage auze; mkulima wa pamba atengeneze nyuzi auze, au atengeneze nguo ndiyo zizuzwe. Kwa namna hiyo, tutaweza kumfaidisha mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna tatizo kubwa la soko la mazao yetu. Naomba idara za Serikali ambazo zinahusika katika kutafuta masoko, waende nchi za nje, waingie mikataba, watu walime wakijua kwamba soko liko wapi. Natoa mfano wa Botswana. Wao wamefaidika sana na mifugo yao kwa sababu hata kabla hujaanza kufuga nchi inaaenda kuingia mikataba na nchi nyingine, unajua kwamba unafuga kwa *standards* zipi, ukisha-*produce* yale mazao inakuwa ni rahisi kuuza kwa sababu unajua unalenga soko gani. Isije ikawa kama ile *story* ya mbaazi ambapo watu walilima lakini wakakosa masoko.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kwa ajili ya...

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Ooh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Tarimba Abbas ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata nafasi hii kwa ajili ya kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja na Miaka mitano. Kwa kuwa mimi ni mfuasi sana wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli, kwa uzalendo wake napenda niendeleo kumpongeza kwa kazi nzuri anayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Watanzania na wenzangu waliomo humu kwamba baba yetu huyu amefanya kazi kubwa. Wakati anaingia mwaka 2015 nilimsikia akisema ninyi *TANESCO* acheni mchezo, nafahamu huu mgao wa umeme mnafanya biashara. Mnafungulia maji ili watu waweze kuuza majenereta halafu wauze mafuta. Alivyokemea, kweli sisi tuliokuwa tunaishi Mbeya na Dar es Salaam, taabu ya umeme tuliyokuwa tunapata na kelele za majenereta ziliisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuendeleo kumtia moyo. Hao wanaombeza, waendeleo kubeza, lakini kwa sababu hata Mungu aliyetuumba wengine tunamkataa, tunampenda shetani. Kwa hiyo, ni jambo la kawaida. Kwa hiyo, namtia moyo aendeleo hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mpenzi wa kilimo, siku ile kwenye hoja nilizungumza kidogo sikumaliza. Wakati tukiwa kwenye mpango kazi wa Wizara, mimi pia kama Mjumbe wa Kamati tulizungumza baadhi ya mambo. Moja ambalo linanigusa sana ni kuona Serikali sasa inakwenda kuwekeza kwenye suala la maabara za utafiti wa udongo. Ni muhimu sana. Wajerumani walifanya *portioning* ya nchi hii, wakasema hapa tutalima pareto, hapa tutalima kahawa, kwa sababu walipima udongo katika nchi hii na wakaweza kutoa mawazo yao kwamba tukilima hiki hapa tutafanikiwa. Najua ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba tunainua kilimo, lakini naona kwamba tuwekeze kwenye maabara za utafiti

wa udongo, ni muhimu sana kwa sababu tutatoa mwongozo na tutaweza kuelekeza watu walime namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia upande wa mifugo, tumekuwa tuna shida ya chanjo. Chanjo nyingi ambazo tunazileta nchini zinatengenezwa kutoka katika nchi mbalimbali na hizi chanjo wanasema kwamba zinatibu magonjwa mengi na magonjwa mengine ambayo zinatibu hapa Tanzania hayapo. Sasa ningependa kuona Serikali inashirikiana na hiki Kiwanda cha *Health Bioscience* kuona kwamba kinakamilika kwa haraka, kama kuna vikwazo vyovyote vya kikodi au vya kivibali, basi viondolewe ili kiwanda hiki kianze kutengeneza chanjo hapa hapa nchini kwa sababu tutatengeneza chanjo zinazolingana na mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, tutaweza sasa kuzalisha mazao ya wanyama ambayo tunaweza kuyauza hata Nchi za Ulaya pamoja na Nchi za *SADC*, kwa sasa tunashindwa kwa sababu ya ubora wa mazao yetu. Kama hizi chanjo tutazalisha hapa, tutadhibiti magonjwa na tutaweza kuongeza tija kwenye mifugo. Najua muda utafika, baba yetu akishamaliza hii miradi ya umeme tutakwenda kumwomba fedha za kimkakati ili tuwekeze kwenye utafiti wa chanjo, kwenye maabara, kwenye mifugo pamoja na mazao, najua haya mambo yatakwenda vizuri, kwa sababu haya mambo ni ya kupanga tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tumesema kwamba utalii, *ecology* kule Arusha inaharibika. Sasa naona sasa ni wakati muafaka tuweze kufungua milango ya utalii wa Nyanda za Juu Kusini. Baba yetu Magufuli pale Iringa ametuletea pesa, tutajenga Kituo cha Utalii (*Tourism Hub*). Sasa ili haya mambo yaende vizuri tungehakikisha kwamba hizi barabara, kwa mfano ya Ruaha, ya kutoka Udzungwa kuja Iringa Mjini pale, tutengeneze *ring fence* tunavyotoka Mikumi tunaingia Udzungwa, tunaingia Kalenga kwenye Jimbo langu tunakwenda Ruaha Mbuyuni. Kwa hiyo haya mambo yatakwenda vizuri tukifanya namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la umeme, kaka yangu Mheshimiwa Muhongo alisema kwamba tuwe na vyanzo vingi vya umeme. Sasa kaka yangu pale Mheshimiwa Kalemani tuliongea juu ya hawa *RP Global* ambao wanataka kuleta umeme kwenye jimbo langu umeme wa *solar*. Namshukuru amelipokea, nimwombe watakavyokwenda kumwona...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Abbas na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ili niweze kuwa sehemu ya wachangiaji katika Rasimu ya Mpango. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya, maajabu ambayo nimetendewa kati ya Wabunge ambao 28 waliopita bila kupingwa ni pamoja na mimi, nina kila sababu ya kuwashukuru wannachi wa Jimbo la Kalambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni sehemu ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa hiyo nilitoa mchango wa kutosha. Hata hivyo, leo nitajielekeza katika masuala mawili; la kwanza itakuwa upande wa kilimo na la pili kama muda utatosha litakuwa upande wa *local contents*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kimekuwa sio cha kuvutia kwa sababu hakuna *incentive* ya kutosha ambayo imewekezwa ili mwananchi ambaye analima aone tija katika kilimo. Nawe ni shujaa unajua kabisa yaliyotokea miaka ya nyuma, leo nikipita nauliza hivi yako wapi mafuta yaliyokuwa yanatokana na karanga? Siyaoni, yako wapi mafuta ya kula

yanayotokana na pamba? Siyaoni. Iko wapi *Tanbond*? Siioni, iko wapi *Super Ghee* siioni, iko wapi samli iliyoboreshwa, siioni. Yako wapi mafuta ambayo yanatokana na mahindi ambayo yamezalishwa Tanzania? Sioni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufike wakati sasa ili wananchi wanaotoka Rukwa, Ruvuma, Iringa na maeneo mengine ambayo wanazalisha mahindi wasipate tabu ya kutafuta soko, wanafanya kazi kubwa sana katika kulima, si wajibu wao kutafuta soko. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba inaweka mazingira yaliyo bora ili mkulima kazi yake iwe ni kulima mbegu iliyokuwa bora na soko litafutwe na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutafanyaje? Kwa kuhakikisha kwamba sio kwamba mahindi yatumike kwa ajili ya chakula cha binadamu peke yake, tu-*extract* kutoka kwenye mahindi tupate mafuta inasemekana kwamba ni mafuta yaliyo bora na tukienda *supermarket* unayakuta. Mafuta haya yanapatikana wapi? Kama iko mbegu mahsus ni wajibu wa Serikali kwa kupitia *research and development* kutuletea mbegu hizi ili wakulima wetu waweze kufaidika na kilimo hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mbali Zaidi, sasa hivi bei ya mafuta ya kula imepanda kweli kweli. Zaidi ya dola milioni 126 tunatumia kama nchi kwa ajili ya kuagiza mafuta. Tafsiri yake ni kwamba ajira tunawapelekea wengine na sisi tunabaki kuwa soko. Ifike wakati wa kuwekeza vya kutosha ili mafuta ya kula ambayo yanachukua mzungu mkubwa kwa Taifa tuweze kupeleka kwa watu wetu ili kilimo kiwe na tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la *local content*. Ukitafuta namna gani tunamsaidia Mtanzania, mzalendo ili aone fahari ya kuzaliwa Tanzania tofauti na mwingine ambaye hakuzaliwa Tanzania, unatafuta kwa kurunzi ndiyo unaenda kuziona hizo fursa. Ifike wakati kwa makusudi mazima kama ambavyo wenzetu wamefanya kama Afrika ya Kusini, mwananchi wa Afrika Kusini anajua



haki zake katika kuwekeza na fursa zipi ambazo anatakiwa kuzipata. Ni wakati muafaka tusione aibu ya kumpendelea Mtanzania ajivunie na fursa za kuwa Mtanzania na zionekane wazi. Hizi sheria ambazo zipo unaenda kwenye madini ndiyo unakutana nayo, sijui unaenda wapi zote zikusanywe kwa pamoja ili ionekane dhahiri kwa Mtanzania fursa alizonazo na upendeleo wa Dhahiri, tusione aibu kuwapendelea Watanzania. Wako wa nchi za jirani ambao wao wamekuwa na wivu na watu wao. Ni wakati muafaka, tusichelewe muda ndiyo sasa hivi, tuhakikishe kwamba tunawalinda Watanzania kwa kuweka vivutio vya wazi kabisa bila hata kuona aibu katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda upande wa ujenzi, kazi kubwa sana imefanyika katika ujenzi wa miundombinu, lakini ni watu gani ambao wamejenga hiyo miundombinu na hiyo fedha ambayo wamepata wameenda kuwekeza wapi, utakuta kwamba inaenda kwa wenzetu. Ni wakati muafaka kuhakikisha kwamba tunawasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Nimepata nafasi nzuri sana ya kuupitia Mpango huu. Nimeuona, tumeujadili, nasema ni Mpango mzuri ambao Serikali imekuja nao, lakini naiomba Serikali iweke *room for improvement*. Haya maoni ambayo yanatolewa yote ni maoni mazuri, wayachukue, isiwe kama ni taratibu zile nyingine kwamba tunazungumza lakini bado wanakuja na Mpango ule ule, mapendekezo yale yale, hilo haitakuwa jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najikita zaidi katika *private sector*. Ningependa sana huu Mpango uje waziwazi kwenye *private sector*, tuwe na *vibrant private sector*, hakuna uchumi unaoweza ukaendelea bila ya kuwa na *private sector* ambayo ina nguvu, inayochochea *exports*, lakini vile vile inachochea *domestic spending*, bila mambo haya tutakuwa tunajidanganya. Tutakuwa tunazungumza lakini tunajifanya kama tunasahau kama *private sector* ni mbia mkubwa sana wa maendeleo katika nchi yetu. Tumeangalia na *figure* zimetolewa na Wizara. Tuchukue tu mfano wa ule Mpango ambao umemalizika 2021. *Contribution ya private sector* ilikuwa inatarajiwa trilioni 48 karibu asilimia 45 ya kile kinachotarajiwa. Huyu si mtu wa kawaida. Huyu ni mbia ambaye lazima tuhakikishe tunakuwa nae na tunamuamini, *private sector* lazima iaminawe. Tusitengeneze *private sector* ambayo hatma yake tunapeleka *wrong waives, wrong information or wrong message* kwa *investors* nje kwamba kufanya kazi au biashara Tanzania ni jambo gumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni wazi, hebu angalia hawa wataalam wa *World Bank*, kuna huyu mtaalam anaitwa Simeon Diankov na Gerald Paul, Wachumi wa *World Bank* hawa walivyotengeneza ile *ease of doing business index*, Tanzania katika kuangaliwa, tuko watu wa 141, tumewekwa kama *medium*. Sasa jamani tunashindwa, *Rwanda is very easy to do business*, Rwanda jamani? Kitu gani kinatufanya *Rwanda* wao iwe ni *easy to do business*, sisi iwe ni *medium*, basi hata *Zambia*? *Zambia* nao wanafanya vizuri, wako *easy*, Kenya wako *easy*, sisi tunafunga wapi kiasi kwamba kwetu sisi ionekane tuko katikati, tunachotafuta ni nini? Tunatafuta *industry ya private* iwe inapewa nafasi zake. Sasa hivi iko *suffocated, it is a fact*, nimepata bahati ya kufanya kazi Serikalini, nimefanya kazi katika *Private Sector*, sasa hivi na mimi eti nami ni mwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sikiliza, kampuni moja inazungukwa na *regulators* si chini ya sita au saba. Huyu anamuuliza hiki, yule anamuuliza hiki, yule anamuuliza hiki. Hajui aende wapi, *who is the core regulator*, aende wapi. Akipata matatizo, akiwa *aggrieved* huyu mtu anapata shida

kubwa sana. Kampuni zinapata shida kubwa sana na haya ambayo yalikuwa yakizungumzwa kwamba *business* zinafungwa, naomba Serikali iangalie. Haiwezekani kampuni moja itaangaliwa na *TRA, BOT, TCRA, OSHA, Fair Competition and Filling Company*, hiyo ni mfano wa kwenye *betting*, huko usifikiri kuna *Gaming Board of Tanzania* peke yake, hawa ninaowatajia wako nyuma kila siku wanagonga milango. *How can you do business?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachohitaji ni kuona kwamba mtu ambaye anafanya *business* Tanzania asababisha mwingine aliye nje avutike kuja Tanzania. Kwa kufanya hivyo tutapata kodi nyingi, tutaajiri watu wengi, lakini vile vile tutaondoa manung'uniko. Leo hii mtu akiwa *aggrieved* anakwenda wapi? Kwa nini tusiwe na *regulatory ombudsman*? Wafanyabiashara hawataki kwenda Mahakamani kushindana na Serikali. Katika vitu ambavyo wafanyabiashara hataki ni ugomvi na Serikali, lakini angekuwepo mtu hapo kama vile wa *tax ombudsman* hata *regulatory ombudsman* amekuwa *aggrieved* na chombo fulani cha Serikali huyu bwana anakwenda kwa *ombudsman*, anakwenda pale anazungumza mambo yake yanawekwa sawa, mambo yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea na utaratibu tulionao sasa hivi, tuna *suffocate private sector* na *private sector* kama nilivyosema awali ni eneo moja ambalo ni mbia mkubwa sana wa biashara, mbia mkubwa wa maendeleo na ni maeneo ambayo tunahitaji kuyaangalia kwa nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Mungu atubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela na Mheshimiwa Issa Mtemvu ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia

Mpango wa Maendeleo awamu ya tatu na Mpango wa Mwaka mmoja. Nitaanza kwa kuchangia kuhusu kukuza uchumi wa nchi pamoja na pato la nchi na hasa kukuza uchumi wa viwanda. Nikianza kuchangia kwenye uchumi wa viwanda siwezi nikasema viwanda vitakua bila ya kilimo, uvuvi, ufugaji, maji pamoja na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia zaidi ya 66 ya wananchi wamejikita kwenye kilimo. Kwa hiyo, lazima tuangalie kwa undani kuhusu kilimo ndiyo tutaweza kukuza pato la Taifa na pato la mwananchi yeye mwenyewe mfukoni mwake. Kwa hiyo jambo la muhimu sana hapa la kuangalia ni kuhusu kilimo kiwe rafiki, kiwe cha kisasa, kilimo kiweze kuvutia kwa wananchi na hasa kwa vijana na kiwe kilimo cha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kuwa Mawaziri wa Kilimo, Uvuvi pamoja na Mifugo, wanafanya vizuri sana. Pamoja na mikakati iliyowekwa, inabidi tuweze kutimilika vizuri sana. Kwa upande wa vijana wanapata shida, lazima tuone jinsi ya kuwavutia vijana na watu wazima, wote waone kuwa kilimo ni rafiki ili kila mmoja avutiwe kuingia kwenye kilimo. Tufanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza tuangalie zana za kilimo. Nakumbuka zamani yalikuwepo matrekta ya vijiji ambayo yalikuwa yanasaidia wananchi kulima kwenye mashamba yao. Kwa hiyo, kama hiyo inawezekana naamini hata vijana wanaotoka vyuo vikuu wanaweza wakaingia kwenye kilimo, hata vijana wanaomaliza VETA, hata vijana ambao hawajasoma, wote wanaweza kuingia kwenye kilimo kwa sababu hawatatumia nguvu, watatumia zana za kilimo ambazo zinapendekezwa kama matrekta na kadhalika ili kusudi tuepukane na jembe la mkono ambalo linatoa jasho kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linavutia kwa vijana hasa kuwekeza kwenye kilimo waweze kukopesheka na watakopeshekaje? Tuweze kupata wawekezaji binafsi na hasa kilimo cha mkataba. Kilimo cha

mkataba ni kizuri sana kwa sababu hicho kilimo wataweza kulima na baada ya kuvuna na kuuza wataweza kukata zile hela ambazo watakuwa wameingia pamoja na mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu sana kwa hawa vijana pamoja na kilimo kuwa rafiki na kukibadilisha kilimo lazima tuwe na mbegu bora. Tuwe na mbegu za mafuta, ni kweli kila mmoja sasa hivi anasema bei ya mafuta ni ghali. Unajuliza kwa nini, Tanzania tuna ardhi nzuri, tuna wasomi wazuri, tuna kila kitu kwa nini iwe hivyo? Kwa hiyo tuangalie hata michikichi hiyo sio lazima izalishwe Kigoma peke yake, hata Morogoro tunazalisha mchikichi, hata Kagera wanaweza wakalima mchikichi, hata Mbeya hata Kilimanjaro. Kwa hiyo ni kiasi cha kuweka uzito kuona tutafanyaje tuweze kuondokana na umaskini kwa kupitia kilimo hasa kwa kuangalia pamoja na masoko. Kabla hujaanza zao uweze ku-*focus* kwenye soko, ukiwa na soko bila shaka utaweza kuzalisha kwa wingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la viwanda, lazima tuweze kuwa na ufugaji. Kwenye ufugaji tufuge mifugo ambayo ni ya kisasa, sio bora kufuga. Ni kufuga kwa kisasa na kuzalisha kwa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye uvuvi, tuwe na *blue economy*, tuone kuwa tunafanyaje kwenye uvuvi kusudi tuweze kuwa na viwanda ili wananchi wote waweze na wenyewe kunufaika kwenye mambo ya kilimo, uvuvi, mifugo na kwenye ufugaji wa nyuki pia, asali ipo lakini hatuna soko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi, lakini naamini imeeleweka. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe; lakini pia niishukuru familia yangu; tatu nishukuru wananchi wa Jimbo langu la Lulindi walioniamini; nne nishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa kuniamini kuwa naweza kufanya hizi kazi kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nataka nizungumzie suala la *performance*; nataka nijaribu kuweka wazi katika jambo hili. Wakati unapotaka kuchunguza *performance* ya mtu au kitu, cha msingi sana kinachohitajika kutumika pale sio *percentage term*, unatakiwa utumie *an absolute term*, maana yangu ni nini? Ni kwamba ukichukua bilioni moja ukazidisha kwa asilimia 10 unapata milioni 100, lakini ukichukua milioni 100 ukazidisha kwa asilimia 27 au asilimia 30 unapata milioni 30. Kwa hiyo, ukisema kwamba eti kwa sababu umetumia *percentage* kubwa wewe ume-*perform*, huo ni upotoshaji mkubwa, kwa hiyo nataka nieleweke hapo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende katika utendaji wa Serikali. Hakuna hata mtu mmoja ambaye anasema kwa dhati kabisa kwamba, eti Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hakufanya vizuri kwa dhati kutoka rohoni kwake, atakuwa anatania tu. Kiuhalisia yaliyofanywa ni mengi sana, hatuwezi kuyamaliza hata tukisimulia wiki nzima maajabu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kwamba suala la maendeleo ni mtambuka. Tunahitaji kuhusisha vitu vingi na sekta mbalimbali kwa ajili ya kutengeneza hayo maendeleo. Barabara za Dar-es-Salaam za mwendokasi, ni jambo zuri sana, lakini nashauri barabara hizi zizingatie pia na ukuaji wa miji ile. Nashauri kwamba barabara hizi ikiwezekana zifike hata Mkuranga kwa ajili ya

ku-*accommodate* watu wanaoishi maeneo kama ya Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mradi wa bandari Mtwara umetumia pesa nyingi sana, takribani shilingi bilioni 157. Naomba mradi huu uunganishwe haraka sana na reli ya *Standard Gauge* ambayo itafika kwenye miradi mikakati ya Mchuchuma na Liganga. Tusiendeleo tu kuongea mdomoni, tufanye kwa vitendo kama kweli tunataka maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine mradi huu pia uunganishwe na barabara zote za kimkakati zikiwepo barabara zile za ulinzi. Kwa mfano, barabara inayotoka Mtwara – Mtawanya - Mpilipili – Chikoropola - Nanyumbu. Barabara hii nafikiri ni muhimu sana kwa ku-*boost* maendeleo ya watu wa Kusini na viwanda vya Kusini, hasa kiwanda cha korosho ambacho nakitegemea mimi kama mmoja wa wahamasishaji kipatikane kule lakini kiwe ni kiwanda kikubwa kabisa cha kushawishi watu wengi sana kuuza pale, kusudi tuweze kupata bei nzuri. Hali ilivyo sasa hivi hatuwezi kupata bei nzuri kwa sababu tunauza *raw material*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda *EPZ* iwe ndio msingi wa maendeleo kwa sababu ndiyo inaweza ikasababisha watu wengine wakawekeza kikamilifu. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengi, lakini niseme naunga mkono hoja kwa sababu yaliyo ndani ya Mpango ni mazuri. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Issa Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Mussa Sima ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Mpango huu wa bajeti wa miaka mitano 2021/2022 mpaka 2025/2026 pamoja na mwaka mmoja wa 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vipaumbele vyote ambavyo vimeainishwa, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake kwa ujumla kwa maana nimeshiriki katika kuuona Mpango ulivyowasilishwa kwenye Kamati, kama Mjumbe wa Kamati na nimechangia kwa kina. Kwa sasa nijielekeze katika maeneo mawili tu. Eneo la kwanza ni *master plan* ya Dar es Salaam kwa ujumla, lakini la pili, jinsi gani tutatumia usimamizi na ufuatiliaji katika miradi, hasa ya kimkakati na mingine kwa maana ya *monitoring and evaluation* katika miradi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wachache wa Dar es Salaam wamezungumza kwa ujumla juu ya *master plan* ya Dar es Salaam na hasa katika maeneo ya miundombinu kama mafuriko na upimaji wa ardhi. Nipongeze sana huu mpango wenyewe, katika *page* ya 97 wameeleza juu ya mkakati wa kuboresha maeneo hayo ya mabonde, lakini kuboresha pia maeneo ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwa Dar es Salaam ambayo tuna *population* yenye makadirio takribani milioni sita kwa kufikia mwaka 2020, lakini tukiwa tunajua hata *tax collection* haipungui asilimia 80 na hata mchango katika *GDP* Dar es Salaam inachangia zaidi ya asilimia 75. Kwa msingi huo, tunataka kuona Dar es Salaam inakuwa kama sehemu ya kimkakati sana katika kuongeza mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kutafuta fedha siyo kuangalia fedha zinakwenda wapi, tutakuja kwenye bajeti. Hapa mimi naona kama mkakati ukiwekwa vizuri Dar es Salaam inafaa sana kwenda kwenye *housing building strategy*. Wakati niko Diwani Manispaa ya Kinondoni tulikuwa tuna mpango wa kuondoa nyumba kongwe za Magomeni, takribani nyumba 605, ni mpango wa zaidi ya miaka 8 kuanzia 2012, leo nyumba zimejengwa. Naona mpango huo



ungeendelea Dar es Salaam; tuna maeneo kama Tandale, Magomeni, Manzese, tukafanye mipango ya kujenga nyumba ambazo zitatusaidia kuinua uchumi wa watu, lakini tutaweza kuwa ni sehemu ya mapato sasa kwa jinsi ambavyo tutaingia makubaliano na wale wakazi ambao wana ardhi za msingi au ardhi zile ambazo ni za kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili kwa haraka ni upimaji wa ardhi. Mpango umesema vizuri una nia ya kupima ardhi nchi nzima, sasa waende kweli kimkakati wapime ardhi. Waipime ardhi ya Dar es Salaam kutokana na *population* niliyosema, makadirio ni watu milioni sita, tukipima ardhi kwa watu wote hawa, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema nia yake ni nzuri kwenye hili, basi tutaweza kuona jinsi gani mapato tunayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko eneo hili la usimamizi na ufuatiliaji. Tutakubaliana hapa miradi mingi hata hii ya kimkakati bado *item* au *component* ya ufuatiliaji haipo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nivumilie dakika moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti ...

**MWENYEKITI:** Nina orodha ndefu Mheshimiwa. Uniwie radhi, ahsante sana.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Sima, Mheshimiwa Dkt. Pauline Nahato ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Utukufu aliyeniwezesha kusimama hapa leo. Jambo la pili niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ambao walinipa kura nyingi sana za kishindo zilizonisababisha mimi kuingia ndani ya Bunge na kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru chama changu cha Mapinduzi, lakini pia niishukuru familia yangu. Nasema ahsante sana wote walioshiriki kuniwezesha, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, lakini pia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja. Ili tuweze kujenga uchumi ni lazima tushirikishe uchumi wa viwanda pamoja na masuala mazima ya kilimo, bila kuhusianisha hivi vitu hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda unategemea sana sekta ya kilimo kwa asilimia 80. Kwa hiyo, vyovyote vile iwavyo lazima tuweke mkakati wa makusudi kuhakikisha kwamba kwenye eneo la kilimo tunakaa sawasawa. Ni lazima tuhakikishe kwamba pembejeo na zana za kilimo zinapatikana kwa urahisi ili kuweza kufanya mageuzi makubwa sana katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani nao pia kuanzia vitongoji, vijiji, kata, wilaya kwenda mpaka mkoa ni lazima kuhakikisha kwamba wanakuwa ni wale ambao wanaweza kwenda mpaka chini na kutoa mafunzo mazuri kuhusiana na masuala ya kilimo ili wananchi wetu waweze kufanya uwekezaji wa kilimo wenye tija. Badala ya hivi ilivyo sasa wananchi wanalima kiholela na wala udongo haupimwi kwamba kwa udongo huu sasa mnaweza kulima migomba

au pamba, wanalima tu kwa kubahatisha. Kwa hiyo, wataalam wakisimama makini kabisa na wakaweza kupima udongo ni imani yangu kwamba tutatoka hapa tulipo na tutasonga mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo na umwagiliaji. Nilidhani pia kwenye eneo hili tuhakikishe kwamba Serikali inaweka fedha nyingi katika kuandaa miundombinu ambayo itawezesha suala la ulimaji wa umwagiliaji ili wananchi au Tanzania yetu tuweze kuwekeza kwenye kilimo na tuweze kuvuna mara mbili kwa mwaka au zaidi. Hapo ndipo tutakapoweza kuviwezesha viwanda vyetu viweze kufanya kazi na viweze kuzalisha na hatimaye kuleta ajira nyingi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia suala la mbegu lizingatiwe. Nashauri Serikali ione namna gani itaweza kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie suala la masoko. Hivi sasa tunazungumza masuala ya kilimo lakini wananchi wanapokuwa wamevuna mazao yao masuala ya masoko ni kubahatisha, hawana masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumza hapa wale ambao wanazalisha mazao ya nafaka katika Nyanda za Juu Kusini ukiangalia zao la mahindi wananchi bado wana mahindi ya mwaka jana na yakakutana na mwaka huu. Kwa hiyo, ni wazi kwamba, mwananchi hapo hawezi kufanya uwekezaji wenye tija na wala hatuwezi kufikia malengo tunayoyatarajia. Kwa hiyo, nilidhani kwenye eneo hilo basi, liwekewe mkakati wa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Benki ya Kilimo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga Mheshimiwa, ahsante.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenikatili. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mussa Sima, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita ajjandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Nami nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema. Pia nikishukuru chama changu, niwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Singida Mjini kuniamini tena kwa mara nyingine ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijikite ukurasa wa 25 eneo ambalo linazungumzia kukuza ujuzi. Kulikuwa na Tume imefanya utafiti iliyokuwa inaitwa Tume ya Mipango mwaka 2014 ilifanya utafiti wa kuangalia hali ya soko la ajira nchini, lakini matokeo ya utafiti ule umeonesha iko tofauti kubwa ya uhitaji wa ujuzi kwenye soko lakini na ujuzi unaotolewa katika vyuo vyetu vya elimu ya ufundi. Wameenda mbali zaidi wakaamua kufanya *reference* kwenye nchi za wenzetu za China, India, South Africa na nyingine, lakini huko wamekwenda mbali sana walipaswa watueleze tulikwama wapi kabla ya kwenda kufanya *reference*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nieleze hapa, tulikuwa na vyuo vya kati (*FDCs*) ambavyo leo tumezi-*transform* kuwa *university*. Mtu anapopata *degree* unamuandaa kuwa *manager*, kuwa *administrator*, lakini hawezi kuwa mtu mwenye ujuzi ambaye anahitaji kusimamiwa, sasa tumehama kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri hapa na nitoe mfano. Naibu Waziri kule China, wenyewe wanaita *Vice Minister*, anaitwa Lu Xin, mwaka 2014 aliamua kwa dhati kuridisha *universities* 600 kuwa *polytechnic*. Sisi leo tunatoa hivi vyuo vya kati tumevipeleka kuwa *university*, kitu ambacho sio sawa lakini hatujachelewa. Nataka niombe Mpango huu sasa uamue vile vyuo vilivyokuwa vya kati vimekuwa *university*

virudi kuwa vyuo vya kati, tutakuwa tume-*solve* tatizo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Korea Kusini alikuwepo Rais anaitwa Park Chung-hee amefariki mwaka 1979 alikuja na mpango maalum, mpango huu aliamua wawekeze kwenye chuma. Korea Kusini *population* yake inafanana na sisi lakini ardhi yake asilimia 70 ni milima, asilimia 30 tu ndio wanayoitumia kwa makazi, lakini hawana *resource* yoyote, *resource* tulizonazo sisi hata hizo Asian *countries* hazina, sisi tunazo za kutosha sana; wakaamua kuwekeza kwenye chuma na chuma hiki wana-*import*. Sisi tuna Mchuchuma na Liganga kwenye Mpango haelezwi, hatuweki mkakati wa Mchuchuma na Liganga tunategemea kufanya mapinduzi gani ya viwanda? Tunategemea kufanya mapinduzi gani ya kilimo kama hatuwekezi kwenye chuma na chuma tunacho, wala hatuhitaji ku-*import* chuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niombe Serikali kwa nia njema kabisa, huu ndio wakati sahihi wa kutumia Serikali zetu kwa sababu uwekezaji mkubwa umefanyika na tunatumia vitu vya nje wakati sisi tunavyo ndani. Naomba tufanye mabadiliko kwenye eneo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri eneo moja dogo sana; leo kilimo chetu hiki wanaotuwezesha ni wakulima wadogowadogo na wanaofaidika na kilimo hiki ni makampuni makubwa. Lazima tutengeneze ukuaji wa dhana ya pamoja, *shared growth principle* na lazima tuwe na *authority* tutengeneze mamlaka ambayo itasimamia ukuaji wa dhana ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumaanisha nini? Makampuni makubwa ni lazima tuwe na mamlaka ya kuya-*control* kuyalazimisha yafanye biashara na makampuni madogo. Natoa mfano mdogo, leo nenda Lushoto, Muheza kote kule, matunda yanazagaa lakini Azam yule anaweza kuyanunua yale matunda yote na tukainua kile kilimo cha watu wetu wa chini. Nenda Singida kule leo alizeti inazagaa,

lazima aje mchuuzi ndiyo aweze kuuza alizeti, tunawezaje ku-*promote* hii *peasant economy*? Hapa ndipo tunafanya wakulima wetu wanafeli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, umefika wakati wa kuanzisha mamlaka itakayosimamia mikataba ya makampuni makubwa na kwa ajili ya makampuni madogo ili kuweza kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ajiandae.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitizama katika Dira ya Maendeleo ya 2025 pamoja na masuala mengi ambayo yameongelewa tunazungumzia juu ya elimu bora kwa wasomi wetu wa vyuo vikuu ili tuweze kupata Taifa bora lakini sasa katika elimu hiyo ya vyuo vikuu tunaona kwamba kuna maeneo ambayo tunatakiwa kuyazingatia. Eneo la kwanza ambalo tunatakiwa kuzingatia zaidi ni teknolojia ya ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kabisa kwamba kulingana na idadi ya wanafunzi ambao tunao katika vyuo vikuu vyetu mbalimbali, ili kuweza kuwafikia wanafunzi wote ni lazima teknolojia ya mawasiliano iboreshwe kwa sababu sio rahisi wanafunzi wote kukaa darasani kwa wakati mmoja. Bado eneo hili la elimu ya masafa marefu halijatiliwa mkazo na mfumo huu kimsingi ungeweza kupunguza gharama hata za ada kwa wanafunzi kwa kuwa wanafunzi hao wanaweza wakasoma hata wanapokuwa sehemu mbalimbali katika mikoa yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia upo umuhimu wa kuboresha ufundishaji kwa vitendo. Ukiangalia sasa hivi

tumeboresha zaidi kujenga majengo kama mabweni lakini katika ufundishaji wa vitendo, hususan katika fani ya sayansi na teknolojia, Serikali iweke kipaumbele katika kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana katika *university* zetu zote. Pia ipo haja ya kuhakikisha vyuo vinapanua uwezo wake wa kufundisha wanafunzi kwa kutumia teknolojia na uwezo ambao utaongeza wanafunzi kuwa wengi katika vyuo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna tatizo la motisha kwa wafanyakazi. Wafanyakazi wengi ambao wapo pale hawana motisha. Walimu wengi au wahadhiri hupandishwa madaraja lakini hawalipwi stahiki zao kwa wakati. Unakuta kwamba mtu anajitahidi kufanya utafiti lakini akishapandishwa daraja hapati pesa kwa wakati na hiyo huwafanya kukata tamaa sana hasa katika eneo la utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili linaenda sambamba na kuhakikisha kuwa wale waliopandishwa madaraja wanapata motisha ili uweze kuwasaidia. Mtu anakuwa labda ni *Assistant Lecturer* amekuwa *Lecturer* au amepanda cheo amekuwa Profesa unakuta anaitwa Profesa lakini mshahara haujapanda. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali kwamba iweze kuangalia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya motisha kwa wafanyakazi, hasa Wahadhiri, ni pamoja na kuangalia masuala ya maeneo wanayoishi kwa mfano hata kupewa *allowance* za nyumba, *allowance* za kufanya kazi kwa muda ule wa ziada ili waweze kufanya kazi kwa motisha na madarasa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaloweza kulishauri ni kwamba, sasa hivi Serikali imeongeza wanafunzi wengi sana katika vyuo vyetu na unakuta Mwalimu huyo anafundisha muda mrefu na anaweza akafundisha hata mara tatu kwa sababu wanafunzi wanaingia *session* tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nafikiri pia liangaliwe zaidi ni katika suala la hili *GPA*, unakuta kwamba

mwanafunzi amemaliza *degree* yake ya kwanza ana *GPA* nzuri lakini sasa hapati yale masomo ya kuendelea, anapofika *Masters* (Shahada ya Uzamili) anatakiwa apate *GPA* ya 4. Kwa hiyo haya masuala yote yaweze kuangaliwa ili katika elimu ya juu tuweze kutoa wanafunzi ambao ni bora na Walimu nao waweze kuwa katika mazingira mazuri...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo na Mheshimiwa Jafar Chege ajiandae.

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini kabla ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa afya hii njema hadi leo niko Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kiteto kwa imani kubwa na wamenichagua kwa kura nyingi sana. Nawaahidi kabisa kwamba nitawajengea heshima kubwa hapa Bungeni haijawahi kutokea. Vilevile nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuiteua na nikapeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kutoa maoni yangu kwa Mpango huu wa Maendeleo. Mpango wa Maendeleo ni mzuri sana na kwa kweli katika kupitia zipo taarifa kama tatu hivi ambazo ni kubwa kweli. Kwa hiyo, maoni yangu ya kwanza nafikiri kama hatutayatendea haki sana mapendekezo haya kwa siku zilizopangwa kama nne hivi. *Document* ya kwanza ina kurasa karibu 164; ya pili 51; nyingine 107. Sasa ukichanganya zote



na dakika tano hizi utajua kabisa kwamba pengine tungehitaji wiki mbili hivi za namna ya kuzungumza ili tuweze kuishauri Serikali vizuri sana katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda kuwa mchache, nijielekeze kwenye kilimo. Kilimo hapa tumeambiwa kwamba pato la Taifa ni 27% na kinawaajiri Watanzania zaidi ya 65%. Nimshukuru sana Rais kwamba mapendekezo ya maendeleo mwaka huu ni kuwekeza nguvu kwenye kilimo. Tukiwekeza nguvu kwenye kilimo na hususan mbegu zipatikane kwa wakati na kuwaondoa wakulima kwenye jembe la mkono na ku-*mechanize*, tutaweza kulikwamua Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano katika kuendeleza kilimo siyo tu yana tija kwenye uchumi, lakini vilevile na mahusiano makubwa sana ya kupunguza umaskini kwa Watanzania walio wengi. Kwa hivyo kwa kweli naomba Wizara ya Kilimo isilale katika hii miaka mitano, tuwekeze nguvu kubwa sana kwenye kilimo na kwenye mbegu, unajua nchi zile zilizoendelea sasa wana-*patent* hizi mbegu, kwa hiyo tusiwekeze tu kwenye kufanya utafiti, lakini pia tu-*patent* mbegu zetu ili tuweze kulinda masoko yetu huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwekeza kwenye kilimo, kwenye mifugo, kwenye uvuvi na tukaweka nguvu zetu zote huko tutakuwa tumeshughulika na vitu wanavyoita watu wengine *the really economies* kwa sababu ndiyo Watanzania wengi wako huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni umeme na ningemwomba sana Waziri wa Nishati anisikilize vizuri hapa, Hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa nane na nimeshamwandikia Mheshimiwa Waziri *memo* nyingi sana kuhusu suala la umeme. Nafurahi sana tumewekeza kwenye umeme na nawapongeza sana na Wizara wakati wanajibu maswali hapa walisema hivi, kwamba wamejiwekea miezi 18 kumaliza tatizo la umeme kwa vijiji vyote vilivyobaki. Hii ni ishara nzuri sana, lakini ni lazima sasa tuangalie umeme

tulionao, Mheshimiwa Rais alisema hivi na naomba ninukuu, ukurasa wa nane wa hotuba ya 2015; "Mheshimiwa Spika eneo lingine ni TANESCO, TANESCO pamekuwa ni suala la kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara na kuwepo na umeme wa mgao na hilo limelalamikiwa sana na wananchi wetu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto kwa miezi mitatu sasa umeme ni kukatikakatika halafu hatupati taarifa yoyote ile. Sasa wakati tunawekeza huko kutengeneza umeme, lazima sasa tuwe na uhakika wa umeme tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naunga mkono hoja lakini...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kengele imeshalia

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo atafuatiwa na Mheshimiwa Jafar Chege na Mheshimiwa Boniface Butondo ajiandae

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kusema kidogo kuhusu huu Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Nchi yetu. Nimepitia makabrasha yote ya Mpango huu na hotuba mbili za Mheshimiwa Rais, ya 2015 pamoja na hii ya mwaka 2020 ambayo tulisomewa tarehe 13 Novemba hapa wakati wa kuzindua Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhakika kabisa Mpango huu wa Tatu nina hakika utafanikiwa na unakwenda kutuina kwa viwango vya juu zaidi na kuboresha maisha ya mwananchi wetu. Hii inatokana na kwamba Mpango wa Pili wa Maendeleo pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ambao ulisimamiwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John

Pombe Magufuli, umefanikiwa sana kwa hali ya juu. Kwa mafanikio yale nina hakika kabisa kwamba Mpango huu unakwenda kuinua maisha yetu na utaboresha maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nita-*comment* kwenye maeneo mawili; miundombinu; tulishuhudia barabara zikijengwa, madaraja yakijengwa, lakini barabara zetu zikishamalizika kujengwa, kule zinakopita unakuta ukihama barabarani mita mbili tairi linazama. Kwa hiyo niruhusu nilishauri Bunge hili na Serikali yetu kwamba kuanzia sasa tutakwenda kujenga barabara nyingi sana ambapo tumelenga kujenga barabara kilomita 6,600 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi hiyo kila barabara itakayojengwa tufanye *extension* kwenye vijiji na kata ambazo zitakuwa zimepakana na zile na barabara kwa kiwango cha kilomita tano kila kijiji kiweze kufaidi. Hali hiyo niliweza kuiona kwenye nchi fulani nilikwenda kutembelea, nikaona kwamba ilifungua sana maisha ya wananchi ambao wako kwenye vijiji ambavyo vimepakana na zile barabara. Nikaona hilo jambo ni zuri na niishauri Wizara ya Ujenzi iliweke kwenye sera zetu ili barabara zote zitakazojengwa kuanzia sasa zifanye *extension*, zifanye matawi kwenda kwenye vijiji na tunaamini kwamba itafungua maisha na maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais alitoa ahadi nyingi sana, nishauri kipaumbele kipelekwe kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais. Hii itaondoa minong'ono ambayo nimekuwa naisikia mara kwa mara kwamba ooh ahadi za kisiasa tu, ahadi za kutafuta kura na kadhalika, lakini zile ahadi alizitoa mbele ya wananchi wengi kwa hiyo nashauri kwamba zipewe kipaumbele kwenye huo Mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia niseme kitu kwenye kilimo. Tangu nasoma kulikuwa kuna kitengo cha

umwagiliaji kule Wizara ya Kilimo, lakini mpaka leo bado hatujaweka nguvu kubwa kwenye umwagiliaji...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Shukurani sana kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Chege atafuatiwa na Mheshimiwa Boniface Butondo na Mheshimiwa George Malima ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza kupitia kitabu cha Mpango tunaoadili wa mwaka mmoja na miaka mitano ukurasa wa 13; nipende tu kusema ndugu zangu Wabunge wote twende pamoja, pamoja na kwamba tunajadili Mpango ambao uko mbele yetu, tujaribu kukumbushana tu kupitia ukurasa wa 13 yale mazuri ambayo ameyafanya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ili tunapokwenda kujadili twende sambamba pasipo kupotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, baadhi tu peke yake idadi ya kaya imeongezeka, zilizounganishiwa umeme zaidi ya 14.9% ndani ya miaka mitano (2015 mpaka 2020 Desemba). Vijiji vilivyounganishiwa umeme kutoka vijiji 2000 mpaka vijiji 10,000. Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji, juzi Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tunajadili hapa namna idadi ya wanafunzi walivyoongezeka mpaka madarasa yamepungua na mengine mengi ambayo ameyafanya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kwa hiyo tunapokwenda kujadili Mpango uliopo mbele yetu tunatakiwa tujadili yale mazuri ambayo yako mbele, lakini tujaribu kuainisha changamoto, namna gani sasa Waziri wa Mpango, Waziri aliyewasilisha Mpango huu aone namna

gani sasa anatoka hapa ili kwenda mbele kuyafanyia kazi yale mawazo yote ya Waheshimiwa Wabunge bila kubagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia hilo niende kujadili Jimbo langu la Rorya. Leo asubuhi tulikuwa tunajadili hapa Mheshimiwa Waziri alikuwa anajibu kuhusiana na hoja ya maji. Ndani ya Jimbo la Rorya, zaidi ya 77% imezungukwa na maji maana yake shughuli kubwa ya kiuchumi ukiacha shughuli ya kijamii ya maji, ni uvuvi. Mpango unasema kuna mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa zaidi ya dola milioni 500 ambao unatoka kwenye Jimbo la Rorya unakwenda Tarime, lakini kijiji ambacho unatoka jimbo ambalo unatoka huo mradi halijawekwa kwenye mpango wa utekelezaji wa hayo maji. Kwa hiyo, naomba sana, tunapojadili na tunapopanga mipango tuangalie namna gani inagusa wananchi kwenye maeneo ambao mradi unatoka ili kwenda maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ushauri wangu kwenye upande wa viwanda, natamani sana nimshauri Mheshimiwa Waziri upande wa viwanda, viwanda hivi ninavyovizungumza yawezekana visiwe vina mashiko sana hasa maeneo ya vijijini. Ningetamani sana Serikali ije na mpango wa namna gani ambayo itaanzisha viwanda ambavyo zinashiriki moja kwa moja kwenye shughuli za maendeleo za kiuchumi za kule ndani ya halmashauri, ikibidi waainishe mazao ya kibiashara ambayo yanatolewa kwenye halmashauri husika ili Serikali iwe na mpango wa kiwanda kulingana na zao la kibiashara linalozalishwa kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ukitoa tathmini ongezeko la viwanda, leo tunasema kuna ongezeko la viwanda zaidi ya 8,400, yawezekana kwenye maeneo mengine hicho kiwanda hakipo. Kwa hiyo, yawezekana ukisema kuna ongezeko la viwanda kuna baadhi ya maeneo haliwagusi moja kwa moja wale wananchi, maana yake watakuwa wanashabikia ule mpango, lakini hauwagusi wale wananchi wa chini kabisa ambao tunawawakilisha. Ningetamani kwenye hii mipango Serikali izingatie sana unapopanga mipango ya kuongezeka

viwanda, basi viwanda viwe moja kwa moja kwenye maeneo ambako kuna uzalishaji kwa wananchi hasa ukizingatia yale mazao wanayozalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nizungumzie sana upande wa uvuvi, mimi kama nilivyosema 77% ya jimbo langu inazungukwa na maji, shughuli kubwa inayofanyika kule ni uvuvi, lakini ndani ya miaka hii mitano iliyopita nyinyi wote mtakuwa mashahidi, wavuvi hawa hawana furaha kwenye maeneo yao. Ningetamani sana kama nilivyosema mara ya kwanza, Serikali ije na mpango wa namna gani itakaa na hawa wavuvi, ianishe na ione ni changamoto gani kubwa inawasumbua, kama shida ni nyenzo zile za uvuvi, wenyewe wanasema wanaponunua hakuna shida, ikija huku inakuwa na shida, Serikali ione namna gani inavyowasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningepomba Serikali kupitia Ofisi ya *DPP* iende ikaone wale wavuvi wadogo wadogo waliokamatwa kwa miaka mitano kwa makosa ya uhujumu uchumi ili iweze kuona namna gani inaweza ikawasaidia ili kuwaondoa, kwa sababu kuna wengine kimsingi mwingine hana hata fedha, lakini amekamatwa kwa makosa ya uhujumu uchumi. Kwa hiyo tuone namna gani kupitia Ofisi ya *DPP* inaweza ikawaona hawa watu na ikawasaidia kwa maana hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umeisha Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniface Butondo atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Kasinde na Mheshimiwa *Engineer* Isaack Aloyce Kamwelwe ajiandae.

**MHE. BONIFACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwa mara ya kwanza nasimama katika Bunge lako Tukufu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Spika na wewe Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuwa viongozi wetu katika Bunge hili Tukufu. Pia nitumie fursa hii kukishukuru Chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuiteua na kupeperusha bendera ya Chama changu Cha Mapinduzi na hatimaye kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa namna ambavyo wamenipa kura nyingi za kishindo kwa asilimia 87.4. Vile vile niwashukuru sana Wanakishapu kwa ujumla, lakini niishukuru familia yangu, kwa namna ya pekee nimshukuru mke wangu, lakini niishukuru na familia yangu kwa ujumla kwa namna ambavyo wamenipa ushirikiano kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata kura za ushindi na hatimaye kufika katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango katika Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka mmoja na miaka mitano. Kwanza nianze kwa kuishukuru sana Serikali yangu kwa jitihada kubwa ambayo imekuwa ikifanya. Sote tuna macho ya kawaida na hatuna macho yenye miwani ya mbao, kwa sababu yako mambo mengi ambayo dhahiri na wazi yamekuwa yakionekana ni mafanikio makubwa kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Elimu; sote tunafahamu elimu ya sekondari kwamba sasa hivi tuna sekondari katika kila kata na baadhi ya kata zingine tumeanza kuongeza sekondari. Pia shule zetu za msingi zimeboreshwa, ukilinganisha na hali halisi ya kipindi cha nyuma. Yapo mambo mengi vile vile kama vile ujenzi wa *Standard Gauge*, ambao sasa hivi unaendelea kwa kasi kubwa; uboreshaji wa huduma ya Shirika la Ndege. Shirika hili lilikuwa limekufa na sasa hivi maendeleo ni makubwa, sote tunanufaika na huduma hii ya usafiri wa anga; kuna mradi huu mkubwa wa ufuaji wa umeme wa Mwalimu Nyerere, ni

hatua kubwa ambayo Serikali yetu imewekeza na kufanya mradi huu unakwenda vizuri; na suala zima la uanzishwaji wa viwanda vikubwa, viwanda vya kati na viwanda vidogo. Hii ni hatua kubwa ambayo ni dalili tosha kwamba hatua ya kimaendeleo katika nchi yetu tunakwenda vizuri..

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi kwa sababu sisi siyo wananchi isipokuwa ni taasisi za kifedha za kimataifa ndizo zilizofikia hatua ya kuiona Tanzania inastahili kuingia katika uchumi wa kati. Kwa hiyo tupo *assessed* kwa utaratibu wa kitaaluma kabisa kabisa na ndiyo maana tumefika mahali tumeingia katika uchumi wa kati.

Kwa hiyo ni jukumu letu Watanzania kuweka mbele uzalendo ili mradi tuhakikishe uchumi wa kati lakini katika kipato cha juu, sisi wenyewe Watanzania kama wazalendo tuhakikishe kwamba tunapambana na tunakuwa wamoja kuhakikisha kwamba maendeleo ya uchumi wetu yanapaa inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie tu mafanikio haya yanaonekana kwenye Jimbo langu la Kishapu, huwezi ukaamini kwa miaka nane ya nyuma na huko nyuma zaidi *coverage* ya maji ilikuwa chini ya 20%, lakini leo tunavyozungumza nina Mradi mkubwa wa Maji ya Ziwa Victoria ambao kwasasa hivi *coverage* ya maji pale iko kwenye asilimia 50. Miradi inayotekelezwa baada ya miezi kama minane nina uhakika nitaweza kufikia *coverage* ya 70%. Hii ni hatua kubwa sana,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara zinazojengwa kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza haya nataka niseme kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Kassinge atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Isaack Aloyce Kamwelwe na tutamalizia na Mheshimiwa Assa Makanika.



**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa nafasi, lakini pia kwa sababu nachangia kwa mara ya kwanza, nami nitumie fursa hii kuanza kwa kumshukuru *Allah* Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala*, lakini pia kuishukuru familia yangu, wapigakura wangu wa Jimbo la Kilwa Kusini, pamoja na Chama changu Chama Cha Mapinduzi kilichonipa dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo naanza kuchangia nikianza na sekta ya viwanda. Sekta ya Viwanda katika nchi yetu ipo malighafi ambayo bado hatujaweza kuitumia na hapa nazungumzia malighafi ya gesi asilia. Katika Wilaya ya Kilwa eneo la Songosongo tunazalisha gesi pale ambayo inatumika kuzalisha umeme au kufua umeme, lakini mabaki yanayotokana na gesi asilia bado hayajaweza kutumika kwa ajili ya viwanda na hapa nazungumzia viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kupitia Mpango huu Kiwanda cha Mbolea Kilwa Masoko kitakachotokana na malighafi ya gesi asilia kiingie katika Mpango huu tunaenda kuutekeleza kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nije kwenye Sekta ya Kilimo; eneo mahususi ambalo tutawasaidia wakulima wetu ni kuhusianisha kilimo pamoja na Sekta ya Viwanda. Mosi, viwanda vya kuwawezesha wakulima wetu kupata mbolea kwa urahisi vianzishwe karibu na maeneo ambayo viwanda hivyo vitawasaidia wakulima kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyanda za Juu Kusini ambapo kwa kiwango kikubwa wenzetu ndiyo wakulima wakubwa wanaozalisha kwa ajili ya kulisha nchi na ziada mpaka tunaambiwa kwamba kuna chakula au mahindi yamebaki huko yamekosa soko, nashauri kupitia Mpango huu kuanzishwe kiwanda cha mbolea Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoani Njombe ambapo tayari wananchi wametoa eneo la kutosha. Kwa kufanya hivyo tutaweza kupunguza changamoto ya pembejeo ya mbolea katika msimu wa

kilimo. Wizara ya Kilimo itakuwa inapunguza kazi ya kutoa bei elekezi kwa sababu ya mbolea inayotokana na sekta binafsi, tukianzisha kiwanda pale tutasaidia Mikoa ya Njombe, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuna eneo la sekta ya uvuvi, Mpango unaelezea suala zima la uvuvi katika kuanzisha bandari za uvuvi lakini hii iende sambamba na masoko ya samaki. Wilayani Kilwa hususani Kilwa Kivinje ni miongoni mwa maeneo ya uzalishaji mkubwa wa sekta hii ya uvuvi ikiwa ni pamoja na Mafia.

Nashauri kupitia Mpango huu tuanzishe bandari za uvuvi Kilwa Masoko na Mafia na tuanzishe soko kubwa la samaki pale Kilwa Masoko kwa sababu nchi jirani na hususani Congo wanakuja kununua samaki tani kwa tani lakini Serikali hatujaweza bado kuratibu eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naunga mkono Mpango huu na nashauri upitishwe kwa mujibu wa mapendekezo tunayoyatoa Wabunge hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Isack Aloyce Kamwelwe, tutamalizia na Mheshimiwa Assa Makanika.

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na upendo hasa kwetu sisi Watanzania, kwa kutufanya tuendelee kudumisha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru uongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa kuendelea kuliteua jina langu ili niingie kugombea. Pia niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Katavi ambao

wamenirejesha kwa mara nyingine ya pili katika Bunge hili.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze sana Wizara ya Fedha kwa Mpango mzuri lakini nitoe ushauri kwa upande wa *TRA*. Mpango wa Pili wa Maendeleo uliweka makadirio ya kukusanya shilingi trilioni 107 na niipongeze sana *TRA* wamekusanya zaidi ya asilimia 80. Ni kazi nzuri hongereni sana lakini ni kwa sababu ya usimamizi mzuri wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hiyo katika miaka mitano imefanya kazi kubwa sana lakini ni imani yangu kwamba wangeweza kukusanya Zaidi. Kwa kuzingatia kwamba kwenye Mpango huu wa Tatu unaoanza mwaka 2021 kwenda 2022 matarajio ni kukusanya shilingi trilioni 114 kwa ajili ya kutekeleza mipango ya maendeleo kwa muda wa miaka mitano mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri *TRA*, ni lazima wadumishe uhusiano kati ya *TRA* kwa maana ya Serikali na wafanyabiashara. Wabunge wenzangu wamechangia kwamba wafanyabiashara watatu wanakwenda kununua bidhaa moja China lakini makadirio ya *TRA* yanatofautiana katika yale makontena matatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni rahisi na kwa bahati nzuri Serikali yetu imeshaweka mkongo wa Taifa, teknolojia ya kidigitali tunayo, tunaweza tuka-*transfer* fedha kwa kutumia teknolojia ya kidigitali. Badala ya wafanyabiashara kutembea na dola mfukoni kwenda China kununua bidhaa, kwa nini tusifanye benki *transfer*? Tukifanya benki *transfer* na rekodi zikawepo *TRA* ukadiriaji hauwezi kuchukua muda, tutakwenda haraka na mlundikano wa makontena ndani ya bandari unaweza usiwepo tena.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi navyoongea kuna watu wanakimbia mizigo yao kwa sababu analeta mzigo lakini makadirio yanakuwa makubwa kuliko ile fedha aliyonunulia

na ile mizigo inaendelea kurundikana bandarini. *TRA* wanayo sheria baada ya siku 14 wanatakiwa kuweka ule mzigo katika mnada lakini hilo halifanyiki. Niwashauri sana *TRA*, ili muweze kukusanya fedha nyingi tuwe na mahusiano mazuri. Niombe tu, ikiwezekana hata Bunge litunge sheria kwamba sasa manunuzi ya bidhaa kutoka nje lazima fedha ipelekwe kwa benki *transfer* badala ya kuweka mfukoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii miaka mitano, Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, kutoka ndege moja amenunua ndege sasa zimefika kumi na mbili...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Oooh! Muda umeisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. ISACK A. KWAMWELWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Assa Makanika.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuipongeza sana Wizara kwa kuleta Mpango huu. Nitajikita katika vipaumbele vitano vya mpango huu na nitajikita kwenye kipaumbele namba tatu ambacho kinasema, kukuza biashara na kipengele namba nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nijielekeze kushauri mambo kadhaa kwa ajili ya Mpango huu ambao

umekuja mbele yetu. Kwanza, nitazungumzia mpaka wetu wa Kongo na Kigoma. Mpaka huu kihistoria unaonyesha kwamba umekuwa na mchango mkubwa wa kukuza uchumi katika Mkoa wetu wa Kigoma na hata kwa Taifa letu la Tanzania. Hivi karibuni hali ya kibiashara Mkoani Kigoma imedorora na imekuwa ni ya chini sana kwa sababu mpaka ule umekuwa hauthaminiwi. Hii ni kutokana na sera za kiuchumi ambazo kwa kweli Serikali ikizifanyia kazi tunaweza tukatoka mahali hapa tulipo na kuelekea sehemu ambayo tunataka twende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisoma historia ya mpaka ule wa Kongo na Tanzania inaonesha kabisa mwaka 1986 mpaka 1993 kulitokea Mkuu wa Mkoa wa pale kwetu Kigoma, Mkuu wa Mkoa wa kumi kama sijakosea, alikuwa akiitwa Christian Mzindakaya. Mzindakaya alifanya mambo makubwa sana katika uongozi wake ambayo yaliweza kuitoa Kigoma mahali ambapo katika hali ya uchumi ilikuwa ni kwenye shimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye alifanya vitu vichache tu; alichokifanya ni kurekebisha baadhi ya sera za kiuchumi, mfano *visa fee* ya wa Kongo kuja pale Kigoma aliweza kuishusha, lakini akaondoa na usumbufu wa wageni ambao umekuwepo hivi sasa na unashusha uchumi katika mkoa wetu wa Kigoma. Hivi sasa Mkongo akitoka Kongo kuja Kigoma anasumbuliwa na taasisi nyingi, akiingia tu kidogo *TRA* atakuwa nyuma, akikaa kidogo hata Polisi atamfuata kwenye *hotel*. Jambo hilo limekuwa likiwachukiza na hatimaye linaweza kushusha uchumi wetu. Naishauri Serikali kwamba kwa kutumia tu mpaka wa Kongo tunaweza tukapata mapato makubwa sana na tukaweza kusaidia hali ya uchumi katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie zao la kahawa. Zao la kahawa linaweweseka sana na nimeweza kushauri hata hapo nyuma nimekaa na Naibu Waziri Kilimo nikamweleza, zao la kahawa linadorora kutokana na vyama vya ushirika tulivyonyavyo. Vyama vingi vya ushirika mpaka dakika hii havijawalipa wakulima pesa zao na hawa

wakulima wamewakopesha toka mwaka jana na wengine mpaka dakika hii wanawadai. Mfano pale jimboni kwangu kuna Chama cha Kalinzi Mkongoro kina wanachama 273 bado kinadai pesa zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hali inasababisha zao hili la kahawa na tena kahawa inayotoka Kigoma imeonesha inapendwa duniani kote. Kwa namna hii ambavyo tunalimbikiza madeni ya wakulima kwa kweli inashusha hali ya zao hili la kahawa na kusababisha kukosa mapato mengi kwa sababu zao la kahawa ni la tatu kwa kuingiza fedha kigeni hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na muda pia nigusie kipengele cha elimu. Ni kweli tunaandaa vijana wetu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuomba taarifa kwamba kwa leo Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwa michango ambayo mmeitoa katika kusaidia huo Mpango utakaotayarishwa uangalie mambo gani. Naamini Serikali imewasikia na itaenda kuyafanyia kazi mambo mengi na ya

msingi kabisa ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyapendekeza.

Ninalo tangazo moja hapa, wako wageni wetu ambao ni Umoja wa Wauza Nguzo Ghafi wanaitwa UWANGUTA na pia ni wasambazaji wa nguzo za umeme. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnawaona wazalendo hawa, hawa ni wadau wakubwa sana kwenye umeme tunaopigia kelele hapa. Hawa ndiyo wasambazaji wa nguzo, hata wale wasambazaji wengine wanauziwa na hawa. Tuwaongezee makofi kidogo wawekezaji wazito hawa. Karibuni sana na uzuri mmezisikia hoja nyingi hapa za umeme kwa hiyo na nyie mkzalishe nguzo nyingi ili zifike kila mahali ambako Wabunge wanahitaji umeme. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 10 Februari, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*